ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kateuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais

51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

57.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 2 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, karibuni tena katika shughuli zetu leo tarehe 2 Julai, 2012, poleni kwa kazi nyingi, mlikuwa kwenye semina nzito, ambapo hapana shaka mafunzo mliopata yatasaidia sana. Kwa kweli kulikuwa na mafunzo makubwa, muhimu ambayo ni mazuri pamoja na nidhamu ambayo inatawala Baraza hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, upigaji wa makofi usiokuwa na utaratibu si nidhamu nzuri. Wakati Spika anapoingia ndani ya ukumbi hakuna makofi ni kimya na wala si nidhamu. Kwa hivyo, tudumishe nidhamu ya Baraza pamoja na heshima ya Baraza.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 168

Ukosefu wa Miundombinu Mahsusi kwa Ajili ya Walemavu

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Kny: Mhe. Salma Mussa Bilal) – Aliuliza:-

Ni muda mrefu sasa watu wenye ulemavu wakiwemo wagonjwa hupata shida sana kuzifikia taasisi mbali mbali zikiwemo Wizara za serikali kwa kukosa miundombinu yenye usawa wa matumizi kama vile '*lift'* na '*rams'* ili kuweza kufikia maeneo wanayohitaji huduma mbali mbali.

(a) Mhe. Waziri, ni kwa nini wizara na taasisi nyingi hazina miundombinu mahsusi iliyojengwa kuwasaidia watu wa kundi hilo wanapofuata huduma katika majengo hayo?

(b) Kwa lengo la kuwasaidia watu hao naomba kufahamu ni wizara ngapi za serikali zenye miundombinu hiyo?

(c) Kwa wizara na taasisi ambazo hazina miundombinu hiyo, serikali imepanga mikakati gani na kwa kipindi gani kuhakikisha kwamba taasisi hizo ikiwemo Baraza la Wawakilishi zinafanya marekebisho hayo?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 168 lenye vifungu (a), (b), (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi, kwamba ni kweli taasisi na wizara nyingi hazina miundombinu kwa watu wenye ulemavu, ambapo hupelekea tatizo kubwa wanapofuata mahitaji yao katika taasisi hizo.

Hili limetokana kwamba Mkataba ambao unaoongoza Haki na Fursa Sawa wa Kimataifa juu ya Watu Wenye Ulemavu ni wa mwaka 2006, na kabla ya hapo uzingatiaji wa masuala hayo ulikuwa hautiliwi maanani na jamii.

Mhe. Spika, tayari hatua za awali zimeshafanyika kwa kuziandikia wizara zote kuhusu suala hili, ili kuwataka wanapojenga majengo yao wasisahau kuweka miundombinu itakayowaruhusu watu wenye ulemavu kuweza kufikia huduma hizo.

Kwa mfano, hivi karibuni tu Wizara ya Katiba na Sheria tumeiona imo katika mchakato wa kujenga jengo lake jipya. Tayari ofisi yangu imeshawapelekea barua ili kuwakumbusha kwamba jengo linalojengwa ni lazima liwe na mahitaji muhimu kama vile *lift*, utelezi (*rams*), choo maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu, milango mipana, *corridors* pana, vishikizi na kadhalika. Tuna imani kwamba jengo hilo litakapomalizika litakuwa limezingatia masuala yote muhimu ya watu wenye ulemavu.

Katika jitihada hizi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, imeteua Maofisa Waratibu katika kila wizara na taasisi za serikali kwa ajili ya kusimamia pamoja na masuala mengine, suala zima la kuhakikisha kwamba miundombinu inafikiwa na watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, baadhi ya taasisi zenye miundombinu hiyo ni kama Bodi ya Mapato, jengo la *ZSTC* Kinazini, Hospitali ya Mnazimmoja, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Hospitali ya Mwembeladu, Shirika la Bima na Mfuko wa Barabara.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wote hao kwa kuhakikisha kwamba wametekeleza suala la kuwa na miundombinu ya watu wenye ulemavu kuweza kuwafikia.

Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, itaendelea kuwakumbusha wizara na taasisi hizo zizingatie suala hilo. Vile vile Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu, litaendelea kufanya ziara za mara kwa mara katika taasisi hizo ikiwa na lengo la kuwahamasisha juu ya masuala mengine ikiwemo na miundombinu.

Hata hivyo, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itashirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati juu ya suala hilo hasa katika kuwabana wanaokwenda kinyume na Sera na Sheria, na hata ikibidi kuwashawishi wizara hiyo kuangalia tena Sera inayohusu Majenzi na Majengo katika kuzingatia mahitaji muhimu kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, nakuomba sana kupitia Baraza lako hili tukufu, naomba tena tuweze kulifanyia marekebisho jengo lako hili la Baraza la Wawakilishi, ili angalau iwepo *lift*, kuwe na choo maalum cha kutumiwa na watu wenye ulemavu kuwepo na utelezi (*rams*), vishikizo mbele ya jengo hili pamoja na mahitaji yote muhimu, ili watu wenye ulemavu waweze kulitumia vizuri kama wananchi wengine. Nakushukuru.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi asubuhi ya leo kuweza kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika mchakato wa kutafuta *Tender* kwa Wakandarasi, je Mhe. Waziri wanakuwemo watu wenu wa Wizara kwa ajili ya kutoa ushauri endelevu kwa lengo la kupatiwa hawa walemavu miundombinu yao kama vile *lift* au vigari vya kusukumiwa?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ofisi yangu kwa kuona mapungufu ambayo yalikuwepo awali ndio kama nilivyojibu katika swali mama kwamba tumeanzisha Maofisa Waratibu wa kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu katika kila Wizara na taasisi, ili kusimamia na kuona kwamba shughuli zote za maendeleo zinawahusisha watu wenye ulemavu.

Nam. 125
Kuziba kwa Mtaro wa Saateni

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-
Mara nyingi zinaponyesha mvua kubwa kuna baadhi ya maeneo hujaa maji na kuathiri makaazi ya watu. Kwa kuwa bwawa la Sebleni maji yake yalikuwa yakimwagikia upande wa Kaskazini kupitia Amani Fresh kuelekea Saateni ambako mtaro huo umeziba.

Je, serikali itafanya juhudi gani ya kuzibua mtaro huo bila ya kuathiri makaazi ya watu wa Amani Fresh, Kwamtipura na maeneo ya jirani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 125 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana kabisa na Mhe. Mwakilishi kwamba mara nyingi wakati wa mvua kubwa zinaponyesha kuna baadhi ya maeneo hujaa maji na kuathiri makaazi ya watu ikiwemo mtaa wa Sebleni. Serikali inaelewa tosha tatizo hili la kujaa maji katika bwawa la Sebleni pamoja na tatizo la mtaro wa maji ya mvua katika eneo hilo.

Hali hii Mhe. Spika, imetokana na mtaro unaopokea maji hivi sasa kuwa na uwezo mdogo wa kutoa huduma hiyo.

Serikali inakusudia kujenga mtaro mkubwa ambao utakaochukua maji ya mvua hadi pwani. Ujenzi wa mtaro huo ambao utakuwa na urefu wa zaidi ya kilomita mbili utaanzia Magogoni kupitia maeneo tofauti na utachukua maji ya bwawa la Sebleni. Mhe. Spika, ujenzi wake unatarajiwa kuanza mara baada ya matayarisho ya mradi kukamilika ndani ya mwaka huu kupitia ule mradi wetu mkubwa wa *ZUSP* au Mradi wa Kuimarisha Mitaro ya Kupitia Maji ya Mvua Mjini.

Mhe. Spika, naomba nitoe na nimuombe sana Mhe. Mwakilishi awashauri wananchi wetu kwa nia njema tu wasijenge karibu na zile fukwe za mto au ziwa la Sebleni, kwa sababu mvua haziaminiki na zinakuja wakati wowote na zinapokuja zinaathiri nyumba zao. Kwa hivyo, tujitahidi tusijenge pembezoni mule mwa ziwa la Sebleni. Ahsante.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba utajengwa mtaro mkubwa ambao utatoka Magogoni mpaka kumwaga maji sehemu ya baharini.

(a) Je, ni lini kazi hiyo itaanza?
(b) Kama itanyesha mvua kwa sababu hivi sasa tunajua kwamba tuna mabadiliko ya tabia nchi na hata miongo haiendi vizuri, kwa sababu serikali ni kama kiumbe ana macho na masikio. Kwa nini kama serikali isiwe wao wanasimamia zaidi kuwa watu wasijenge kwenye maeneo yale pale, ili wasipate yale matatizo ya kujaa kwa maji kwenye nyumba zao?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya bajeti kwamba mwanzoni mwa mwaka huu na tokea mwaka jana kulikuwa na matayarisho ya mradi huu.

Matayarisho yenyewe kwanza kutafuta wasimamizi, halafu kutafuta *tender* na kwa taratibu za *World Bank* hayo ni mambo muhimu sana, na wala huwezi kuyaruka na kama si hivyo utakiuka zile taratibu zao. Kwa hivyo, utaziona hizi taratibu zinachukua muda mrefu, lakini ndio utaratibu wao.

Mhe. Spika, tunashukuru *Alhamdulillah* kwamba kazi hiyo tayari tumeshaifanya, sasa wanatafutwa wakandarasi na baada ya kupatikana wakandarasi kazi hiyo itaanza mara moja.

Kwa kweli kwa muda mrefu sana mtaro ule na mimi naukumbuka sana, na mara ya mwisho nakumbuka ile barabara ya katikati inayovuka kutoka Sebleni kwenda upande wa pili ilivunjwa na kuwekwa *culverts* kubwa kwa lengo la kutanua, ili yale maji yanayotoka ziwa la Sebleni. Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwamba hivi sasa umeziba na tutajitahidi kuufukua kwa muda kwanza.

Upande wa pili wa swali lake kuhusu wananchi, hili naomba tushirikiane na wala si kama suala la serikali peke yake. Kwa hivyo, kama ni Mwakilishi, Diwani, Sheha, basi naomba tusaidiane tufuate zile taratibu na mipango ya miji, ili wananchi wasijenge pembezoni kama alivyosema hali ya hewa pamoja na tabia nchi haziaminiki, hivyo ni vyema tujaribu kuepuka kabla ya athari.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujenga mitaro ni kupunguza maji katika mji wa Zanzibar na kuweka usafi katika mji wetu. Lakini katika mitaro hiyo inayojengwa pembezoni au juu ya mitaro mnakuwa na vidaraja ambavyo inakuwa ni njia za kupitia wananchi baina ya upande mmoja na mwengine.
Kwa bahati mbaya kipindi kilichopita niliuliza swali humu, na nilimwambia Mhe. Waziri kuhusu kujenga kidaraja ambacho kiko Kwamtipura tena ni njia kubwa ya wananchi wanapita. Mhe. Waziri alituahidi kwamba vidaraja

hivyo vitashughulikiwa, lakini hadi leo hii ninavyozungumza ni mwaka wa pili vidaraja vile bado havijajengwa na viko juu ya hiyo mitaro ambayo inapitisha maji tena ni njia kubwa.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri hivi sasa kumejengwa msikiti katika kidaraja hicho ambapo Waswalihina wanaotoka upande mmoja na wale wa upande mwengine wote wanataka waende msikitini, sasa wakati mvua inaponyesha njia inakuwa hakuna hata hiyo ya kwenda msikitini.

Je, ni kitu gani Mhe. Waziri kimemkwamisha kujenga vidaraja hivyo hadi leo?

Je, kwa sababu namkumbusha tena kwa mara ya pili, ni lini atachukua hatua ya kujenga kidaraja hicho, ingawa alituahidi kwamba atakijenga?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa bahati nzuri Micheweni hakuna mto anaovuka Mhe. Mwakilishi. Lakini hata hivyo kwa kumjibu swali lake, kwamba Mhe. Mwakilishi viko vidaraja vilivyojengwa, lakini sikujua pengine ulikusudia wapi hasa *specifically* ambapo tujenge.

Kwa hivyo, mimi sikatai na ninaomba tukitoka namuahidi tena Mhe. Mwakilishi na siku zote humwambia Mhe. Subeit Khamis Faki aniamini, na aniambie hivyo vidaraja ambavyo anataka vijengwe basi tutavishughulikia na wala hakuna matatizo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri alisema kwamba watajenga mtaro mkubwa sana kupitia mradi wao mkubwa, ambapo mtaro huo utakuwa ni kutoka Magogoni mpaka pwani. Je, Mhe. Waziri uko tayari kutuambia mradi huo unagharimu kiasi gani na kama hakujua haoni kama atalidanganya Baraza hili?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza namuomba sana Mhe. Mwakilishi kwamba sisi hatuna lengo la kulidanganya Baraza na wala hatuthubutu, labda pengine baadhi ya *statement* zetu ikiwa kidogo si barabara basi isichukuliwe kwamba tunalidanganya Baraza aa! Hatuna nia hiyo, isipokuwa nia yetu safi kama aliyonayo Mhe. Mwakilishi. *(Makofi)*
Kuhusu mradi nakumbuka tumeshazungumza mara nyingi hata kwenye kitabu chetu cha Wizara ya Fedha kuwa uligharimu Dola za Kimarekani milioni 57. Sasa Mhe. Mjumbe anaweza ku-*convert*, lakini kama kuna wasi wasi kidogo, basi ajaribu kuangalia hiyo *figure* na kwenye kitabu cha bajeti cha mwaka jana, mwaka huu mpaka cha Wizara ya Fedha imo hiyo *figure*. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 42

Kukimbia kwa Wataalamu

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara hukimbiwa na wataalamu wake kama vile *Professors*, *Lecturers* pamoja na stahiki mbali mbali za utumishi wanazowalipa wataalamu hao.

Je, ni hatua gani zilizochukuliwa na SMZ za kimaslahi katika kuwadhibiti wanataaluma hao wasikimbie.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa nchi nyingi zilizoko kusini mwa Jangwa la Sahara hukimbiwa na wataalamu wake hususan Madaktari, wakiwemo pia *Professors* na Wahadhiri katika baadhi ya maeneo, pamoja na stahiki mbali mbali za utumishi wanazolipwa wataalamu hao.

Mhe. Spika, sababu zinazowafanya wataalamu hao kukimbia nchi zao ni nyingi, ikiwa ni pamoja na kufuata maslahi na stahiki nono zaidi ya zile ambazo walizokuwa wakipatiwa na nchi zao. Lakini wapo ambao pamoja na kupatiwa marupurupu na stahiki na nchi zao bado wanakimbia kutokana na kukosa Uzalendo.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-
Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kuwajengea matumaini wataalamu wetu wasikimbie ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- Mwezi wa Oktoba, 2011 serikali imenyanyua maradufu mishahara ya wataalamu wetu ilingane au kukaribiana na mishahara inayolipwa na wataalamu wa nchi za jirani, ili wataalamu hao waendelee kubaki katika utumishi wa SMZ na kuendelea na kazi kuliko kukimbilia sehemu nyengine za ndani au nje ya nchi.

- Kwa upande wa madaktari kada ambayo kwa hapa kwetu Zanzibar hukimbiwa sana, tumeanzisha tena posho mbali mbali zikiwemo *on calls allowances*, pamoja na posho la mazingira hatarishi. Aidha kuanzia mwaka mpya wa fedha Julai 2012/2013 Miundo ya Utumishi mipya itaanza kutekelezwa pamoja na kutoa tena nyongeza za mishahara kwa wafanyakazi wa wizara zote na kwa mujibu wa tarehe zao za nyongeza hizo za mwaka.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika maelezo yake ameeleza pamoja na kuwa wafanyakazi wengine wanapatiwa maslahi ya kutosha, lakini bado huwa hawabakii katika nchi.

(a) Kwa vile Tanzania Bara ni moja kati ya nchi mbili zilizofanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivi sasa madaktari wanagoma, tuseme mgomo huu kwa madaktari wote unasababishwa na nini?

(b) Ni kitu gani hasa kilichofanya wafanyakazi hawa walioko kusini mwa hii Afrika na isiwe kaskazini kuwa na mpango wa namna hii wa kukimbilia nchi nyengine kwa ajili ya kutafuta maslahi zaidi?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, mgomo wa madaktari Tanzania Bara unasababishwa na nini kwa kweli sifahamu, kwa sababu sijapata kushiriki katika kuzungumza na madaktari hao waliogoma wa Tanzania Bara. *(Makofi)*

Kitu gani kinachosababisha wataalamu kuondoka nchini. Mhe. Spika, nilieleza mwanzo sababu zinazosababisha wataalamu wetu kuondoka nchini, ni zile za kuona kwamba hawalipwi maslahi makubwa kuliko zile nchi ambazo wanakimbilia.

Lakini sababu nyengine ni ile kama nilivyosema katika swali langu mama ni ukosefu wa uzalendo, hasa tukizingatia kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka jana tumehakikisha kwamba tunaanza zoezi la kuweza kuwalipa vizuri wataalamu wetu wa hapa Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri hivi majuzi madaktari wetu wa Zanzibar waligoma wakidai posho zao, *risk allowances* pamoja na posho za nyumba.
Je, muda mrefu wanaambiwa mambo yao yanashughulikiwa, unatoa kauli gani kwa madaktari hao?

Vile vile na baadhi ya madaktari wanapokwenda likizo huwa hawalipwi posho zao za kilizo, una kauli gani Mhe. Waziri kuhusu hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza nataka kukataa katakata kwamba madaktari wa Zanzibar hawajapata kugoma. *(Makofi)*

Lakini Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Fedha tulichukua juhudi ya kukaa na viongozi au wawakilishi wa madaktari hawa pamoja na uongozi wa Afya kwa zile stahiki ambazo waliona kwamba hawajapatiwa.

Mhe. Spika, tayari suala hilo tumeshalitekeleza mwezi wa Mei wameanza kulipwa zile posho ambazo walikuwa wanadai madaktari, na mambo mengine yatafuatia kwenye bajeti ijayo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wizara na taasisi mbali mbali zinaajiri wataalamu wenye viwango tofauti vya elimu, na wengine huwa wanajiendeleza ndani ya kazi.

Ni kwa nini hutokezea pengo kubwa la kimshahara au kimaslahi baina ya wataalamu walio sawa na wale wanaopata nafasi ya kuteuliwa sehemu mbali mbali na Uteuzi wa Rais, kwa nini inatokezea hivyo?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba taasisi mbali mbali huajiri wataalamu, lakini kwa vile mwenyewe amekiri kwamba hivi sasa wataalamu wenye sifa zinazolingana wanalipwa viwango sawa kwa hapa Zanzibar, kutokana na yale marekebisho yaliyofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mwaka jana. Wataalamu wote wanaolingana sifa zao wanalipwa kima sawa cha mshahara inategemea ule utaalamu uko katika kada gani.

Lakini kwa nini wataalamu hupishana na viongozi wa taasisi wanaoteuliwa na Mhe. Rais, ni kwamba kuna mazingatio maalum ya kuwalipa wataalamu kwa mujibu wa sifa pamoja na *scheme of service* inayotayarishwa na wizara yangu, kuna viwango maalum.

Pamoja na hayo, katika kuwalipa wateuliwa na wanasiasa nako kuna vigezo maalum. Kwa hivyo, kwa vyovyote vile haiwezekani kumlipa mtaalamu na kumlipa mtu ambaye anateuliwa na Rais.

Kwa mfano, mtu mwenye *Master Degree* madhali ameteuliwa, basi bila ya shaka anacholipwa maslahi yake ni kile cheo ambacho ameteuliwa, na yule analipwa kwa mujibu wa utaalamu wake, na ndio maana mtaalamu yule anaporudi anabakia na mshahara ule, lakini kwa kuzingatia ule utaalamu wake
kuna mambo mengine pale ambayo anayapata kwa wakati ule inabidi ayaache kwa sababu ule uteuzi anakuwa hanao tena.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Suala langu halikujibiwa nilivyouliza. Niliuliza kwa nini kuna pengo kubwa, sikuuliza kuna tofauti, kuna tofauti kubwa sana baina ya wataalamu walio sawa katika kazi, lakini mmoja akateuliwa na Rais kwa nafasi yake kuna tofauti kubwa sana, anaweza akamlipa yeye mara tano yule aliyeteuliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, mimi nadhani nimejibu, tofauti niliyoisema yule ni mteuliwa wa Rais na huyu ni mtaalamu, sasa lugha nyengine ya kiarabu siijui lakini kitumbatu ninajua.

Nam. 84

Ubovu wa Madaraja Kaskazini Unguja

Mhe. Kazija Khamis Kona: Aliuliza:

Kwa muda mrefu sasa, madaraja katika njia ya Kaskazini Unguja yako katika hali mbaya sana, kiasi cha kukwamisha shughuli za kiuchumi za wananchi wa Mkoa huo pamoja na kuhatarisha maisha yao. Mifano hai ni madaraja ya Kitope, Mto mchanga, Kinyasini na Chaani.

a) Je, Mhe. Waziri unalieleza nini Baraza hili tukufu kuhusiana na tatizo hili.
b) Ni lini hasa madaraja haya yatafanyiwa matengenezo makubwa au kujengwa upya kwa maslahi ya Taifa hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 84 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, barabara ya Malindi kwenda Mahonda, Kinyasini mpaka Mkokotoni unapita Donge na kurudia Mahonda ni miongoni mwa barabara zinazoingia katika mradi wa barabara zinazoingia mjini yaani *Zanzibar town entry roads*, ambazo zitafanyiwa matengenezo makubwa ya upanuzi pamoja na ujenzi wa madaraja yakiwemo yale aliyoyataja Mhe. Mwakilishi. Upembuzi yakinifu na sadifu yaani *feasibility study and detail engineering design* ya

mradi huo wenye jumla ya kilomita 77.965 ambao umefadhiliwa na Benki ya Dunia ambapo jumla ya dola milioni moja laki moja na ishirini zimetumika kumlipa Mhandisi Mshauri kwa kazi za maandalizi ya michoro na nyaraka za zabuni yaani *tender documents*, tayari Mhandisi Mshauri Kampuni ya *Inter Continental Consultants and Technocrats Pvt. Ltd (ICT)* ya India kwa kushirikiana na kampuni ya *Apex /Engineering CSo. Ltd* ya Tanzania wameshawasilisha Wizarani draft final design report kwa kutoa maoni yetu.

Barabara nyengine zitakazonufaika na mradi huo ni barabara za Muembeladu hadi Amani, Kariakoo - Mwakwerekwe, Tunguu nyengine ya Amani hadi Kiembesamaki na Mnazimmoja hadi uwanja wa ndege. Serikali itatafuta ufadhili kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo ambazo zitaanza mara tu baada ya kupatikana kwa fedha za ujenzi huo. Gharama za ujenzi huo inakisiwa kuwa ni USD 122.31milioni sawa na shilingi 195.70.

Kwa hivyo Mhe. Spika, madaraja hayo pamoja na barabara hizo zitajengwa mara tu fedha zitakapopatikana.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza Mhe. Naibu Waziri nilimuuliza swali langu kuhusu madaraja, kwa sababu madaraja yale yapo chakavu sana na yanaweza kuhatarisha maisha ya wananchi wetu. Sasa ninamuomba Mhe. Waziri kumuuliza swali langu kama hivi ifuatavyo. Je, Mhe. Waziri kwa kuwa huo mradi na ndio kwanza mnaupanga haujakamilika je, wizara yako itachukua hatua gani ya dharura kuyatengeneza madaraja yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Kazija Khamis Kona swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kwamba madaraja haya kwa kuanzia na la Kitope, Mahonda mto mchanga, Kinyasini, Chaani ni miongoni mwa madaraja ambayo yamekuwa machakavu na ni ya muda mrefu. Lakini kama Wizara ya Miundombinu tumekuwa na desturi ya kuwafanyia ukarabati kila hali inaporuhusu. Na nadhani katika mwaka huu uliokwisha wa 2011 tuliweza kufanya ukarabati katika madaraja hayo yakiwemo ya Kitope na Mtomchanga, lakini kwa bahati mbaya sana na katika hali ambayo inasikitisha sana tulijaribu kuweka mawe yale ambayo tunaita *koni* tukaweza tukaya-*paint* pamoja na kufanya ukarabati wa madaraja yale tukaweka na vyuma pembeni. Katika hali ya kusikitisha sana wananchi wa maeneo husika wamekwenda kukata vyuma vile. Sasa sababu mimi ninachoomba kwamba sisi kama Wizara tutaendelea kuyafanyia ukarabati madaraja yale ili kunusuru wananchi na watumiaji wengine wa barabara.

Lakini pia naomba nitoe wito kwa wananchi wanaokaa maeneo yale watusaidie kulinda hasa miundombinu yetu yanayohifadhi na kuimarisha madaraja hayo kwa ajili ya kutoa huduma kwa watumiaji wengine wa barabara.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa idhini yako ninaomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa kuwa Wizara ya Miundombinu inapenda sana kujenga miradi yake kwa kutumia nadharia *design and building*, ni nadharia ambayo wazanzibari hawaikubali na wanaona ni upotezaji wa fedha, je madaraja haya ambayo ni mabovu pia wanakusudia kuyapeleka katika nadharia hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuna miradi mingi tunayoiendeleza, na katika miradi yetu ni mradi mmoja tu ambao tunajenga kwa mfumo huu wa *design and building* nao ni mradi wa uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume. Lakini Mhe. Spika, tumeweza kufanya ujenzi wa madaraja mengi pasi na kutumia mfumo huu, hivyo ni imani yangu kwamba madaraja haya nayo tutayajenga kama tulivyoweza kujenga madaraja ya Mwera, Maji Mekundu, Mwanakombo, Mkokotoni pasi na kutumia mfumo huo. Ninamuomba tu Mhe. Mwakilishi ajenge imani utaratibu huu ni mzuri uliopo na tutauendeleza.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Naibu Waziri katika jibu lako umesema kuwa mmetengeneza mawe yanaitwa koni je Mhe. Waziri huoni kutengeneza mawe yale ni kuipa hasara serikali? Lakini pili je huoni iko haja sasa hivi kutengeneza matuta karibu na daraja yenyewe kuokoa ajali zisiwe nyingi?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Mwakilishi wa Jimbo la Kitope swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, katika utoaji wa huduma za barabarani lazima Zanzibar ikubaliane na iendane na sheria za kimataifa kwa kutambua kwamba watumiaji wa barabara sio tu watakuwa wazanzibari lakini watakuwa ni pamoja na wageni wote watakaokuja kutembelea nchi yetu. Kwa msingi huo uwekaji wa koni ule ni miongoni mwa taratibu zinazokwenda kimataifa na haukuwa utashi wetu. Hivyo kutengeneza koni zile haukuwa mzigo kwa serikali isipokuwa ni kuendana na sheria na taratibu za utumiaji wa barabara.

Suala la matuta Mhe. Spika, tumelizungumza kwa kina na kwa mapana ni sababu zipi zinazofanya tuweke matuta na sababu zipi zinazofanya tusiweke matuta, lakini nimuombe tu Mhe. Mwakilishi kama ana *concern* yake basi aje Wizarani tutakutana na wataalam tutalizungumza.

Nam. 135
Ufutwaji matokeo ya kidato cha IV Zanzibar

(Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 170
Vikundi vya Ushirika Zanzibar

Mhe. Salma Mussa Bilali: Aliuliza:-

Serikali imekua ikihimiza na kuhamasisha wananchi wake kuanzisha vyama vya ushirika ili waweze kujisaidia kimaisha. Jitihada hizo zimezaa matunda kwa vile wajasiri amali wengi wamejitokeza kuanzisha vikundi vingi sana.

Kwa upande mwengine Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika bado haijajipanga vizuri kukabiliana na huduma kwa vikundi hivi. Kumekuwa na tatizo la kuhamahama kwa Ofisi, hii imesababishwa na kukosa jengo la kudumu. Aidha watendaji wanakosa vitendea kazi vya kutosha. Kufuatia kadhia hii wananchi wanaendelea kila siku kusumbuka kufuatilia huduma za ofisi zenye kuhamahama na wengine kurudi kwa kutojua Ofisi ilipo.

Je, ni lini Serikali/Wizara itaipatia Idara ya Vyama vya Ushirika jengo la kudumu ili iweze kupata utulivu wa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-
Ni kweli Idara ya Ushirika imekuwa ikihama kutoka eneo moja hadi jengine. Hii ni kutokana na mabadiliko ya Wizara ambayo yamekuwa yakifanyika, walianzia Ofisi ya Waziri Kiongozi, baadae Wizara ya Kilimo na sasa hivi wako Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Mhe. Spika, kwa taarifa ya Baraza lako tukufu Mheshimiwa naomba niwahakikishie sasa hivi Idara hii ipo katika maeneo ya Amani kwenye eneo la viwanda vidogo vidogo. Na *inshaallah* mipango iko mbioni katika kuhakikisha kwamba jengo letu litakapokamilika la Wizara ya Kazi basi watahamia hapo kama ni sehemu yao ya kudumu.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri wa Uwezeshaji. Mhe. Waziri kwa kuwa jengo hilo la Viwanda Vidogo Vidogo walilohamishiwa hao Idara ya Ushirika ni chakavu na bovu, na wakati wa mvua huwa linavuja. Je Wizara yako ina mpango gani wa kulikarabati jengo lile au kuwapatia jengo jengine ambalo ili kuweza kunusuru uharibifu wa vifaa na nyaraka za Idara hiyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, hivi sasa hatuna mpango wa kuhamia eneo jengine isipokuwa tutakalofanya ni kufanya ukarabati angalau kwa kiasi ambacho vile vifaa havitoendelea kuharibika pale.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 –
Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nirudie tena kukumbusha hasa mafunzo ambayo tumeyapata jana, tunapanga *points* zetu vizuri na tunakwenda moja kwa moja kwenye mada iliopo na tunajitahidi kutorejea kama inavyokatazwa na Kanuni.

Wachangiaji tumepokea wengi kiasi na tunategemea michango tuimalize leo, na kesho mapema asubuhi tufanye majumuisho. Kwa hivyo, tuendelee na mchangiaji anayefuata baada ya Mwenyekiti ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadaye anafuata Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa baraka hii ya leo ya kuweza kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
Mhe. Spika, nikushukuru wewe sana leo kusikia sauti yako inatoka vizuri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akubariki na uendelee na hali nzuri hiyo kama wenzangu wanavyokusifia kukosa wewe kuja Barazani, basi Baraza linakuwa halinogi. Kwa hivyo, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akujaalie uendelee kupona na uwe na afya yako nzuri sana Mhe. Spika, lakini mazoezi mimi na wewe ni muhimu tufanye. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sitaki nipoteze muda wako, lakini kwanza nitaanza na maswali mawili tu ambayo ndiyo yatakuwa ufunguo wa mkutano wetu huu wa leo. Swali langu la mwanzo ambalo nimeliona nililete kabla ya kufika kwenye ukurasa wenyewe, na juzi tu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alilijibu vizuri sana, lakini sikupata wasaa wa kuweza na mimi kulifafanua na kuleta utamu na ufanisi wake na nini nilichokuwa nimekikusudia.

Mhe. Spika, nilitoa ushauri wangu ambao ni mzuri wa kitaaluma kabisa, tena wa kidiplomasia na hasa katika Mafunzo uliyotupa wewe Mhe. Spika chini ya UNDP, basi nilitoa ushauri ule wa kuleta ufanisi na hasa katika hali ambayo tunayokwenda nayo huku mbele katika mchakato wa Katiba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niliomba sana mimi kwamba hivi sasa ipo haja ya kuweka Wizara ya Vikosi peke yake, tena ninazo sababu zangu Mhe. Spika. Kwa kweli sababu hizi juzi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alinijibu kuwa sisi tunapiga kelele wizara nyingi, lakini Mhe. Spika tukiziondoa wizara mbili kati ya Kilimo na Uvuvi na kuifanya iwe moja basi hapo haijaondosha ile sura na itakuwa tumepunguza. Sasa tukizichanganya zile ndipo hapo tutakuwa na uwezo wa kuiweka hiyo Wizara ya Vikosi.

Mhe. Spika, vikosi tunavidharau na wala hatuvipi heshima yao ya kiaskari. Lakini tukiwa na wizara yao basi itajengeka ile sura ya heshima ya sura ya vikosi tena ni nzuri tu, hasa hata ukiangalia mazingira ya vyeo. Kwa mfano, leo Kanali wa JKU ana vyeo vitatu kwa mtu mmoja yule, lakini kwa kuwa ana jina moja, kwa sababu ameteuliwa na Rais anakuwa ni mmoja tu.

Sasa tukiweka wizara maalum hata vile vyeo vitabadilika. Katika kikosi kimoja ambacho utaona mazingira ya kubadilika kwenye vyeo vyao ni Kikosi hichi tu cha KMKM ambacho kuna *special rank* kinaitwa *Commodore,* hawezi kuvaa mtu mwengine yeyote ile kidogo ndio imeleta sura nzuri, lakini vilivyobakia vyote Mhe. Spika mtu anakuwa na vyeo vitatu na wala humjui *brigadier* nani.

Kwa hivyo, hilo nimeona nitoe salamu za kuweza kufikisha Mhe. Waziri alione kwa makusudi kwamba bajeti inayokuja aniletee sura hiyo, kama si hivyo nitazuia kifungu.
Mhe. Spika, la pili katika kuchangia kwangu kitu kikubwa katika wizara hii hivi sasa tulilie kitu amani, ili tuijenge katika sura nzuri ya Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kupitia wizara hii na wao ndio walinzi wa amani katika nchi yetu.

Kwa maana hiyo, naomba kusema hivi, kwamba Mhe. Spika wananchi wetu hawatuamini na kutotuamini kwetu ni kuondoa hizi taaswira za zogo za hapa na pale hazifai. Kwa kweli niwaombe sana ndugu wa Jumuia ya Uamsho watuachie kazi tutaimaliza ya kutetea Haki ya Mzanzibari kwa kupitia na hasa hapa ndipo pahala pale katika Wizara hii ya Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa sababu Ofisi hii ya Rais, yeye Mhe. Waziri ndiye mtendaji mkuu wa suala hili.

Kwa hiyo, tunamuomba sana hilo na watapokaa katika Vikao vyao vya Muungano, basi watuletee zile *minutes* za vikao, ili tuweze kujua tumefikia wapi.

Sasa naingia kwenye kuchangia ukurasa wa 14 kifungu cha 20 ah! Mimi Mhe. Spika, hufarajika sana kusikia wazee wetu nakusudia kwamba Mhe. Rais, Makamo wa Rais au Waziri anapokwenda nje hupata faraja sana, na kumbe wakenda kule wanakuwa wanaleta neema. Lakini jambo la kushangaza neema zile ukizisikia, kama leo nilivyoona hapa kwenye kifungu cha 20 kuhusu mambo ya afya, kumbe tulikuwa na Kitengo cha Saratani hapa na juzi nilisema kuhusu suala la vifaa vya saratani.

Mhe. Spika, siku moja nilimuuliza Mhe. Waziri je, katika Bango Kitita mnapokwenda kwa Mhe. Rais tukigundua Waziri ambaye anadanganya kwa Rais yuko tayari kujiuzulu? Mhe. Waziri alinijibu kwamba lazima atajiuzulu kabla ya kutangazwa na Rais. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niombe radhi sana sasa sijui kama wizara hii ndio itaanza kujiuzulu au wizara nyengine kwa kuonesha dhahiri kama kweli Mhe. Rais anadanganywa kwenye Bango Kitita na nitaendelea huko mbele, ili tuone jinsi gani Mhe. Rais wetu anavyodanganywa.

Lakini niseme Mhe. Spika, kwamba Kitengo cha Saratani hapa tayari kipo, na juzi nilisema kuwa mashine zipo, lakini tumepigwa changa la macho. Sasa sijui ni jumla ya mashine hizi tumeletewa msaada au mashine ambazo zimetolewa fedha za wavuja jasho kwa kwenda kununulia vifaa hivi.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika, vifuatiliwe vifaa hivyo basi aniletee jibu la kusema kwamba ndio vifaa vile na kama si vile basi tunaomba kuwa hivyo vitakavyokuja atueleze kwenye Baraza, na atuoneshe kama hivyo ambavyo alikwenda Mhe. Rais na sio kama ambavyo tunakwenda kule tukamdanganya, na mpaka leo hii vifaa hivyo bado havijafanya kazi vipo tu kwa sababu vimepungua.

Mhe. Spika, nasikitika sana Waheshimiwa wetu mnapokuja kutujibu majibu au mnapotaka kuchangia na nyinyi basi muweze kuchangia masuala ambayo yenye msingi na msifutuke tu mkatuona labda sisi tunafyetuka tu. Kwa kweli sisi tunafuatilia nyanzo hadi nyanzo, na hili tunakwambia kabisa Mhe. Spika tena utuamini Wawakilishi wako, kwamba tukipewa jambo lenye maslahi ya umma, Mhe. Spika tunafuatilia lakini zile mashine za Saratani zinatuuma sana, kwa sababu leo ukimtoa mtu *biosis* na ukiipeleka Dar-es-Salaam hali kama hiyo hivi sasa kuna mgomo hebu niambie hafi mgonjwa wako na halafu leo mtu anatuchezea hivi na kuja kutujibu majibu hivi hivi tu kuhusu hizi mashine.

Mhe. Spika, suala hili hatukubali na wala si pahala pake, lakini nimegusia kidogo na nitakusamehe kwa hili na nitakwenda huko kunakohusika ambako nitakwenda kugaragara hasa, kwa sababu fedha za wavuja jasho zinaniuma, kwamba serikali yetu au viongozi wetu wanakwenda nje kwa ajili ya kutafuta wafadhili na kutuletea na sisi tunazembea mpaka leo Mhe. Spika kitengo hichi hakijafanya kazi kipo tu.

Vile vile utaleta vipi mashine ambayo haina *catalogue* umepata kuona wapi, haiwi peni ukiletewa unapewa na *catalogue* yake jinsi ya kutumia na wino gani unaotumiwa mule kama ni *chemicals* au vipi, lakini mashine zile hazina *catalogue,* mshamdanganya Rais na sasa wataanza kujiuzulu wenyewe waliomdanganya Mhe. Rais kabla Baraza kuja kutamka rasmi hapa. *(Makofi)*

Kitabu hichi kinanishangaza jambo moja Mhe. Spika, kwamba sisi unatukataza tusirejee, lakini kitabu hichi kinajirejea. Kwa hivyo, nina wasi wasi wakati wa kupanga bajeti hizi kulikuwa na makundi mawili, yaani kati ya Katibu na kundi lake na Mhe. Waziri na kundi lake, hali hii inanishangaza sana katika kichwa changu, kwa sababu kuna mambo yanajirejea yale kwa yale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba sana wakati mwengine wazee wetu wakituletea kitabu wawe *straight forward,* moja kwa moja watupe zile *points* na isiwe yale mambo ya kujirejea.

Vile vile tumeambiwa hapa kuna mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya KMKM, hatujui mpaka hivi sasa ni kiasi gani cha gharama zilizotumika pale, na serikali inataka iongezwe tena fedha nyengine. Sasa suala hili namuomba Mhe. Waziri aniletee kwa maandishi kunielezea mradi ule tokea mwanzo mpaka kufikia pale umetumia kiasi kadhaa na hivi sasa unahitaji kuombewa kiasi kadhaa, je huko nyuma utaratibu wake ulitumika vizuri, tunataka kujua hilo.

Nikiendelea na mchango wangu haraka, ili niweze kutoa nafasi kwa wenzangu naomba niingie kwenye ukurasa wa 33 kuhusu mambo ya Vitambulisho. Mhe. Spika, mimi nilikuwa mkali sana kuhusu masuala ya vitambulisho na kwa kuona Wazanzibari wanakosa haki zao, basi mimi nikawa mkali Mhe. Spika, wanakosa haki zao lakini wanapewa watu wengine ambao sio wanaostahiki. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Spika, nikajiuliza na nikafahamu kuwa tuna tabia sisi tukisema hapa na masuala yanaishia kwenye meza tu na wala Mawaziri wetu hawafuatilii. Kwa kweli hii ndio hoja ambayo inatupasa hapa Mhe. Spika, kwa sababu unatupa fedha kwa ajili ya kutusomesha vizuri Mhe. Spika, lakini tunachokuja kukifanya hapa ni sawa na kuimba nyimbo tu ndicho tulichokigundua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza niwashukuru sana watendaji wa Idara hii ya Vitambulisho, kumbe na wao wanasikiliza nini wanachoambiwa na hawangoji kuambiwa na Waziri wao, isipokuwa wanafanya utekelezaji wao wenyewe na kuangalia lile lililozungumzwa.

Baada ya kugundua watu ambao walipewa vitambulisho kinyume na utaratibu na wala hawakustahiki. Mhe. Spika, nili-*review* mwenyewe na kuhangaika na kupata ukweli ulivyo. Kwa kweli idara hii iko wazi na wala haimfichi mtu na inakwenda na mambo ya *science and technology*. *(Makofi)*

Sasa nilipokwenda kule Mhe. Spika, niliambiwa kwamba Mhe. Makame Mshimba Mbarouk tayari watu wako tumeshawatoa ni hawa hapa na wengine wamekimbia wenyewe, wengine wamenyang'anywa na wengine wamefikishwa kunako chombo kinachohusika cha sheria. Mhe. Spika, nimewapongeza sana, kwa sababu mimi mwenyewe baada ya kusema na nimewafuatilia, hivyo niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilipokwenda kule nikayakuta mambo mengi ah! Mimi hupiga kelele kule Kitope watu wetu hawapati vitambulisho. Lakini nilichoambiwa Mhe. Spika, utaratibu upo, nikauliza utaratibu gani, kumbe kuna Fomu ya Rufaa na ukijaza fomu hiyo tayari mtu wako anakwenda, na kuna Tume Maalum ambayo wameiunda wenyewe ikiongozwa na kijana mdogo tu, ambaye ni Mwanasheria anakwenda kuangalia uhakiki wako, ili uweze kupewa na ukigundulikana umekwenda vizuri, basi unapewa kitambulisho *immediate*.
Kwa hivyo, nimeiona fomu hii na nikaona niichukue iwe *example* kwa wenzangu, kwamba hoja zetu tukipiga makelele twende na utaratibu, kwa sababu tukipiga kelele twende kisayansi, ndio maana Mwalimu wangu Mhe. Mwanasheria Mkuu ananiambia ukitumia jambo, basi tumia na sheria. Mhe. Spika, naomba kwa wenzangu kwamba sheria hii ipo na inafanya kazi.

Jambo jengine ambalo nimeligundua Mhe. Spika, kuna watu unajua siku hizi vijana kila mtu ana mbinu zake ah! Kwa kuwa Mshimba maarufu nchi hii basi atakwenda kutumia Mshimba, jina jengine kwa Wete na huko Wete Mshimba hawamjui tusidanganyane, lakini kumbe hajui Mshimba kama tayari nimeshapata kitambulisho na kule anakokwenda kusema, sasa tizama mashine zinavyosema na wamepata *model* ambazo ni za kisasa.

Mhe. Spika, ukitiwa tu mule umeiba jina la watu ngoma inakataa unasema huyu *no* huwezi kupewa kitambulisho, kwa sababu gani inatoa *records* zako. Kwa hivyo, tuwape sifa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lazima tukubaliane na mimi nitaifanya kazi hiyo kwa mara nyengine nita-*return back*, ili niweze kufanikisha suala hili. Kwa kweli kuna orodha kubwa tu ambayo wananchi wetu bado hawajenda kuchukua vitambulisho.

Kwa maana hiyo, hebu tufanye zoezi hili kwa makusudi kwa kupitia na wao wenyewe watuongoze. Kwa mfano, kwa upande wa Pemba Wilaya ya Wete kuna watu 9200, Wilaya ya Micheweni watu 6000, Wilaya ya Mkoani watu 7, na kwa upande wa Unguja Wilaya ya Mjini watu 28000, Wilaya ya Magharibi 22, Wilaya ya Kati nayo pia na hali kadhalika Kaskazini B ni watu 7000.

Mhe. Spika, mimi nitawaomba hawa watushirikishe na wala wasione tabu na sisi tuko *free* hatuna haja kwamba watupe malipo, lakini tuone hii haki inafika. Kwa hivyo, naomba wangefanya utaratibu na wao wakajaribu kuangalia je, katika ile Kaskazini B vimo vya Kitope, Donge au wapi, basi waje tuwatafutie wenyewe na mimi niko

tayari kubeba mzigo huu pamoja na wao kuwasaidia na haki hii isipotee, Mhe. Spika kwa nini vikae kwenye ofisi tu. Kwa kweli nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi sasa wanao mtindo mmoja ambao ni mzuri sana, wawekezaji wetu wanapata matatizo ya kunyang'anywa ardhi, kwa sababu hawana *security* ya kuwalinda.

Kwa hivyo, wao wametafuta kitambulisho cha kumtambua kama yule mwekezaji hapa Zanzibar yupo kwa mujibu wa sheria na anawekeza kwa mujibu wa sheria, na hii *well and good* na mimi nawapa sifa kubwa sana. Kwa kweli tunawataabisha wawekezaji hivi sasa, yaani wanafutiwa maeneo kwa kuonewa, lakini akiwa na kitambulisho huwezi kumfutia sheria imeshakubana na wewe, tayari yule ni jamii moja, isipokuwa tofauti ni haki tu, sasa kwa hili nawashukuru sana.

Mhe. Waziri pitisha haraka hii uwaletee *investors* Zanzibar tutawakosa kabisa kwa mchezo tunaoufanya huu uliokuwa hauna msingi.

Sasa mimi niwashukuru sana kwa hilo na mimi niko tayari kuonana nao bega kwa bega. Suala hilo Mhe. Waziri wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wanatumia kemikali na ukiangalia hata mafungu yao hayastahiki wanapewa ovyo ovyo, kwa kweli hawa vijana niseme kwamba nawashukuru na Waheshimiwa wenzangu nakuombeni sana fatilieni mlango wao uko wazi hawana tatizo lolote. Watakupeni darasa, watakusaidieni, aliyekuwa hakupewa atapewa fomu ya rufaa tutakwenda kufuatilia masuala hayo.

Mhe. Spika, niende na mimi katika masuala haya ya Mamlaka ya Serikali za Mikoa. Tumeambiwa Wakuu wa Mikoa wamepewa majukumu maeneo hayo ni pamoja na kutoa miongozo, kutafsiri sera, sheria pamoja na amani na utulivu.

Mhe. Spika, ikubaliani nalo hili si kweli. Kitabu kinasema sawa, utendaji hauendi unavyotakiwa. Mhe. Waziri tunapoandika kitu kwanza tukifanyie uchunguzi, tuna miaka mingapi sasa hivi tunazo mamlaka hizo na lipi lililofanyika nitajiwe moja tu kwanza lililoweza kuwajibika na kufanya muongozo wa aina hiyo.

Lakini niingie ukurasa wa 48, Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mhe. Spika, nishukuru sana kwa jitihada ambazo zilikuwa zinaongoza katika Mkoa huu hasa katika kilimo, lakini zaidi kulikuwa na suala ambalo lina utata katika serikali kuu kuwapatia vyanzo vya kuweza kufanya kazi zile kuwa ni kidogo sana na matrekta yanachelewa kuletwa na karibuni nilimuona Mhe. Waziri alikuwa mdau mmoja wa kufungua matrekta yale kule JKU kwa kupitia JKT lakini sijui *finishing* yake imeishia wapi. Tulimwambia ajitahidi kuyashusha kwenye majimbo ili angalau hata sisi Waheshimiwa tukopeshwe ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu waweze kulima kwa wakati. Sasa hilo ni moja ambalo niliomba tuweze kusaidiwa.

Niingie sasa ukurasa wa 57 Manispaa. Mhe. Spika, Manispaa kuna sehemu moja Mhe. Waziri Wawakilishi wengi wanapioga kelele suala la njia. Mhe. Waziri kifungu hiki nitakuwa sikipitishi na nitakuwa mkali sana kama yale mawe hayajaondoshwa na njia ile ikapitika.

Juzi nilikuwa shuhuda mimi mwenyewe na Mwenyezi Mungu haya mambo huyafanya kuwa nikiyasema hapa basi baadhi ya wakati huwa nayaona machoni, hutokezea na mimi mwenyewe kuwa shahidi tosha. Kwa sababu siku moja nilisema suala la makontena kuwa jamani nyee, yataleta athari kuondosha mchana watu wanakwenda huku na kule, sasa liliwahi kutokea pale *Cine afrique* pale Malindi, alimanusura gari ivurugwe na upakiaji wa makontena, nimeshuhudia mwenyewe limebeba 40*ft.* Sasa haya mambo mengine jamani tukisema msitudharau mjue tunaona.

Mhe. Spika, njia hii iondolewe bwana, juzi imeleta zogo msururu mkubwa sana, mimi nitakubaliana zipitishwe tani za gari hilo nakubaliana na wewe, kuwa magari makubwa yasipishwe *ok* nakubaliana hilo, lakini vyengine vyovyote tunaomba aondoe leo jioni vile vikuta watu wapite njiani.

Hivi karibuni nilimuuliza swali Mheshimiwa wangu akasema kwamba *account* hiyo iko *independent* haikuwa *account* ya Manispaa ya suala la makusanyo ya fedha za Forodhani. Hebu nataka nimwambie Mhe. Waziri aje atueleze ni kiasi gani mpaka sasa hivi zimekusanywa na pesa zile zimegawiwa mafungu mangapi kati ya Mji Mkongwe na wao, mgao wao ukoje, hilo naomba sana Mhe. Waziri aniletee.

Lakini la pili jamani kuwe na muda wa kukusanya pesa za *parking*, Forodhani Mheshimiwa mzima nime-*park* nakula *ice-cream* nakuja kudaiwa kodi usiku, hee, Waheshimiwa tuwe na muda wa kukusanya fedha na tuseme ikifika muda fulani jamani aa mimi hizi pesa nyengine nazikataa hazendi serikalini tusidanganyane, hizi zitakuwa za *part time* ya mtu. Ikwa sababu jamani mpaka usiku, mimi nimekwenda nchi nyingi tu sijaona kodi namna hiyo, ikifika wakati *finishing, finishing* tu huria tena mnakwenda zenu basi na sisi tuwe na muda wetu Mhe. Spika. Sasa hilo mimi sikufurahika nalo.

Mhe. Spika, niseme jengine kwa haraka suala la duka na *supermarket*. Supermarket ile pale ni duka la Manispaa wenyewe, usajili wao wenyewe, lakini fununu za hapa na pale Mhe. Spika, wenyewe watu wa Manispaa walimpa mwekezaji kwa muda wa mwezi mmoja bure ili akimaliza arejeshe Manispaa wamepata mfadhili wa kujenga *model* ya kisasa, ofisi za kisasa kama ofisi za watu wengine. Cha kushangaza Mhe. Spika, kitu hicho hakikufanyika muda ukaisha yule bwana akaona apande ngazi za juu atafanikiwa, Mhe. Spika, tuwaheshimu madiwani wana kanuni zao na sheria, kwa hili Mhe. Waziri sikubaliani nalo mwekezaji amuondoshe mara moja alirejeshe kwa wenyewe Manispaa wafanye kile kitu wanachokitaka.

Kifungu hiki mimi nitapambana nacho sikubali wala siiungi mkono hoja hii kama jambo hili sikupewa taarifa maalum. Haiwezekani wao wametoa notisi ya muda wa mwezi mmoja wawe *free* halafu mwekezaji anapita kwa nyuma ya mgongo anakwenda kwa waziri na waziri anasema *stop*, hiyo haiwezekani bwana, ni lazima Mhe. Spika, madiwani wetu wapewe heshima, posho lenyewe wanawapa dogo halafu wawazuilie miradi yao.

Mhe. Spika, kwa kumalizia mwisho niseme kwamba hili suala namuomba sana Mhe. Waziri, halafu Mhe. Waziri katika buku kubwa pesa za likizo shilingi 85 milioni lakini askari wa chini hawapewi likizo na wakipewa likizo hawapewi pesa wakati fungu limo humu kwa nini, hebu tuelezeni. Askari hawapewi pesa za likizo lakini kwenye buku kubwa zimo shilingi 85 milioni mnatoa kwa matabaka ina maana wenye vyeo ndio watapewa pesa za likizo wa chini wanyanyaswe kwa nini na hawa wapewe.

Halafu pesa za michezo kuna Idara moja tu KMKM ndio wanalipwa shilingi 35 milioni, JKU wana michezo ya kila aina hawana pesa humu sijaziona, KVZ, Zimamoto senti tano sijaona kwa nini wao wasipewe na wao ndio idara hiyo hiyo. Ningeomba sana Mhe. Waziri na wao waweze kukamilishiwa wapewe fedha zao nao inavyotakiwa.

Nimalizie sasa Mhe. Spika, samahani sana kwa kuchukua wakati wako kwa sababu ya mambo matamu, kila ninapokwenda mimi ndio najisikia utamu. Kwa sababu kuwatetea wanyonge ni haki yetu. Mhe. Spika, mshahara sasa hivi wa maaskari wetu wa kwenye vikosi haustahiki umeshapitwa na wakati wanapokea mshahara mdogo sana, tunaomba sana hiki si kitu cha masihara. Hii yote inakuja kwa sababu gani, pesa zetu za Muungano hamtaki kuziomba, hamtaki kuzifuatilia na ndio maana inatufika kazi hii.

Mhe. Spika, leo askari wetu anapewa pesa za chini ni aibu, anashindwa na Polisi kwa sababu ya Muungnao na wakati na yeye huyu yumo ndani ya Muungano. Waheshimiwa tusilale, tuwachukulie wananchi pesa zao kule kunako Muungano tuwaletee ni haki yetu Wazanzibari na ni wajibu wetu kusema ukweli ile ni haki yetu imo ndani ya katiba hatusemi hivi hivi tu. Mhe. Waziri wewe shahidi umetusomesha na jana tulikuwa naye mbunge ametoa vitu kutoka Bara hii ni haki yetu.

Hiki kikao cha mwisho mnapokwenda huko mhakikishe mnatuchukua na sisi ubavuni tutawaambia pale pale *message* itakuwa imeshafika; tunarudi na nyinyi mnarudi na pesa zetu. Hiyo Mhe. Spika, *message* imefika.

Kwa kumalizia kuna mambo kumi ya Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kaeleza. Katika mambo kumi hayo ni amani na utulivu, mshikamano huo ndio tunapiga kelele na tushawaomba wenzetu ndugu zetu wa Muamsho. Sasa wamenyamaza kimya na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awajalie wasifanye fujo watuachie tumalize ili nchi yetu isiendelee na fujo maana utalii utaanguka kwa sababu watalii wanaogopa mambo kama hayo.

Lakini Mhe. Spika, nasema tuwajibike tusifanye kazi zetu kwa maslahi yetu wenyewe, amesema mwenyewe Mhe. Rais. Katika wizara zako sasa Mawaziri tukiwaambia wawajibike wafuate kitabu hiki watawajibika tu, wameshindwa kutuletea pesa za Muungano, wameshindwa kufuatilia pesa za maendeleo ya bajeti watawajibika.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, niseme kuwa naunga mkono hotuba ya Mwenyekti na ninakaa kitako namngoja Mhe. Waziri anieleze yale niliyomwambia na bajeti yake shilingi yangu siitii hapa nimeiweka kwenye mfuko. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Awali ya yote Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) aliyeniwezesha kusimama hapa na kuniazima pumzi zake hizi ninazo hapa kwa muda huu. Kwa neema hiyo basi namshukuru Mwenyezi Mungu.

Vile vile nitakuwa si mwingi wa fadhila Mhe. Spika, kama sikukushukuru wewe uliyeniruhusu kusimama mbele yako kuzungumza mawili matatu. Vile vile nikupongeze kutokana na hekima zako, busara, maarifa jinsi unavyoendesha kikao hiki kwa umakini na umahiri mkubwa. Kuna baadhi ya Waheshimiwa wengine nimewasikia juzi Uroa wanasema kwamba, pindipo kama hutaendelea na nafasi hiyo hawatagombania tena majimbo.

Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri kwa jinsi alivyohakikisha hotuba yake hii na vile vile nimpe pole kutokana na wizara yake ilivyokuwa kubwa na muda wake mwingi. Kwa kuanza sasa nianze na kitabu hiki ambacho kinavutia kutokana na rangi yake kijani ni kijani yenyewe hasa.

Kwanza nataka nipongeze katika ukurasa wa nane (8) kwa mambo kumi yaliyoweza kufanyika. Nikitoka hapo nije katika ukurasa wa 13 bila ya kupoteza muda. Kumbukumbu ya mazungumzo yanaendelea lakini utendaji wake kwenye migogoro ya ardhi bado haujapatikana ufumbuzi hadi hii leo. Hilo limekuwa tatizo ambalo limeota mizizi.

Nikitoka hapo nije katika ukurasa wa 14, katika safari wanazokwenda viongozi tumeambiwa Wizara ya Afya kuna lengo la ku-*share* matibabu ya maradhi ya Kisukari, Figo, Moyo na Saratani kutoka Sharja, lakini bado utendaji wake mpaka sasa hivi hatujaona matunda yake.

Mhe. Spika, sasa nije katika Soko kuu la Darajani soko ambalo liko katika hali isiyoridhisha hata kidogo, kutoka mbele ya mazingira yake hadi ndani. Soko limekuwa linatishia usalama wa afya za wananchi. Mhe. Waziri ningemuomba sana, kwa heshima na taadhima akazuia haraka kwenye sehemu ya kuchinjia kuku mazingira yake hayafai. Kuna msemo unaosema, "Ukitaka kula kuku usiangalie anachokula", lakini kwa kweli kuna tope, kuku wanatupwa ovyo na lile soko linachangia pesa si kidogo Mhe. Waziri na sifikirii kama kuna gharama kubwa ya kujenga soko lile, mazingira yake hayaridhishi hata kidogo hivyo nimuombe kwa mara ya pili akalizuia soko lile kwa haraka na kufanyiwa matengenezo.

Tukiendelea kwenye soko hilo hilo kuna vibaraza ambavyo hata havina gharama kubwa na wale wanachangia shilingi mia tano kwa kila siku, kwenye vipenu nje pale kwenye eneo la barabara ya Zakaria, bati zake zote zimeshaanza kuanguka chini na sijui lina gharama ya kiasi gani kutengeneza lile na wananchi wanachangia pesa pale.

Sasa tuje katika Soko la Samaki ndani, hali vile vile hairidhishi kabisa wanalipa pesa wale lakini kutengenezewa kwao hakuonekani mpaka leo, nafikiri tangu alipofanya marekebisho Marehemu Dr. Hassan Haji Wambi mpaka leo soko lile halijafanyiwa marekebisho. Tumepiga kelele kuhusu kubeba nyama na bado zinaendelea vile vile kubebwa, afya za watu zinazidi kudidimia na wale wote bado wanachangia, sasa sijui pesa za pale zinatumika kwa matumizi gani. Soko toka lilipotengenezwa nafikiri halijafanyiwa marekebisho ya aina yoyote ile.

Mhe. Spika, tuje mbele kule kwenye sura yenyewe hasa ya soko, hali ya baraza zile haziridhishi, walioweka mameza pale kupanga watu na wale wanachangia vile vile wangejengewa angalau barabara za moja kwa moja halafu chini wakatiliwa vistoo. Lakini ukipita wakati wa jioni pale magunia yaliyofunikwa pale utafikiri choo cha shamba.

Samaki vile vile wanaendelea kuchanjwa barabarani, tulilipigia kelele muda mrefu kwa Mhe. Waziri, tukija soko lenyewe pale mbele *stand* ambapo ndio kituo kikubwa cha magari wanachotumia wananchi. Tumepiga kelele pale kuna wachimba dawa bado hali inaendelea vile vile kuchimba dawa, taa tumepiga kelele zitiwe pale bado hazijatiwa hadi leo na sifikirii kama pana gharama kubwa hasa kutokana na utendaji wa Mkurugenzi wetu alivyo ni mchapa kazi keshafanya mambo mazuri tu.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika Barabara ya Mkunazini. Kwa taarifa nilizonazo Mbunge wa jimbo lile tayari kesakabidhi kitengo chako shilingi 40 milioni, barabara ile hairidhishi na sisi wengi hali tumeiona ilivyo watalii wetu jinsi wanavyopata tabu, wenzetu wakienda kufanya ibada katika makanisa, watalii wakienda katika Soko la Watumwa na kipande chenyewe wala si kikubwa hata hivyo. Hiki nitahitaji maelezo Mhe. Waziri.

Jengine Mhe. Waziri nitazuia kifungu kutokana na Barabara ya Malindi *roundabout* na mwenzangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kalizungumza suala hili. Hiki kimekuwa ni kilio cha muda mrefu na kwa kweli umekiri kuwa barabara hii utaifungua haina sababu yoyote, kwenye kikao cha kwanza na cha pili lakini bado hali inaendelea tete. Mara ya mwisho lilikuja jawabu kuhusu tatizo la Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, kama Mji Mkongwe Mhe. Waziri hao ndio wanaoleta matatizo kwa nini barabara ile ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuelekea ndani kupitia njia ya Jamatini mpaka kwa Muzammil njia ile iko kati kati ya Mji Mkongwe, kwa nini inatumika ikawe kisingizio barabara ile tu. Umekiri Mhe. Waziri mimi naomba uoneshe uungwana wako na mimi ndio maana nikachangia mapema hapa ili nisije nikazuia kifungu ukaja ukasema baadae utafungua, bora ukafungue

Hilo nikuombe kabisa Mhe. Waziri, ndio maana nikachangia mapema nafikiri hili halina mjadala jioni nategemea ile njia itakuwa wazi, hata hivi sasa nilipopita naona kuna fununu fununu ya kuondoshwa yale madude pale. Kwa hivyo, nikupongeze sana Mhe. Waziri, litabaki suala la mabati ya *no entry* tu kuondoka pale.

Mhe. Spika: Mheshimiwa jitahidi kuielekea hiyo *mike* hapo ili Mhe. Waziri na Waheshimiwa wengine wakusikie vyema, ielekee vizuri ili na waziri asikie vizuri achukue dondoo kwa kuja kutoa majibu muwafaka.

Mhe Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana. Sasa nije kuhusu suala la Zimamoto. Zanzibar ina majumba mengi sasa ya ghorofa na kipindi kifupi tu hata mwezi mmoja au miwili haijafika eneo la Mji Mkongwe limekuwa likiathirika sana kwa kuungua kwa nyumba na hivi sasa magari ya *fire* kwa maeneo yale hayapiti, sijui wizara yako imechukua mikakati gani. Hivi juzi tumezima moto Darajani pale gari haikuweza kupita, juzi juzi tena Joskona kulitokea mtihani kama huo na gari hazikupita, sijui wizara yako imejipanga vipi.

Halafu jengine zaidi askari wa Zimamoto wa Uwanja wa Ndege Pemba wanalala katika mazingira ambayo hayastahiki kuishi binadamu, vitanda na magodoro yao hayaridhishi Mhe. Waziri, pamoja na kwamba asilimia 99 kimepatiwa kikosi hiki lakini naomba hapo Mhe. Waziri patahitajika marekebisho.
Chuo cha Mafunzo. Chuo hiki kimefanya kazi kubwa sana katika nchi hii kinastahiki kupongezwa kwa dhati kabisa, lakini bajeti yao bado hairidhishi na kuna hatari ya kurudia tena vile vile wanafunzi wale kula mlo mmoja badala ya milo mitatu. Bajeti yao haikidhi na cha kusikitisha zaidi ni kwamba wanaambiwa wachangie karibu shilingi 30.27 milioni kupeleka *ZRB* sijui hiki kitu ni kweli Mhe. Waziri.

Kuhusu Soko la Mwanakwerekwe nirudie tena nimesahau, wakati wa masika hakupitiki kule tope zinanuka sana na kipande si kikubwa kinahitaji kurekebishwa Mhe. Waziri.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi katika asubuhi hii ya leo kuchangia machache katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja katika Ofisi ya Vitambulisho. Vitambulisho ndani ya nchi yetu na nchi nyengine zozote zile duniani vina maana yake maalum, sasa vitambulisho ndani ya Zanzibar yetu ni nusu na robo ya maisha ya mwanadamu. Baadhi ya watu walifikiria kuwa vitambulisho ni kwa sababu ya kufanyia uchaguzi tu au kupigia kura, lakini sio hivyo, maisha yote ya mwanadamu yanataka uwe na kitambulisho cha mkaazi. Sasa nashukuru nchi yetu au serikali kwa jumla kutoa maamuzi ya kutengeneza vitambulisho, lakini vitambulisho hivi imekuwa ni kinyume na vilivyofikiriwa.

Kwa sababu katika vitambulisho kuna watu wa makundi matatu au manne au zaidi ya hapo, kuna watu ambao wamekamilisha masharti yote kuanzia miaka 18 na kuendelea wana vyeti vya kuzaliwa na kila kitu, wale tayari hawana tatizo la kupata vitambulisho; kuna watu kuanzia miaka 45 na kuendelea mpaka miaka mia au na zaidi ambao hawana vyeti vya kuzaliwa lakini ukiwaangalia tu au kwa vithibitisho vyengine kama vya kumalizia skuli,

pengine mtu keshazeeka hata meno hana tena na yule pia anaambiwa kama hana cheti cha kuzaliwa hapewi kitambulisho. Ingawaje ofisi ilitoa taarifa hapa kwamba watu kama wale wenye umri kama huo waende Mahkamani wakachukue *affidavit* baadae watapewa vitambulisho.

Lakini Mhe. Spika, nataka nikwambie, bado Vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi ni vikwazo katika maeneo mengine na wanaokwamisha hatua hii ni wenzetu Masheha. Baadhi ya Masheha bado hawajawa tayari kutoa haki hii kwa kila Mzanzibari ambapo kila Mzanzibari ana haki ya kupewa kitambulisho hiki. Kwa hivyo, ninaiomba sana wizara yako Mhe. Waziri utumie hekima zako zote lakini uzungumze nao ndugu zetu Masheha watu wakienda wasiwakwamishe mtu anaweza kwenda zaidi ya mara ishirini akifika anaambiwa leo fomu hamna, kesho fomu hamna njoo keshokutwa watu wanachoka Mhe. Spika na hii ni haki yao. Kwa hivyo, nakuomba sana katika hili na pia naomba nitoe ushauri katika hili.

Kwa kuondoa usumbufu wa watu wengi, watoto pengine kwa nini hii hali hairudishwi mle maskuli kwa wale wanafunzi waliokwishamaliza skuli kama vile *Form IV*, *Form III*, mtu anajulikana kama huyu tayari wakafanyiwa marekebisho pale pale skuli kupunguza huu msongamano wa kwenda kule kwenye ofisi za vitambulisho. Naomba sana Mhe. Waziri ulichukulie hili hatua muhimu kwa sababu ni haki ya kila Mzanzibari kupata kitambulisho ambaye keshatimiza masharti.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niende kwenye Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake kazungumza mengi katika hili kuhusu mambo ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa na kawapongeza sana na kuwasifu wenzetu hawa wa Mabaraza ya Miji na Serikali za Mitaa kuhusu ukusanyaji. Katika mtazamo wa kitabu chake wamevuka lengo kwa sababu mtu pengine kakusudia kukusanya shilingi 40 milioni kakusanya zaidi ya shilingi 40 milioni. Lakini katika hilo Mhe. Waziri mcheza pao hutunzwa, nafikiri ahata katika kikao kilichopita miongoni mwa makusanyo hayo wanayokusanya vyanzo hivi vya mapato wengi ni wenzetu, ndugu zetu Madiwani na hawa wanafanya kazi kubwa ya kuisaidia serikali katika kukusanya na kufanikisha mambo tofauti kama vile kutoa madawa ya kichocho, kutoa dawa za vyandarua, kila kitu Madiwani ndio wanaoshiriki kwa njia moja au nyengine katika kukusanya vyanzo vyao vya mapato.

Lakini cha kusikitisha Mhe. Waziri mpaka sasa bado Madiwani wetu hawajafikiriwa, jamani Madiwani na wao ni wenzetu, tumefanya chaguzi tano ya Rais wa Zanzibar, Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mbunge, Mwakilishi na Madiwani na serikali imetumia pesa nyingi sana kwa chaguzi tano hizi kwa nini ndugu zetu hawa hatuwafikirii na wao. Hebu janami waoneeni huruma na wao ndugu zetu Madiwani wafaidi matunda ya serikali yao, nakuomba sana Mhe, Waziri uwatizame ndugu zetu Madiwani.

Halafu katika hotuba yake pia amezungumzia kuhusu hawa hawa Madiwani sasa hivi tayari wana mashirikiano mazuri na wanajua mipaka yao, wanajua matumizi yao, wanajua kila kitu; na waziri amesema kuwa ameshawafanyia semina nyingi madiwani pamoja na masheha. Nakuomba Mhe. Waziri utakaposimama hapa utwambie ni semina ngapi walizofanyiwa Madiwani hawa wa Unguja na Pemba ili tujue na wao kama kweli hili jambo wamefanyiwa au laa. Kwa sababu pengine kwenye kitabu mna semina za madiwani lakini wenyewe wana malalamiko kwamba hawajawahi kufanyiwa hata semina moja angalau kuelekezwa na wao au kutoa mawazo kuonekana tu kwamba na wao wanajulikana ndani ya nchi hii.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naombe niendelee kidogo katika suala la miradi. Kwenye miradi nitakuja moja kwa moja kwenye miradi ya shamba la mbogamboga lililoko Bambi. Mhe. Spika, kuna shamba la mbogamboga lililoko Bambi JKU limetumia pesa nyingi na huko nyuma tuliambiwa lile shamba ni shamba la majaribio. Sasa hivi pia katika maombi nimeona tena miradi hii inaomba tena pesa kama shilingi 300 kama sijakosea, naomba Mhe. Waziri kabla ya kuidhinisha pesa hizi katika kuliendeleza shamba hili la JKU la mbogamboga basi tuelezwe kwa kina nyuma pesa nyingi zilizotoka kwa kuunda mradi ule je, tumepata faida gani na hasara gani kabla ya kuidhinishiwa pesa nyengine.

Mhe. Spika, naomba niendelee tena hapa hapa kwenye mambo ya Manispaa na Mabaraza ya Miji. Mhe. Spika, mji wetu bado hali haijawa nzuri, mji unanuka aibu kupita kwenye mitaa hasa pale Mjini Darajani ukipita utafikiri kuna mzoga umekufa, watu wapo wameajiriwa wengi, wanafanya kazi, kila siku bajeti zinapitishwa za usafishaji lakini cha kusikitisha bado hali haijawa nzuri Mhe. Spika. Nakuomba Mhe. Waziri hili ulifuatilie sana katika mji wetu bado uchafu ni mwingi mno.

Wenzangu waliotangulia kuchangia walisema hapa kama pale kwenye Soko la Samaki Darajani ukipita unaona uchafu hata kununua kitu ukala, ni kweli Mhe. Waziri na bila shaka na wewe mwenyewe katika maeneo yako ukitembelea unaiona ile hali. Kwa hivyo, ninakuomba ile hali idhibitiwe san asana.

Halafu katika kukusanya mapato huko kwenye Mabaraza ya Miji mimi nataka nitoe masikitiko yangu makubwa, Baraza langu la Mji wa Wete linakusanya mapato mengi mno lakini katika ile Ofisi ya Baraza la Mji wa Wete kuingia huna hata pa kukaa, ofisi ndogo, mbovu haifai, chafu na sijawahi kuona pahala angalau pa kufikiriwa kwamba ile ofisi nayo itafanyiwa marekebisho japo madogo madogo. Mhe. Waziri nakuomba sana Wilaya ya Wete ni wilaya inayofanya kazi za serikali, inasimamia kila kitu na kila kitu kinathibitika pale na kukamilika lakini naiona umeiweka nyuma katika ile ofisi yetu ya Baraza la Mji angalau ionee huruma Mhe. Waziri, nakuomba sana.

Halafu Mhe. Spika, naomba niendelee hapo hapo kwenye vianzio vya mapato kwa sababau kwenye vianzio vya mapato bado ni vidogo. Vianzio vya mapato waliopewa wale Mabaraza ya Miji ni vidogo mno. Wakusanyaji wamekuwa wengi, sasa wao haki wanayoipata ni kidogo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ninamuomba awaongezee vyanzo vyao vya mapato na wao, halafu wewe mwenyewe utaiona faida au maslahi ya kuongezewa. Kuna vitu vingi. Wao pengine wanakusanya zile shilingi mia mbili mbili za maandazi tu kutoka pale mjini au vijijini, lakini mambo mengine kama ya viwanda vidogo vidogo vya kuchongea na mengi. Nakuomba Mhe. Waziri hebu nifikirie hili uwaekee hasa mipaka yao ya makusanyo na utaona watakavyokusanya zaidi. Lakini katika hali hii ya kukusanya pesa za maandazi tu, pengine mtu anakaa tokea asubuhi mpaka jioni maandazi yenyewe hayajatoka, leo unamwambia lete shilingi mia mbili, ni tatizo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niingie kidogo katika suala la vikosi. Kwenye vikosi Mhe. Spika, naomba niende kwenye mafunzo. Wale ndugu zetu wanaopelekwa kwenye mafunzo kama lilivyo jina lake ni Chuo cha Mafunzo si chuo cha adhabu. Pale wenzetu wanatakiwa wawe katika hali nzuri, wale vizuri na kuishi vizuri ndipo akili itakapotulia na wao wakatubu yale waliyoyafanya huko nyuma mpaka kufikishwa pale.

Lakini la kusikitisha Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo bado hakijawa ni Chuo cha Mafunzo, kimekuwa chuo cha kuwatesa wale waliopo. Kwa sababu uchafu mwingi, huduma ndogo, eneo dogo. Vile wakikaa tu basi wanaambukizana maradhi kutokana na ile hali ilivyo.

Nimeshawahi kwenda kukagua pale Mhe. Spika. Halafu la kusikitisha pale bado unaweza ukenda pale ukakuta watu wameekwa ndani kwa ajili ya mambo mabaya mabaya, tuseme kama dawa za kulevya, bangi na vitu vyengne. Sasa pale utaona wamekaa mule labda kwa namna ya kujifunza na kutulizana na ile hali wasiipate. Lakini cha kusikitisha Mhe. Spika, mule mule ndani walimo unga na bangi wanapata na kila balaa munafanywa mule mule ndani.

Sasa sijui hawa wenzetu walinzi waliopo pale wanafanya kazi gani au vinapitishwa saa ngapi vitu hivyo vibaya katika magereza yetu. Nakuomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwa sababu pale ni pahala pa kujifunza, wale ndugu waliopo pale wakitoka wajutie waliyoyafanya na waendelee kuwa na hali nzuri ili kulijenga taifa letu.

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda nikushukuru na kumshukuru Mhe. Waziri lakini katika kulifikiria hili la Madiwani, ninalitilia mkazo, awatilie sana Madiwani wetu Mhe. Spika, ndio wanaoleta matumaini ndani ya nchi hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ninakushukuru na mimi kunipatia fursa ya kuzungumza machache kuhusu hoja iliopo mbele yetu. Huku nikitilia maanani mafunzo tuliyoyapata jana kule shamba.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika ukurasa wa 33 unaohusu Idara ya Vitambulisho. Mhe. Spika, katika ibara ya 60 mpaka 64 Mhe. Waziri amezungumzia sana juu ya Idara hii ya Vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, kwa kweli hii ID kwa hivi sasa Wazanzibari ni issue. Ni kitu muhimu sana hivi hiki kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Bila ya Uzanzibari Ukaazi katika nchi hii basi mambo mengi utayakosa. Kwa mnasaba huo ninaweza kusema kwamba Uzanzibari Ukaazi ndio haki ya kila kitu, ndio haki ya msingi hasa ya Mzanzibar, kwa sababu bila ya hii huwezi kupata ajira, leseni ya kufanya biashara, mwanafunzi hawezi kupata mkopo wa elimu ya juu, ninadhani kuna siku hata kusafiri hutopata kusafiri kwa sababu pasipoti huwezi kupata ya nchi hii bila ya kuwa Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, na kutokana na hayo nilitegemea kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ingefanya juhudi zote kuhakikisha kwamba kila mwenye haki ya kupata hiki kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi anapata. Lakini jambo la kusikitisha Mhe. Spika, kama pana pahala penye ubaguzi katika kupata Uzanzibari Ukaazi basi ni kwenye Idara hii ya Vitambulisho.

Mhe. Spika, hawa jamaa ni wabaguzi sana. Mimi sifahamu kwamba hili tendo la kuwanyima Uzanzibari Ukaazi ni katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi au vipi, kwa sababu hivi vitabu vyote, hiki cha mwaka jana kina rangi ya manjano na hiki cha mara hii kina rangi kijani, sasa sijui kwamba kitendo cha kuwanyima Wazanzibari Ukaazi ni katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, sidhani kwa sababu mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ni mtu ambaye ninayemjua kwamba aliyekuwa si mbaguzi, anayependa umoja, haki na hata Makamo wake Mwenyekiti ni mtu wa haki sana kwa upande wa Zanzibar. Sidhani kama ni ilani ya Chama cha Mapinduzi Mhe Spika, mimi ninadhani ni ubinafsi uliobobea.

Mhe. Spika, Mkurugenzi wa Vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi ameanza kuwabagua Wazanzibari tangu mwaka 2009 hili tatizo lipo. Huyu kijana hafai, huyu ni mbaguzi, ana kichwa kilichoelimika sawa sawa na taaluma ya hali ya juu lakini moyo uliosahauliwa Mhe.Spika.

Kwa mujibu wa nadharia ni kwamba elimu kubwa kichwani haina faida ikiwa moyoni haina chembe ya wema. Ubaguzi ni jambo baya sana Mhe. Spika. Ukizoea kubagua katika misingi ya kijigrofia, Mtumbatu na Mpemba, Mmakunduchi na Mbumbwini, ukianza kubagua huishi hapo, sawa sawa na kula nyama ya mtu huwezi kuacha Mhe. Spika.

Mimi ninadhani Mhe. Spika, sasa tuseme kwamba tumetoka katika tatizo la kisiasa katika nchi hii, sasa Mkurugenzi wa Vitambulisho vya Mzanzibari pamoja na Waziri wanatuingiza katika tatizo la kijamii tutaliita, tumeondoka kwenye tatizo la kisiasa, sasa tunaingia katika tatizo la kijamii. Hatuwezi tena kubaguliwa, tumepigania uhuru, tumeingia katika serikali ya Umoja wa Kitaifa, sasa tutahakikisha kila anayetubagua anawajibika yeye.

Mimi ninadhani Mhe.Spika, katika hili Mhe. Waziri anawajibu wa kuwajibika. Mimi nilimwambia huyu Mkurugenzi wa Vitambulisho mwaka 2009 nikiwa ni Katibu wa CUF wa Wilaya ya Chake-Chake. Nilimwambia Mhe. Mkurugenzi kuna tatizo zaidi ya watu elfu tano hawana vitambulisho. Akaniambia hapana, nimletee ushahidi. Nimletee watu physically.

Mhe. Spika, nikiwa Katibu wa chama pale wa Wilaya ya Chake-Chake CUF, akanipa mpaka siku Mkurugenzi huyu nimpelekee watu. Watu elfu tano si kidogo. Nikafanya bidii hiyo Mhe. Spika, watu wakala hasara kumfuata katika afisi ya Wilaya ya Chake-Chake mwaka 2009 ilikuwa.

Mhe. Spika, nikammiminia umati pale. Basi aliondoka akasafiri akaja zake Unguja. Matokeo yake umma ukavamiwa na vikosi vya ulinzi pale. Laiti ingelikuwa si umakini wa Jeshi la Wananchi walikuja pale, ninashukuru kwamba Jeshi la Wananchi maelekezo waliyopewa wafanye hawakufanya, tukatoka salama pale. Lakini ilikuwa watu wauwawe siku ile.

Sasa huyu kijana ni hatari Mhe. Spika. Sasa ninadhani Mhe. Spika, huyu kijana awajibike kwa sababu katika hili kwa sababu tushasema sana katika hili, kazi ni kutusikiliza na kutubabisha tu, tutakwenda tutafanya hivi. Mhe. Spika, ninachokuhakikishia kwamba haya maneno tunayopewa sitaki kusema ni ya uwongo kwa sababu ninaogopa kukiuka Kanuni lakini Mhe. Spika, ni kinyume cha kweli. Haya maneno anayotupa ni kinyume cha kweli, kwamba kuna vitambulisho katika Wilaya wenyewe hawendi kuvichukua. Ni kinyume cha kweli Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi ninataka huyo Waziri tufuatane twende katika Wilaya ya Chake-Chake akanioneshe hivyo vitambulisho, halafu mimi nitavigharamia kuvipeleka mimi. Inasikitisha sana Mhe. Spika.

Mimi ninadhani tushasema maneno mengi sana lakini maneno hayakidhi haja. Sasa kuna haja ya matendo. Mimi Mhe.Spika, katika hili ikiwa mtu kudai haki yake ni kuchafua amani au kuipiga vita serikali ya Umoja wa Kitaifa basi katika hili mimi ninakwenda ku-*mobilize* umma katika Wilaya yangu kuhakikisha kwamba sasa tunakwenda kwa Mhe. Rais kudai hivi ID. Tumechoka sasa, hawa wanatudanganya.

Mhe. Spika, ID kwa mujibu wa Mhe. Makame Mshimba katika *Hansard* zake na ziangaliwe, wanapewa wamakonde, Wakenya. Ni aibu na uhaini.

Ina maana kuna siku katika nchi hii ndani ya Baraza hili ataingia Mkenya. Kwa sababu huwezi kuchagua wala kuchaguliwa ikiwa huna ID ya Mzanzibari. Kuna siku ataingia Mkenya ndani ya Baraza la Kutunga Sheria, kuna siku katika Manispaa yetu tutaongozwa na Waganda. Wanaisaliti nchi hawa.

Mhe. Spika, mimi naomba katika hili kuwa hili litatufikisha pabaya, hili litachafua amani ya nchi. Naomba iundwe kamati maalum iende ikachunguze tatizo hili na kulitatua. Iundwe kamati maalum ya Baraza lako iende ikachunguze, kinyume na hivyo, basi pale tulipokwishaondoka tutarudi tena. Katika lile zogo la kisiasa ambalo sasa tumeshachoka nalo, wengine limeshatuweka jela miaka mingi, basi munataka kuturejesha tena pale pale.

Katika hili Mhe. Spika, Waziri atueleze ni lini tutakwenda katika Mikoa yote ya Zanzibar kuhakikisha kwamba hivyo vitambulisho vilivyokuwa havichukuliwi tunavisambaza kwa wenyewe. Na aliyekuwa na haki ya kupewa ni lini atapewa haki hiyo. Asitupige maneno tu humu. Kama hii kazi haiwezi bwana awajibike. Hilo ni moja. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Spika, niende kwenye Baraza la Mji wa Chake-Chake. Baraza la Mji wa Chake-Chake Mhe.Spika, huu mji wa Chake-Chake upo kati kati ya Pemba. Ni mji ni *link* baina ya Kaskazini na Kusini Pemba.

Kwa mnasaba huo Mhe. Spika, hapa ni *stopping over* ya biashara pamoja na shughuli za utalii. Kutokana na hayo ni mguso katika kisiwa cha Pemba. Nilidhani kuwa serikali inalijua hili.

Mhe. Spika, mwaka 2011/12 Baraza hili limekusanya makusanyo ya ziada. Wamesema ni asilimia 105 makusanyo waliokusanya pale. Lakini la kusikitisha Mhe. Spika, kodi za wananchi hazirudi kwao. Uzuri wa hizi kodi zikishakusanywa, lile jambo la wananchi wanufaike na jasho lao.

Kama kuna mji unaonuka Mhe. Spika, kama kuna mji ambao barabara zake hazipitiki basi ni barabara za mji wa Chake-Chake. Mhe. Spika, kila mfanyabiashara wa mji wa Chake-Chake kila siku anapofungua duka tu pale atoe shilingi mia mbili ya usafi. Yaani shilingi sabini na nane kwa kila mfanyabiashara kwa mwaka kwa shughuli za usafi tu hizo.

Lakini Mhe. Spika, inasikitisha sana kuona katika mji mchafu kwenye nchi zilizopo katika jangwa la Sahara basi ni ule mji wa Chake-Chake. Maana ukenda Mhe. Spika, kuna maeneo wameeka vikuta wale Baraza la Mji, zinarundikwa taka kwa marajio kwamba kesho zitazolewa au keshokutwa, ukipita baada ya wiki pale hapapitiki, ni mafunza na harufu mbaya. Sasa kwa nini wanakusanya kodi na mji unakuwa mchafu kiasi kile.

Mhe. Spika, kila gari inayofika Chake-Chake kwa kila siku inafanyiwa *parking* ya shilingi mia tano na ninasema ni zaidi ya gari elfu mbili kwa siku kwa sababu ni kati. Wanaotoka Konde wanakula pale, wanaotoka Mkoani wanakuja pale, kwa hivyo gari za pale ni zaidi ya elfu tatu kwa siku Mhe. Spika, na kila gari inatoa shilingi mia tano kwa siku kwa parking. Utawaona na vidubwesho vyao wanaandika Mhe. Spika, ni wizi mtu. Nenda ukaangalie ile *street* inayotoka *Barclays* kuingia sokoni pale, barabara inayotoka hospitali kwenda soko la samaki haipitiki. Sasa pesa hizi wanazitumia vipi.

Mhe. Spika, mimi ninadhani katika hili lazima akaze buti, aone hasa ni kwa namna gani hizi kodi za wananchi zinarudi kwao. Sio hawa watu wanatuchukulia pesa zetu wakizitia kwenye matumbo yao tu.

Mhe. Spika, ninakuja kwenye Chuo cha Mafunzo kwenye ibara ya 145 na 151 katika ukurasa 81. Naomba Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima uniruhusu kidogo ninukuu hapa, “Idara ya Chuo cha Mafunzo – ibara ya 145, “Mhe. Spika, Idara ya Chuo cha Mafunzo imeanzishwa kwa sheria ya Na.1 1980 na ina jukumu la kuwapokea, kuwalinda wanafunzi na mahabusu kwa lengo la kuwarekebisha tabia na kuwapatia taaluma ili wawe raia wema”. Mwisho wa kunukuu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, ni kubadilisha tabia, yaani ku-*turn mind* kutoka uhalifu kuwa raia wema. Hapa nilidhani Mhe. Spika, kwamba hiki Idara ya Chuo cha Mafunzo walimu wake wangelikuwa makini, serikali ingekuwa makini katika kuwawezesha walimu wa chuo hiki, kwa maana wale askari wetu kuweza kutoa taaluma hii ya kuwatoa watu katika uhalifu na, kuwapeleka katika tabia nzuri ili waweze ku-*cope* na jamii yetu.

Lakini la kusikitisha Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo kuna matatizo. Kuna matatizo na nimeshayapigia kelele mara nyingi hapa. Mimi niseme nina-*interest* kwenye Chuo cha Mafunzo kwa sababu nimeshawahi kukaa Chuo cha Mafunzo karibu mara tatu kule. Kwa hivyo Chuo hiki ninakijua juu chini, sijawahi kukaa kwa uhalifu lahasha nimekaa kule kwa matatizo ya siasa za nchi. Ninashukuru katika kitabu hiki Mhe. Spika, Mhe. Waziri kasema hakuna mtu mmoja aliyeopo kwa kosa la kisiasa. Mimi nilikuwa nimeshakaa karibu mara tatu kwa kosa la siasa.

Sasa Mhe. Spika, kuna matatizo kwenye chuo hiki. Hebu tuone Mhe. Spika, jinsi ya matatizo yaliopo kwenye Chuo cha Mafunzo. Kwanza violation ya human right kwa kiasi kikubwa. Kwenye Katiba ya Zanzibar ibara ya 15, naomba taratibu niinukuu. Mhe Spika, haki ya faragha ya mtu na usalama, naomba niunukuu hii ibara, "Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata kuhifadhi na nafsi yake, maisha yake binafsi na nyumbani kwake na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake". Mwisho wa kunukuu Spika.

Mhe. Spika, kama kuna pahala hapana haki ya faragha ni violation ya Katiba yetu hii ni pale Chuo cha Mafunzo. Tena si kwa yule mwanafunzi tu lakini hata mahabusu ambaye ni mtuhumiwa. Mhe. Spika, unapoingia Chuo cha Mafunzo mambo unayofanyiwa basi ni kinyume ya mambo ya binadamu.

Mhe. Spika, mimi nimeshaingia pale na mwanafunzi basi karibu mwaka mzima nikimuona yule mwanafunzi wangu ninamkimbia. Yaani tulivuliwa tukaekwa uchi wa mnyama pale eti tunapekuliwa, si tusingeekwa kwenye chumba tu, pale pana uwanja wa shaba sote wanatupekua na halafu wanapiga makora pale pale. Hili ni tatizo. Huu ni unyama, huu ni uhasidi, huu ni uhuni.

Wajue kama hawa mafunzo hayo magwanda waliyovaa hivyo vyeo walivyonavyo tunawalipa kupitia migongo yetu sisi walipe kodi wasitunyanyase kiasi hicho. Inasikitisha sana Mhe. Spika, vyumba wanavyo basi mtu kama anataka kupekuliwa achukuliwe apelekwe faragha japo akavuliwa nguo kule ni faragha lakini mbele ya wenzake. Huu ni ushenzi mkubwa na hauvumiliki.

Mimi ninadhani Mhe. Spika, ikiwa umekwenda pale kurekebishwa tabia wavuliwa nguo mbele ya mwenzako munaonana kila kitu, hiyo tabia itabadilika kweli, kutoka raia mbaya kwenda mwema si rahisi.

Jengine ni suala zima la faragha imekosekana. Wamesema wanajenga vyoo katika mahabusu Ubago, kasema hapa Mhe. Waziri. Lakini vyoo hivi wanavijenga nje, vinatumika mchana tu. Usiku Mhe. Spika, ni aibu.

Mhe. Spika, usiku hakwendeki chooni magerezani. Kuna mtondoo. Mhe. Spika, mtondoo ni ndoo. Maana yake bora nikufahamishe uujuwe huo mtondoo ni ndoo. Ndoo inaekwa hapo, chumba kina watu 15, uende chooni hapo hapo kwenye ndoo na wenzake wakikutazama hivi. Jamani hiyo si hatari hiyo.

Mimi ninasema kwamba mfumo mzima wa magereza katika nchi hii haufai. Kuna haja ya kufanya mabadiliko makubwa kwa sababu wanaopelekwa magerezani ni binadamu na si wanyama. Anayeweza kwenda haja mbele ya mwenzake ni mnyama tu na si binadamu. Kwa hivyo mukitupeleka haja mbele ya wenzetu munatubadilisha tabia kutoka wabaya kwenda kwenye raia wema, hii si kweli.

Jengine hapo hapo Chuo cha Mafunzo. Kama kuna sehemu ambayo inavutwa bangi kwa wingi basi ni pale magerezani. Mimi nimekaa vipindi viwili tofauti, miezi mitatu tofauti niliyokaa pale ikifika usiku kile chumba nilichokaa wale jamaa wanapuliza ile bangi, lile moshi wote unatuingia, nimepata ugonjwa wa kichwa gerezani mule kwa bangi inavyovutwa vibaya.

Sasa nadhani ukimchukua mtu kama havuti bangi, akiwa kama si hamili kama nilivyokuwa mimi basi akitoka gerezani atakuwa ni mvutaji mzuri wa bangi. Kwa hivyo badala ya kumfanya raia wema wewe, unamfanya raia mbaya. Ni tatizo hili Mhe. Spika.Sasa ili niendeleze yale mafunzo naomba kidogo kidogo niteremshie maneno ili nisije kwenda kinyume na yale mafunzo yetu juzi kule.

Sasa niende katika Baraza la Manispaa. Baraza hili linapata kodi yake ukitoka kwa wananchi wote. Uongozi wa Baraza la Manispaa wa mji wa Unguja ulikuwa hautakiwi kufanya ubaguzi wa jambo lolote.

Mhe. Spika, inasikitisha kama kuna pahala ambapo panaendeshwa mambo yao ya ubaguzi kuliko pale Baraza la Manispaa ya mji wa Unguja. Katika Manispaa hii kuna maeneo ambayo mlala hoi hunyang'anywa tu hivi, akaambiwa panataka kuboreshwa. Kumbe kuna jamaa yake anataka kumpa.

Sasa katika hili. Katika maeneo ya Michenzani kwenye Idara ya Majenzi, kuna vijana waliondoshwa pale kwa mnasaba eneo lile linataka kufanywa eneo la matumizi ya serikali. Lakini kwa taarifa tulizonazo yule kijana kanyang'anywa eneo ili mkurugenzi ampe jamaa yake.

Hili asije kuthubutu kufanya Mhe. Spika. Ikiwa eneo lile kamnyang'anya mlalahoi linataka kutumiwa na serikali basi patumiwe na serikali lakini akichukua yeye akimpa jamaa yake, basi tutahakikisha tunaondokana naye mbele kwa mbele. Ninamtahadharisha sana katika hili.

Mhe. Spika, nimalizie kwa hawa ndugu zetu Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Tumeambiwa hapa Wazanzibari huenda Rais akazungumza nao, akakutana nao. Ninataka sasa nijue mipango ya serikali, wale kama Wazanzibari wanasaidia nini katika uchumi wa nchi yao, hilo mosi.

Pili wenzetu katika nchi mbali mbali, kwa mfano kama China wanawatumia wale na uchumi wao umekuja juu sana. Jee Mhe. Waziri anaweza kuniambia ni *strategic plan* gani aliyotayarisha kusudi kuona ndugu zetu wanaoishi nje ya Zanzibar wanavyoendeleza uchumi wa nchi hii.

Tatu wale ni Wazanzibari, jee ni lini watafikiria kuwapatia *dual citizenship*, ni lini watafikiria kitu hicho. Jengine ni wale wana haki za msingi katika nchi yao, kama walivyo Wamakonde waliopo hapa. Wamakonde waliopo wanafanya maamuzi mpaka ya kuchagua kiongozi wao kule Msumbiji. Jee ni lini wale watashirikishwa katika maamuzi makubwa ya nchi ikiwa ni pamoja na kuchagua viongozi wao.

Wale Wazanzibari wanaoishi nje ya Zanzibar na wao ni lini watashirikishwa katika suala zima la kuchaguliwa viongozi wao kama wanavyoshirikishwa ndugu zetu wa Kimakonde na nchi nyengine.

Ahsante sana Mhe. Spika, nitaunga mkono hoja pale nitakaporidhika sana kuhusiana na mambo haya ya mtondoo, mambo ya Baraza la Chake-Chake. Ahsante ahsante sana.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kunipa fursa ya kuzungumza machache kuhusiana na mpango huu wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, ninachokifahmu kwamba hapo nyuma tulikuwa tuna mivutano ya kisiasa na ilifikia labda serikali ikaona sasa kuna umuhimu wa kuweka kitengo cha kupeleleza au labda cha kutafuta siri au mfanyakazi atakuwa na sifa gani. Naamini kwamba hivi sasa Mhe. Spika, tumefikia wakati kwamba utaratibu ule au yale yaliyokuwepo, hizo siku za dahari za kiza yameshaondoka. Sasa ni imani yangu kwamba vitengo hivi kwa hivi sasa kama vitaendelea kuwepo, basi utendaji wake wa kazi hautakuwa tena, mimi sina imani kwamba utakuwa ni wa kawaida.

Kwa hivyo, ningependa kusema kwamba hivi sasa vitengo kama hivi visingekuwa na umuhimu mkubwa, kiasi kwamba tukaona tunaviboresha na kuviingizia pesa, bali vitengo hivi tungeviachilia vikaendelea kufariki dunia na tukawa hatunavyo tena katika nchi yetu. Kwa sababu imani yangu ni kwamba tunajenga taifa lenye utawala bora. Sasa kama tunajenga taifa lenye utawala bora na taifa la haki za binadamu, kwa nini tena tuwe na vitengo kama hivi ambavyo vitampekua mtu kumwangalia wewe nani, wewe vipi au wewe au ulifanya vipi. Kwa hivyo, mimi nahisi sasa tuachane na utaratibu huo, tuende na utaratibu ambao una uwazi.

Mhe. Spika, lakini katika hili bado linaendelea na ningependa nimuulize Mhe. Waziri, kwa sababu watu ambao wanapitia katika kitengo hiki, mimi nafahamu ni kama watu ambao wamepita katika mitihani. Sasa unapofanya mtihani mara nyingi huwa na hamu ujuwe matokeo yako kwamba mimi nimepasi au nimefeli, na kama nimepasi nimepasi vipi na kama nimefeli nimefeli vipi. Wale wa Baraza la mitihani wanakuwekea aidha C au A au B au wanakuambia wewe umepata *grade* 4. Sasa sijui utaratibu kama huo upo ili kuondoa yale malalamiko, kwa sababu wanaokwenda kufanya mitihani kama hii wanakuwa ni wengi. Sasa je, sijui kumeandaliwa utaratibu gani wa kuona kwamba wale waliofika katika kitengo hiki wanapata majibu na kuridhika au japo wasiporidhika, lakini wamejiona udhaifu wao. Kwa sababu kama yeye akiwa ni raia wan chi hii atajifahamu zile kasoro zake, atafahamu aah! Kumbe

mimi kasoro zangu ni moja, mbili na tatu, kwa maana hiyo natakiwa mimi nijirekebishe katika moja, mbili na tatu, ili nafasi itakapotokea mara ijayo na mimi niweze kufikiriwa.

Mhe. Spika, nije kidogo katika ukarabati na ujenzi wa ofisi zilizomo katika Wizara hii. Mhe. Spika, ninachokifahamu kwamba katika nchi yetu tuna Tume ya mipango, na ni imani yangu kwamba Tume hii huwa inakaa na kuangalia kwamba nini kifanyike na kwa nini kifanyike na kwa wakati gani kifanyike.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alikuja hapa akatuambia kwamba tutaingiza senti hamsini katika mafuta, ili kuchangia maendeleo fulani ya jambo ambalo halipo. Hii michango yote inatokana na wananchi, na kodi hizi zinatokana na wananchi. Mimi wasi wasi wangu ni kwamba Tume hii huwa haiangalii nini hasa kinatatiza. Nikiangalia hapa nakuta matumizi ya ukarabati wa mawasiliano ya Ikulu yanakwenda karibu milioni 100, imani yangu ni kwamba hivi sasa mawasiliano yapo. Ukienda katika ujenzi wa Laibon utakuta ni milioni 400, nina imani kwamba Rais au wengine wakienda hawalali nje. Ukienda katika ukarabati wa majengo mengine karibu milioni 300, imani yangu ni hiyo hiyo kwamba majengo yapo na kazi zetu zinaendelea kama kawaida.

Sasa nilikuwa nikifikiria kwamba Tume katika kupanga kwake ingeangalia kwamba hivi sasa tuna umuhimu wa kuwa na madeski maskulini. Haya ambayo tunayo hivi sasa kwa nini tuyaendeleze tusiyaanzishe yale ambayo yana umuhimu zaidi, kiasi kwamba tunafikia kuwatoza wananchi kodi. Mhe. Spika, mimi hili nalihisi ni kinyume na ule mpango wetu wa MKUZA wa kuona kwamba tunatoa kipaumbele kwenye masuala gani na kwa wakati gani.

Mhe. Spika, katika kitabu chetu kwenye mpango wetu huu, tumepanga pia kuwaona na kuratibu wale watu ambao Mhe. Saleh aliwataja *Diaspora*. Ninachokijua mimi ni kwamba Wazanzibari wengi walioondoka hapa, hivi sasa sijui tuwaite Wazanzibari au tuwaite nani, kwa sababu walioko Uingereza naona watakuwa wanapata uraia wa nchi zile, walioko Arabuni naona na wao watakuwa wamepata uraia wa nchi zile, si hivyo wasingeishi katika nchi zile. Sasa hawa Wazanzibari tunaotaka kuwaorodhesha ni Wazanzibari wenye sifa gani, ni Wazanzibari ambao walizaliwa Zanzibar baadae wakaenda kukulia kule. Katika hili kuna ziara ambayo imefanywa katika nchi za Kiarabu, sijui matokeo yake ni nini, baada ya kufanya ziara wale tuliowaona walikuwa na hamu gani ya kuja kuwekeza katika nchi yao.

Mhe. Spika, mbali na hayo ni kwamba labda katika kuwashawishi wananchi hawa waje, tulihitaji kwanza sisi wenyewe tuangalie, je tunayo mazingira ya kuwatia hamu hawa ambao tunawahesabu Wazanzibari kuja hapa. Nikiangalia mimi sioni kama kuna miundombinu ya kutosha ya kuwafanya watu hawa warejee katika nchi zetu na kuja kuwekeza. Lakini kama nilivyosema mwanzo ni kwamba wananchi hawa waliondoka katika mazingira tofauti.

Mhe. Spika, nafikiri tunakumbuka yaliyotokea. Je, serikali sijui imeona umuhimu wa kuwaita hawa, kwa sababu wengine walikimbia kwa sababu mali zao zilikuwa- *confiscated* au *nationalised.* Sijui serikali ina mpango hivi sasa kwa wale ambao waliondoka na mali zao zilikuwa zimekuwa *nationalised* au *confiscated* na *Government.* Je watarudishiwa wenyewe ili waone kweli serikali imekuwa na uwazi katika suala hili, kiasi cha kuweza kuwashawishi wao warejee katika nchi yao.

Mhe. Spika, wengi wamezungumzia suala la vitambulisho vya Mzanzibari, na mimi naomba nitie chumvi kidogo katika hili. Nafikiri sheria ya ukaazi imekuja kama miaka 7 nyuma. Toka kuja kwake sijamsikiapo Mjumbe hata mmoja aliyesimama hapa na kusema kwamba sheria hii haina matatizo. Pia Mhe. Waziri anapokuja hapa huwa na yeye anapata malalamiko mengi, na anajitetea kwa nguvu zake zote kwamba kuna moja, mbili na tatu. Lakini namuomba atambue kwamba mpaka hivi sasa kuna matatizo katika sheria hii, na kwa vile kuna matatizo kuna haja ya kufanya marekebisho. Tulipokuwa tunataka kuwatoza wananchi kodi, juzi tu tulileta marekebisho ya kanuni za fedha hapa, na tukaamua moja kwa moja. Kwa hivyo, na hili nahisi kwamba hivi sasa tumeshafikia kuwa tuna matatizo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri mara nyingi huwa majibu yake ni kuwa tukae pamoja, tufanye shura na tuamue nini. Mimi nafikiri kama una watendaji wazuri, basi washajua tatizo ni nini katika suala hili. Kwa hivyo, suala hili linahitaji lifanyiwe utaratibu wa haraka sana, isiwe kila siku tunakuja hapa tunaambiwa aah! Wananchi hawataki kwenda kuvichukua, hilo sio tatizo, tatizo wananchi hawapewi. Kama hajenda kukichukua basi siku yoyote atakwenda kukichukua.

Lakini labda nitoe mfano mzuri wa Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Waziri wa Katiba na Sheria. Yeye alipoona kuna vyeti vingi vimerundikana katika ofisi yake, aliandaa utaratibu wa kuwafikia wananchi wale katika sehemu zao wanazokaa. Hivi sasa ukienda wananchi wengi sasa hivi hawalalamikii vyeti vyao vya kuzaliwa, ukiacha wale ambao vimepotea kwa njia nyengine, ninahisi hili atalifanyia kazi vile vile.

Mhe. Spika, ukienda kwenye vitambulisho, utaambiwa hawajaja kuvichukua na aliyepewa fursa ya kumtambua huyu mtu ambaye anahitajika kupewa kitambulisho Mhe. Spika, ni mtu mmoja, sijui kwa nini akapewa uwezo kama huu. Mimi ninachojua katika Baraza letu tukufu hapa, hivi sasa tunatunga sheria pengine Mkurugenzi wa Baraza la Mji, basi anatakiwa awe na sifa mfano, moja kamaliza Chuo Kikuu na kafanya hivi na hivi, kwa maana awe na uelewa. Lakini leo ukienda kwa wananchi wetu hawa ambao tunawapa kazi kama hii, hawana uelewa. Sijui ni wangapi wanajua kusoma na kuandika Mhe. Waziri katika watu hawa ambao tunawapa kazi hii ya kumtambua kwamba huyu ni mkaazi ama si mkaazi. Utasikia huyu Sheha ana katibu wake, kwa nini. Kwa hivyo, nafikiri wakati umefika sasa, hata kama sheria bado ipo ya kuwa sheha awepo, lakini bado awe na uelewa wa jamii yake, Sheha ni chanzo cha uchumi, sheha ni chanzo cha uelewa wa wananchi, lakini yeye hana uwezo huo.

Mhe. Spika, ni lazima tukubali kwamba Mwenyezi Mungu ameshatuambia, kuwa kuna wanaofahamu na wasiofahamu, tumeambiwa hilo. Pia akasisitiza na kusema kwamba hata hao wanaofahamu basi kutakuwa na wanaofahamu zaidi kwamba "*Wafauqa Kullu dhuu ilmin Aliym*", mbali na wale wanaojua, kuna wengine wanaojua zaidi. Ndipo pale Mhe. Waziri akatupigia mfano kwa yule mdudu anayeitwa buibui. Mdudu yule sifa yake kubwa ni kwamba wanajenga uhusiano mke na mume. Lakini katika uhusiano huo, mazao ya mke na mume ni kupata mtoto, lakini maisha ya buibui yule ni kwamba mmoja wapo katika watatu akishakamilika basi mmoja hulazimika afe anakuwa hafaidiki chochote. Sasa jambo hili wengi walikuwa hawalijui na mpaka sasa hawajui, lakini kuna wachache tu ambao wanalijua. Kwa hivyo, hii ni kuthibitisha kwamba tayari kuna umuhimu wa kwamba anayepewa kazi ile ya kufanya, anatakiwa awe na uelewa.

Mhe. Spika, mimi nashangaa sana kwamba inafika hadi katika nyumba mke ni mkaazi au mume ni mkaazi, lakini mke si mkaazi hana kile kitambulisho. Sijui inakuwaje, na pengine yule mtu anakaa katika kaya yake ile kwa miaka mitano au sita tayari wana watoto ambao wamepatikana na wale watoto wana ukaazi ambao wameupata pale, lakini yule mama anaambiwa wewe si mkaazi, hiki ni kichekesho.

Mhe. Spika, katika katiba yetu ya Zanzibar tumeambiwa kwamba watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. Sasa tuliomo humu tumeapa kwa sheria hii, sijui tunaitekeleza vipi. Najua kwa vile Mhe. Waziri atakuja mwisho basi atakuja kusema, kwa sababu na yeye ana haki ya kusema, lakini hapa bado lipo tatizo katika vitambulisho, wananchi hawapati haki yao hii ya vitambulisho. Tunachokuomba Mhe. Waziri uandae utaratibu, tukimaliza bajeti, kama ulivyopendekeza kwamba utakuwa tayari kufuatana na sisi. Mimi niko tayari nitapitia mikoa yote na wilaya zote, usinipe posho yoyote, ili nikuoneshe matatizo, nitafanya *study* na hawa wataalamu wako ili tukuoneshe tatizo liko hapa.

Mhe. Spika, watu katika nchi kama hii ambayo inajenga misingi ya haki na demokrasia hawafai kubaguliwa, Mwenyezi Mungu kakataza hili na wewe kama ni binadamu unatakiwa usiwabague. Leo unakwenda wananchi wanakuambia mimi nimeshindwa kupata huduma fulani kwa sababu sina ukaazi, mtu miaka 60 amezaliwa pale, sheha amekuja amemkutia pale amehamia, unamnyima haki yake, unafikiria wewe malipo yako nini.

Mhe. Spika, mimi naomba hili Waziri aliangalie, atakuja kujibu kisiasa, sawa,lakini kama alipendekeza yeye basi tuunde utaratibu wa kuona suala hili limemalizwa mapema iwezekanavyo, ili tutakapoingia katika uhesabuji wa watu, basi wananchi wajisikie kwamba na wao ni wakaazi wa kisiwa hiki cha Zanzibar. Si hivyo, wananchi wanaweza wakachukua uamuzi mwengine na huko baadae yakatokea maamuzi mengine.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe bado dakika tano tu.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Mhe. Spika, niende kidogo katika KMKM, nitamalizia na Vikosi Maalum. Mhe. Spika, pia nilikuwa najua kwamba wakati wa miaka ya 1990 kulikuwa kuna vita baridi ulimwenguni, kwa maana hiyo nchi nyingi ulimwenguni zilijiandaa, kufanya nini, kwamba na wao wakati wowote wakija kushambuliwa basi wawe na vikosi vyao vya kuweza kujilinda.

Mhe. Spika, hivi sasa tunavyo vikosi vya KMKM, JKU na KVZ ambavyo kazi zao, kwa mfano KMKM wao kazi yao ni kuzuia magendo na mambo mengine. Lakini hivi vikosi vimekuwa kama ni vikubwa, kwa sababu nikienda katika bajeti ya kikosi cha KMKM Mhe. Spika, utakuta karibu bilioni 9. Ukiangalia kikosi hiki sijui kina wafanyakazi wangapi, na kazi zake wanazofanya ni chache sana, kwa maana hiyo nahisi karibu bilioni 7 zinakwenda katika mishahara tu. Sasa kama ni hivyo na hivi sasa nasikia fununu kwamba vikosi wanataka kuajiri tena. Hivi hili jukumu lao ni lipi, hatujafikia lengo la kwamba hawa askari wetu hawajatosheleza tu, kiasi kwamba kila siku tuajiri wafanyakazi kama hawa.

Mhe. Spika, naheshimu wakati wako naomba nikae, ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii ya kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Halafu nichukue fursa maalum ya kukupongeza wewe Mhe. Spika. Vile vile niwapongeze vikosi hivi vya Idara maalum ya SMZ kwa kazi kubwa ambayo wameifanya wakati wa ajali ile ya meli ya MV Spice Islander.

Mhe. Spika, kazi waliyoifanya ni kubwa na wanastahili pongezi. Kwa hivyo, ni wajibu wetu sisi kuwapongeza kwa sababu ni suala ambalo ni la kujitolea la kuwaokoa wenzetu ambao walipoteza maisha, na wengine kuwanusuru waliokuwa hai. Kwa hivyo, nawapongeza sana.

Mhe. Spika, nianze na Mamlaka ya Serikali za Mikoa, nikianzia na Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Spika, Mkoa wa Mjini Magharibi ndio mkoa mama, na ndio mkoa ambao unaongoza mikoa yote katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mkoa wa Mjini Magharibi katika taarifa yake Mhe.Waziri ameeleza masuala ya wanyama ambao wanazurura ovyo mitaani, pamoja na tatizo la uchimbaji ovyo wa mchanga.

Mhe. Spika, hivi karibuni Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shein, alitoa kauli ya kuhusiana na wanyama ambao wanazurura ovyo, na wale ambao wanatumishwa kwa gari za punda na gari nyengine ambazo zinatumia wanyama. Nimelizungumza hili Mhe. Spika, kwa sababu hivi juzi tu, wakati natembea barabarani niliwahi kushuhudia ajali ambayo ilisababishwa na wanyama, yaani punda. Yule punda alikuwa kabeba mizigo ya mbao, lakini punda ni punda, akili zake za punda ni za kipunda. Kwa hivyo, yule muongozaji wa yule punda au ile gari ya punda ikawa kazidiwa nguvu na yule punda, kwa hivyo ikatokea ajali.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningemuomba sana Waziri, hili suala alichukulie uzito kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa pamoja na uongozi mzima wa mkoa, ili kuhakikisha kwamba suala hili linaondoka katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi. Kwa sababu kila unapopita katika mitaa yetu ya mji wetu, basi utakuta gari za punda na punda wanatembea ovyo ovyo, wanyama wanatembea ovyo ovyo na kusababisha ajali. Kwa kweli suala hii sio sura nzuri katika mji wetu huu, ambapo wanakuja watalii mbali mbali, wakiona hali kama hii kwa kweli ni aibu sana, hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri akalifanyia kazi sana.

Nikiondoka katika suala hilo Mhe. Spika, nije kwenye Serikali za Mitaa, Manispaa ya Zanzibar. Mhe. Spika, hali ya mji wetu kwa kweli bado unatilisha aibu, mbali na juhudi kubwa ambazo zimechukuliwa na uongozi mzima wa manispaa katika kuweka usafi katika mji wetu, pembezoni mwa barabara. Lakini Mhe. Spika, hali ya usafi wa mji wetu bado ni tete. Ukiangalia katika maeneo mbali mbali ya mji wetu huu, hasa katika maeneo yale ya majumba ya Michenzani, katika mitaa ya Mlandege, Gulioni kwa kweli hali ni mbaya.

Hivi karibuni tu Mhe. Spika, katika eneo la Mlandege karibu na Mabluu kule, kuliwahi kutokea moto kutokana na takataka ambazo zimerundikana pale, moto ukawaka na watu wa *fire* wakaja. Kwa hivyo, ni taka zile ambazo zingehatarisha maisha ya wananchi na mali zao kutokana na takataka zile.

Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri pamoja na uongozi wote wa Manispaa ya Mji wetu wa Zanzibar, kuhakikisha kwamba masuala ya takataka katika maeneo hayo, hususan katika maeneo ya mjini, basi yaondoke na tuuweke mji wetu katika hali ya usafi na wa kuvutia.

Mhe. Spika, kama nilivyozungumza kwamba manispaa wamejaribu kuweka vigae mule kando kando ya barabara, zinaleta sura nzuri na haiba nzuri ya mji, lakini ningemuomba Mhe. Waziri kwamba ahakikishe kuwa pamoja na Uongozi mzima wa manispaa na Meya wa Mji wa Zanzibar, kuweka haiba ya mji wetu katika eneo la macho ya mji wa Zanzibar pale Darajani.

Mhe. Spika, ile kazi ambayo inafanywa ya kuweka vigae kando kando mwa barabara, basi ipo haya pale katika mji wa Zanzibar, macho ya Zanzibar Darajani, pale wanapoegesha magari. Mhe. Spika, napo pale vigae vitiwe, pale ndio sura ya Zanzibar. Leo wageni wetu wanapokuja, watalii wakifika hapa wakiambiwa huu ndio mji mkuu wa Zanzibar, kwa kweli ni aibu. Unapokuwa na mgeni ukifika pale utamwambia huu ndio mji wa Zanzibar hapa ndio mjini, unainamisha macho chini Mhe. Spika.

Kwa hivyo, ule utaratibu wanaofanya kule wa kutia vile vigae kando kando mwa barabara, basi na pale Darajani kwenye eneo la kuegeshea magari kung'are, kwa sababu uso unapoosha uso na sabuni ukang'ara, basi utaonekana mwili mzima unang'ara, kumbe umeosha uso tu Mhe. Spika. Kwa hivyo, ule uso wa Zanzibar Mhe. Spika, ung'are.

Halafu Mhe. Spika, nizungumzie yale maeneo ya pale Bwawani. Mhe. Spika, niliwahi kuzungumza na Waziri, akaniambia kwamba kuna mambo mazuri yanakuja pale Bwawani. Lakini kabla hayajaja basi tuweke mandhari nzuri, tupande miti mizuri pale, tuweke usafi na tuweke mazingira mazuri. Leo wageni wetu wanapokuja wakiteremka kwenye meli bandarini kule wanapita pale, watalii wanapokwenda Forodhani wanapita pale, na ile hali wanayoikuta pale ni ya kusikitisha. Mhe. Spika, tuweke mandhari ya mji wetu safi. Namuomba sana Mhe. Waziri alifanyie kazi suala hili, hata hapo mambo yatakapokuja, basi *Inshaallah* ndio tunavyoomba, kama ulivyoniambia suala hili na mimi naamini, na ninaiamini sana serikali hii, kwamba mambo yatakuja mazuri, lakini tuweke usafi.

Mhe. Spika, tusikae tu kwa sababu tunaletewa sabuni, lakini japo huna sabuni kwanza japo maji kwanza uoshe uso wako.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la vyoo katika mji wetu. Mhe. Spika, nasikitika hali ambayo wananchi wetu wanavyokwenda haja katika maeneo ya mji wetu katika vichochoro. Hii inasikitisha. Mhe. Spika, ukija kwenye maeneo yale pale Michenzani kwenye makontena. Nakuomba Mhe. Spika, siku moja ufanye ziara, utembelee pale Michenzani kwenye makotena, utembeetembee mule ndani, utasikitika Mhe. Spika, watu wanakojoa ovyo, watu wanakwenda choo kikubwa ovyo na uchafu unatupwa ovyo.

Lakini cha kusikitisha zaidi Mhe. Spika, kama miezi mitatu au minne iliyopita, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alikuwa mgeni rasmi pale Michenzani katika uzinduzi wa wajasiriamali pale wa *Sunday market*. Kwa hivyo, lilitoka pendekezo Mhe. Spika, kujengwe choo na mfadhili alipatikana ni benki yetu ya PBZ, na lilifuatiliwa vizuri suala lile. Lakini cha kusikitisha Mhe. Spika, mpaka leo Mkurugenzi wa Manispaa hajatoa barua au kibali cha kujengwa choo kile. Hili ni jambo la kusikitisha Mhe. Spika. Mfadhili keshapatikana wa kujenga choo cha kisasa cha kuwahudumia wananchi wetu pale, lakini kibali kinazungushwa, hili ni jambo la kusikitisha sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kujibu maswali haya, basi atueleze hali halisi ya kibali kupatikana, ili choo pale kijengwe ili kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mhe. Spika.

Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa asubuhi kupata nafasi ya kutoa yangu machache katika bajeti ya Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kutoa maoni yangu kidogo. Mhe. Spika, mimi nianze moja kwa moja katika suala la vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Nianze na swali kwamba sote tunaitwa Wazanzibari Wakaazi, na huyu Mzanzibari halisi ni yupi? Kwa hivyo, ikiwa sisi sote ni Wakaazi tu wa visiwa hivi yule ambaye ni halisi ni yupi? *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze na kifungu cha 61 (a) na (c) naomba ninukuu kidogo

Kifungu cha 61 (a) kinaeleza hivi:-

a) “Imesajili Wazanzibari wakaazi 10,578 waliotimiza masharti ya usajili, na kutengeneza upya vitambulisho 3,932 ambavyo vimemaliza muda wake wa matumizi na kuvigawa kwa wahusika”.

Mhe. Spika, inawezekana ikawa hao wamesajiliwa. Lakini nataka nije na swali katika kusajili kuna sisi Wazanzibari wazaliwa pamoja na kwamba tunaitwa Wakaazi, wengine wanatakiwa waishi hapa kwa muda maalum wenzetu kutoka upande wa pili na hatimae na wao wanapewa Uzanzibari.

Je, hawa wa upande wa pili zaidi ya hili sharti la ukaazi kwa muda uliokubaliwa hakuna sharti jengine, kwa sababu sisi awe na cheti cha kuzaliwa, sheha amtambue na sheha anaweza kumkataa mwanawe ikiwa siye. Sasa kwa hawa upande wa pili, baada ya ule muda uliokubaliwa na serikali kuwa amekaa hapa, hivi hakuna sharti jengine na kusajiliwa tu moja kwa moja.

Mhe. Spika, kama ni hivyo huyu Mzanzibari Mkaazi ambaye ni Mzaliwa hatendewi haki kama huyu hana sharti jengine la kuzaliwa, baada ya lile tu awe ni mkaazi na kwa muda uliokubaliwa.

Vile vile tumebaini kuwa kutokana na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwamba wako watu ambao hawana sifa za Uzanzibari na wamesajiliwa, ingawaje ametetea kuwa wamefutwa, lakini wamesajiliwa na wala si kwa makosa, yaani kwa makusudi kabisa.

Mhe. Spika, kuhusu jambo hili kwa kweli serikali mara zote wanapoulizwa swali hili wanatetea kuwa yeyote aliyefanya hivi si kweli hakuna. Lakini mimi nadhani masheha ni watu wenye akili zao, haiwezekani serikali hii iwe inakataza kweli na halafu yeye afanye vile serikali inavyokataza.

Kwa hivyo, haiwezekani kwa sheha kwamba serikali inataka mwenye sifa ndiye asajiliwe, lakini sheha akienda mtoto mwenye sifa, cheti cha kuzaliwa anacho na kumwambia hakuna fomu leo na kesho kutwa, lakini kwa serikali inasema sheha mwenye kufanya hivyo ana matatizo tena ni makosa, mimi sidhani kama ana matatizo na makosa.

Sasa nilichokiona hapa ni kwamba serikali inatuambia lugha nyengine na halafu kwa hawa wanawanong’oneza ah! Pale tuachieni tu, endeleeni na mwendo huo, hofu yangu iko hivyo.

Mhe. Spika, tatizo la kusajiliwa Wazanzibari lipo, tena wengine wanazo sifa na wala hawasajiliwi. Kwa vile ambavyo vinavyotajwa kwamba vimerundikana, Mhe. Spika mtu anakwenda anatafutwa haonekani, na kipo na atakwenda leo na kesho anatumia nauli na hatimaye anavunjika moyo.

Mhe. Spika, vile vile kifungu cha 61 (c) naomba ninukuu kidogo

Kifungu cha 61 (c) kinaeleza hivi:-

(c) “Imeandaa Rasimu ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili Namba 7 ya 2005, ili kuruhusu utoaji wa vitambulisho vya wageni wanaoishi nchini, rasimu hiyo tayari imeshapita Baraza la Mapinduzi na inasubiri kuwasilishwa kwenye Baraza lako Tukufu. Taratibu zote za kiutendaji zimekamilika, ikiwa ni pamoja na mfumo wa utengenezaji wa vitambulisho hivyo, pamoja na fomu za maombi ya usajili”.

Mhe. Spika, hii mimi siungi mkono kwa sababu huyu mwenyeji hasajiliwi na tusajili mgeni. Kwa hivyo, naomba rasimu hii serikali ifikirie zaidi kwa huyu Mzanzibari hasa usajili huu haupati inavyostahiki, lakini tayari tunaandaa rasimu ya kuwapa wageni vitambulisho, ingawaje nadhani huenda vikawa tofauti na sisi tunaoitwa Wazanzibari Wakaazi, lakini vyovyote ah! Sijaona kama kuna busara yoyote ya kumsajili mgeni na kumuacha yule muhusika kupata usajili mwanzo.

Mhe. Spika, mimi kwa upande wangu hili bado sijalikubali vyema na wala sijaliunga mkono.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye kifungu cha 63 (a) na (d), Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 63 (a) na (d) kinaeleza hivi:-

a) “Kuendelea kuwasajili Wazanzibari Wakaazi 10,500 wanaotimiza masharti ya usajili na kuwapatia Vitambulisho”.

Mhe. Spika, kama watawasajili kweli ni sawa, lakini naomba wawasajili Wazanzibari na wala wasisajili watu tu na halafu wakawa Wazanzibari.

d) “Kuanza kutoa vitambulisho maalum kwa wageni wanaoishi nchini kwa ruhusa maalum (*Residence Permit*), na kutunza taarifa zilizokusanywa kwa ajili hiyo katika *database* ya Serikali mara baada ya marekebisho ya Sheria ya Usajili Namba 7 ya mwaka 2005 kupitishwa na Baraza la Wawakilishi”.

Mhe. Spika, suala hili siliungi mkono kuanza kutoa vitambulisho vya wageni kabla ya sisi wenyewe kuwa sawa na kuwapa watu wengine, hili siungi mkono.

Kwa hivyo, naunga mkono kifungu cha (a) kama ni kweli watasajili Wazanzibari Wakaazi na wakishasajiliwa wapewe kwa muda unaotakiwa.

Mhe. Spika, mimi ninao ushahidi katika sehemu yangu kwamba mtoto amesajiliwa na akaambiwa njoo baada ya wiki mbili, alipokwenda akaambiwa bado na kupewa wiki mbili nyengine, alipokwenda akaambiwa bado, yaani imepita miezi 6, halafu mnatuambia kuwa hawavichukui. Mhe. Spika, wanahangaishwa sana, wanataabishwa pamoja na kuzungushwa.

Nikiondoka hapo sasa niende kwenye Halmashauri na kidogo nitazungumza katika Halmashauri yangu ya Mkoani. Mhe. Spika, kifungu cha 121 (b), naomba kunukuu.

Kifungu cha 121 (b) kinaeleza hivi:-

(b) “Imesaidia ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Msikiti wa Michenzani, madarasa Chumbageni, Skuli ya Sekondari Kengeja, Skuli ya Msingi Mahuduthi, Daraja la Mto Mkuu Kengeja, madarasa ya Kengeja na Mwambe vyenye thamani ya shilingi milioni 4”.

Mhe. Spika, hapa nataka ninukuu haya yanayohusu katika jimbo langu tu. Vifaa gani vya ujenzi ambavyo vimesaidia katika Skuli ya Msingi Mahuduthi, Skuli ya Sekondari Kengeja na madarasa ya Kengeja, kwa sababu hapa umeelezwa tu kwamba wamesaidia vifaa vya ujenzi. Kwa hivyo, nataka kufahamu ni vifaa gani vya ujenzi serikali kupitia ofisi hii ilivyosaidia katika sehemu hizo ambazo zimo katika jimbo langu.

Vile vile kifungu cha 121 (d) naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 122 (d) kinaeleza hivi:-

(d) “Kusaidia shughuli za maendeleo ya wananchi katika Wadi ya Kisiwa Panza, Chokocho, Kangani, Mtambile, Kiwani na Mkanyageni”.

Mhe. Spika, pia nataka katika maeneo ya jimbo langu ya Kangani na Mtambile, shughuli gani za kimaendeleo katika sehemu hizi mbili, kwa sababu hapa hawakusema watasaidia shughuli gani, isipokuwa wametaja tu watasaidia shughuli za maendeleo. Kwa hivyo, napenda kujua ni shughuli zipi ambazo hapa zimekusudiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kifungu cha 121 (d) naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 121 (d) kinaeleza hivi:-

(d) “Imeweka kifusi barabara ya Likoni/Kengeja na Msikiti wa Maambani, Chambani.

Mhe. Spika, kwa sentensi hii wizara inaonesha kuwa hii barabara ni wao peke yao ndio waliotia kifusi, lakini hali halisi si kweli. Kwa hivyo, ni vyema wangetumia lugha wamesaidia, kwa sababu wakisema wametia maana yake wametia wao peke yao, mimi binafsi nimechangia. Hivyo, wao wakichukulia kwamba wamefanya peke yao na sentensi hii si kweli. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, basi naomba sentensi hii angalau irekebishwe na isiwe kama ilivyo na kuonekana kuwa wao ndio wamefanya peke yao.

Mhe. Spika, sasa nije katika Baraza la Manispaa la Mji wetu wa Unguja, hapa Darajani kwa vyovyote ilivyo ndio kioo cha Zanzibar. Kwa mfano, mgeni anapoingia katika mji huu anapata harufu ya kujiuliza, ni kweli hapa mjini, kwa sababu *perfume* anayoisikia ni harufu mbovu, mbaya tena inayochukiza.

Hali hii inatokana na kurundikana kwa taka, ambazo zimekusanywa bila ya kuzolewa na kuhamishwa. Mhe. Spika, hivi ni kweli serikali yetu hata kuzoa taka inashindwa, wakati kila mwenye kuweka taka anatoa kodi maalum kwa ajili ya kufanya kazi hiyo ya usafi. Serikali hatuoni haya, basi tutangaze kwenye *internet* kwamba tunaomba msaada wa kuzoa taka, ili mji wetu uondokane na ile hali mbaya iliopo.

Mhe. Spika, mji kuwa katika hali hii iliyo sasa ni jambo la aibu. Kwa kweli hivi sasa tunaelekea miaka 49 ya Mapinduzi na tunatangaza maendeleo mbali mbali, lakini tunashindwa dogo tu la kuufanya mji wetu uwe na sura halisi ya mji.

Mhe. Spika, kuna mambo hata ufanye jambo zuri gani, basi baya moja tu linayaficha mema yote mengine uliyoyafanya, na moja wapo ni kuwa wachafu wa kupindukia mpaka. Kwa hivyo, mazuri yote ambayo tumejiona tumefanya na maendeleo tunayosema kwamba tumefikia. *(Makofi)*

Lakini kwa kuwa tumeshindwa kuuweka mji wetu katika hali ya mji, na wenzetu mnaotembea mnaiona miji ilivyo, hivi huko mnakokwenda ni kweli miji iko kama mji wetu. Mhe. Spika, wanakwenda sehemu tofauti Waheshimiwa Mawaziri tena siku zote, sasa hivi ndivyo miji ya dunia ilivyo.

Vile vile kuna usumbufu wa upatikanaji wa leseni. Mhe. Spika, Baraza linatoa fomu kwa ada na vijana wanakwenda sehemu zote za kulipia kodi zao kama vile *ZRB* na sehemu nyengine, lakini hatimaye wakirudi Manispaa baadhi yao leseni halisi ya kufanyia kazi hawapewi.

Kwa hivyo, sijui hapa tunamkomoa mfanyabiashara au tunaikosesha mapato Manispaa pamoja na serikali kwa jumla, kwa upande mmoja kukosa mapato serikali nadhani haikereki. Lakini hapa lengo ni kumkomoa mfanyabiashara ambaye tayari ameshalipia kodi, sasa katika hatua ya mwisho leseni anazungushwa kama pia. Mhe. Spika, mtindo huu wa utendaji ningeliomba tuurekebishe, ili tujenge taswira nzuri ya serikali yetu katika maendeleo yetu ya kila siku.

Mhe. Spika, tumo katika utawala bora. Maana ya utawala bora ni kutenga haki kwa wote wanaohusika kupata haki hiyo. Katika ziara zetu za kamati tuligundua kuwa Halmashauri za Unguja na Mhe. Waziri atajibu kama alivyojibu kwenye swali, waliajiri watu wa kutosha katika kufanya kazi zao, lakini wale wa upande wa pili wa Pemba waliambiwa wamechelewa. Sasa sijui kwa nini upande mmoja wasichelewe na upande wa pili waambiwe wamechelewa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninaiomba wizara isilete taswira mbaya baina ya visiwa hivi viwili, kwa sababu hivi ni visiwa vimoja, watu wenye silka moja na sote tuko pamoja, kwa hivyo usifanye upande mmoja na ukaja kufikiria vyengine. Kwa hivyo, itakuwaje upande mmoja uajiri na upande wa pili uambiwe umechelewa. *(Makofi)*

Vile vile tumekwenda kwenye vikosi wametuambia kwamba wengine kuletwa huku ni sawa na kuletwa gerezani. Kwa kweli zile haki ambazo wanazopata wakiwa Unguja ni tofauti na wanapokuwa Pemba na wala hazikubaliani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninaiomba serikali isiwafikishe pahala watumishi wakaona kupelekwa Pemba ni kwenda gerezani, kwa sababu kwenda Pemba hawaendi kwenye kisiwa chenye hazina. Kwa maana hiyo, wanakwenda sehemu ya pili ya Zanzibar kwa ajili ya kufanya kazi kama wanavyofanya hapa Unguja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi kwa sababu zangu binafsi juu ya ofisi hii ninaomba nimalizie hapo na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa naomba nimkaribishe Mhe. Rufai Said Rufai na baada ya hapo tumsikilize Mhe. Marina Joel Thomas. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, na mimi sina budi asubuhi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu muumbaji, pia nishukuru kwa kupata nafasi hii.

Mhe. Spika, naomba kutoa maoni yangu machache kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mchango wangu nianzie kwenye ukurasa wa 57 kifungu cha 100 kuhusu Baraza la Manispaa. Mhe. Spika, serikali ilikuwa na dhamira safi kuanzisha Baraza la Manispaa, ili kuweka maeneo ya mji na pembezoni mwake yawe safi na uweze kupendeza kwa wageni pamoja na wananchi wenyewe waweze kuvutika na maeneo yale.

Mhe. Spika, nakumbuka hapo zamani mji wetu ilikuwa ikifika wakati wa jioni ulikuwa ukinukia harufu ya mawaridi na mambo mengine mbali mbali. Lakini wakati huu wa leo, mji wetu umekuwa ni mji katika miji michafu duniani basi Zanzibar inaongoza na imepoteza ile hadhi yake ya kizanzibari.

Kwa kweli tatizo sijui nini, kwa sababu sehemu zinazopangiwa vifungu vya fedha ni maeneo haya ya Manispaa. Vile vile Manispaa wenyewe ni wazalishaji wakubwa katika kukusanya mapato katika sehemu ya mji.

Mhe. Spika, nadhani katika nafasi hii umekosekana upendo, na siku zote panapokosekana upendo, basi maendeleo hayapatikani. Kwa hivyo, wananchi na wafanyabiashara wanadhalilishwa, na inafika wakati wananchi wetu au wafanyabiashara wadogo wadogo kuporwa biashara zao na hata vile vyanzo vyao vya biashara. Sasa hali ikifikia kama hii, mimi nadhani hakuna lolote linaweza kupatikana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika ichukue ile hali ya wafanyakazi wa Manispaa kwa kweli hawana matunzo ya aina yoyote, kama vile nguo za kufanyia kazi, *rain boot* kwa ajili kujihifadhi kwenye miguu yao, *gloves* za mikono na hata kile kifaa cha kuzibia hewa chafu kwenye mdogo.

Kwa kweli hapa hapatakuwa na usafi, kwa sababu kila mmoja anahofu na maisha pamoja na hali yake na afya ndio umuhimu wa mwanadamu. Sasa kama huyu mfanyakazi yuko dhalili hali kama hii na mji utakuwaje, mji utakuwa mchafu sana.

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, katika kumuidhinishia vifungu hivi kumpa uwezo, ili wafanyakazi wawe na mori ya kuifanya ile kazi. Kwa hivyo, wafanyakazi hawa awatunze, na wawe na hali nzuri na vitu hivi vipatikane, kwa sababu wale ni binadamu.

Kwa mfano, leo ukimkuta mama anayefyagia barabarani utamuonea huruma, anazoa taka kwa mikono yake na hata fagio na kibati cha kuzolea taka hana, kwa kweli hii itakuwa tunawadhalilisha wafanyakazi wa Manispaa.

Vile vile kuna suala zima la wafanyabiashara wadogo wadogo kama vile mamantilie. Mhe. Spika, maeneo wanayofanyia kazi mama lishe ni maeneo hatarishi, na Baraza la Manispaa wapo na wanakula pale, Mhe. Spika isijenyesha mvua na hili ni tatizo, kwa sababu pale ni kuhatarisha maradhi ya tumbo na kipindupindu na kila mamantilie analipa pale.

Sasa katika kulipa hawa watu bado wanatishwa, wengine wanaambiwa watoe shilingi 2,000/=, lakini kwenye risiti inaandikwa shilingi 1,000/= na hili tunalifanyia kazi kwani hatujapata uhakika.

Mhe. Spika, naomba kwenye hizi sheria hawa wananchi wetu wanaojiajiri kwa ajili ya kutafuta maisha, hivi kwa nini watoleshwe kodi, watoto wadogo kama hawa, na wataweza vipi kuja juu ukianza kuwaambia watoe kodi mamantilie, pengine yeye akiondoka pale amepata shilingi 5,000/= ya ziada na fedha hizo apate chakula na watoto, mafuta pamoja na vitu mbali mbali.

Lakini shilingi 2,000/= unazichukua wewe na amebakia na shilingi 3, atawezaje kudumu katika maisha yake, hivi atawezaje kuendesha huu mpango wake pamoja na kuweza kuwaajiri wengine, itakuwa tumemdhalilisha huyu mamantilie.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwamba watu wetu wanaojiendeleza kiuchumi tuwaondoshee ulipaji wa kodi, ili waweze kuja juu na waweze kuajiri wengine, na hapo ndipo tuanze kuchukua mapato. Kwa kweli hali tunayokwenda nayo basi siku zote wananchi wetu watabakia katika hali ngumu ya maisha.

Mhe. Spika, ndugu zetu wafanyabiashara wadogo wenye maduka na mambo mengine, pia watu hawa Manispaa wanawadhalilisha sana. Kwa mfano, mtu anaweza kwenda kufuatilia kwa ajili ya kupata ile leseni, lakini huu utaratibu wa kupata leseni utaumwa na kichwa, na atafika kuchukuliwa vitu vyake vyote na leseni anashindwa kukabidhiwa na Manispaa. Vile vile wanapokuja ikiwa huna leseni basi wanaanza kuchukua vitu vyako, na huo ndio mwanzo wako wote.

Mhe. Spika, hawa wanachangia nchi wakati ndio wanaotoa kodi ya nchi na wanafuata utaratibu, sasa na wale wanaokamilisha ule utaratibu basi wasiwe na vikwazo kuumaliza huu utaratibu wa kuwafanya wafanyabiashara wetu waweze kupata hizo leseni zao.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala zima la vitambulisho, ambalo tokea asubuhi linazungumziwa hapa. Mhe. Spika, suala la vitambulisho tukitaka tusitake sheria tumeshaipitisha, na tayari imeshaekewa adhabu zake. Kwa hivyo, kumnyima Mzanzibari Kitambulisho cha Ukaazi ni kumwambia wewe sasa nenda jela ukachezee mtondoo. Mhe. Spika, hakuna maana kwamba Mzanzibari kuekewa vikwazo ambavyo vinamsababishia kushindwa kupata kitambulisho.

Mhe. Spika, nadhani inaelekea kwamba wakati wa kutunga Sheria za Ukaazi, inaonekana kwamba tulielekea sana kwenye siasa kuliko kwenye jamii. Kwa hivyo, kama tulielekea huko, basi mimi naomba hapa tulipo tubadilike, kwa sababu suala la kitambulisho ni suala la lazima, na kila mwananchi awe nacho na wala kusiwe na sheria zinazokandamiza na kumfanya Mzanzibari akose kitambulisho.

Kwa mfano, mimi na Mhe. Mjumbe mwenzangu kuhusu suala alililoboresha Mhe. Rais, tulikwenda Benki Kuu pale Tawi la Zanzibar, na tulisema kwamba tusipeleke vitambulisho vyote tupeleke angalau kimoja tu.

Mhe. Spika, mimi sikupeleka kitambulisho changu, lakini mshughulikiaji wa ile *voucher* aliniambia nimpe kitambulisho, nilimwambia sina kitambulisho nimekisahau, aliniambia huwezi kupata fedha hapa, wakati nilipopeleka *check* ile, aliniambia huwezi kupata fedha mpaka uwe na kitambulisho.

Lakini alipoisoma ile *check* yangu anaiona imeandikwa Mheshimiwa, ndipo aliposema Mheshimiwa wewe itabidi ukamchukulie fedha zake Mheshimiwa huyu na baada ya kutia saini hapa. Mhe. Spika, sasa kama mimi hapa nisingekuwa Mheshimiwa ni mtu wa kawaida, basi haki yangu ile ningeikosa.

Kwa hivyo, kama tumeshafikia hapo Mzanzibari hapati kitambulisho hizi haki zake nyengine za maisha atazipata wapi, na hili ni tatizo Mhe. Spika kuweka sheria ambazo zinamkandamiza Mzanzibari akose kutambulisho, basi ni vyema kubadilika na kama tunayo malengo ya kubadilika.

Mhe. Spika, namuomba sana Mwanasheria Mkuu kufanya utafiti wao kwa ajili ya kuzibadilisha sheria hizi ambazo zinazowakandamiza wananchi, ili wananchi waweze kupata haki zao kama Katiba ya Zanzibar inavyotuelekeza. *(Makofi)*

Sasa niende kwenye Chuo cha Mafunzo. Mhe. Spika, katika sehemu hii kuna udhalilishaji kwa wafanyakazi wenyewe, na hawa ndugu zetu wanaokwenda kuchukua hayo mafunzo pamoja na mambo mbali mbali. Mhe. Spika, naomba uniruhusu nisome kifungu cha 12 (4) na (5) vya Katiba ya Zanzibar, Mhe. Spika naomba kunukuu.

Katiba ya Zanzibar kifungu cha 12(4) na (5) vinasema hivi:-

(4) “Hakuna mtu atakayebaguliwa na mtu yeyote

Anayefanya kazi chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi ya Afisi yoyote ya serikali au uongozi mwengine wa chama chochote na vyombo vyake."

Mhe. Spika, katika Chuo hiki cha Mafunzo kuna ubaguzi mkubwa, ukija katika ile ngazi kuu ya juu kuna viongozi wanafika karibuni thamanini lakini hapa wapemba ni sita tu kwa nini na Zanzibar ni moja. Hao sita mmoja tu ndio aliyekuwa na nyota nyingi katika hao, wawili wamebahatika wana nyota mbili, wane waliobakia mmoja kapewa nyota moja wawili hawana. Hii Mheshimiwa si haki hawa wote ni wananchi wa Zanzibar, hawa ni wafanyakazi wana haki kikatiba, kwa nini iende hivi huu Mhe. haujawa utawala bora.

Lakini pia ukija juzi tu karibuni wamewapeleka watu Mafunzo watu 20 hamna mpemba hata mmoja katika ishirini, tunakwenda wapi Mhe. Spika, kama tunabaguana hali kama hii angalau kwenye ishirini si angalau wanane lakini hata mmoja? Mhe. Spika, hali hii tunayoipeleka nchi ni ya ubaguzi wa Pemba na Unguja kasema Mhe. Saleh wa Kaskazini na Kusini hatimae yake tutafanya dhambi hii mpaka mtu watoto wake aliowazaa. Atampenda mmoja wengine hatowapenda au atampenda mwanawe mweusi mwekundu hatompenda dhambi mbaya tu ya ubaguzi.

Mhe. Spika, katika Wizara hii ubaguzi umekirithiri na yote yamechangia ni Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Kwa hivyo na mimi nasisitiza suala kama hili la ubaguzi ana haki ya kujiuzulu katika hali kama hii hatuwezi kubaguana tulipofika Mhe. Spika, kwa kweli hili ni tatizo. Mhe. Spika, ukija katika suala zima la mafunzo wananchi wetu wanaopata kukosea katika mambo mbali mbali wengine wanadhalilishwa tu, wengine wanasingizia mambo tu, wengine hawana uwezo wa kujitetea wakashindwa kushtakiwa na kufungwa mahkamani. Lakini hayo yaliyoko huko sitaki niseme sana Mhe. Saleh hapa ameeleza vya kutosha kabisa. Lakini katika haki za kibinaadamu kwa kweli magereza yetu bado yana matatizo. Mimi ningewaomba sana waheshimiwa tusidhanie kwamba leo wewe ni spika, au Waziri au Mwakilishi inawezekana japo siku moja akaja akafika huko inawezekana hiyo na kule tuweke mazingira mazuri wale ni binaadamu. Kwa hivyo hivi viti tunavyokaa kuna watu watakuja na watakuja na wengine, inawezekana mtu atafika huko kwa hivyo lazima tuweke maeneo na kujali haki za kibinaadamu, tubadilike Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa kumalizia tu niseme kwamba kama Mheshimiwa Waziri mambo ya vitambulisho atafanya mabadiliko, na sheria hizi kandamizi itafanyiwa mabadiliko, magereza kuendeshwa katika mlo mmoja wakapatiwa milo yote mitatu, kwa sababu juzi kulitolewa kichekesho kikubwa Mhe. Mhe. Mohammed aliuliza hili suala kuhusu wafungwa walioko kule Pemba kupewa mlo mmoja. Baada ya ule mlo mmoja nusu kilo wanaokuja juzi uligawanywa mara mbili, robo kilo wakala asubuhi, robo kilo wakapewa jioni tumefanya nini? Hilo ni tatizo Mhe. Spika, kwa bahati nzuri wakalalamika ndugu zetu hawa ikarudishwa vile vile mlo mmoja. Kwa hivyo bado tatizo Mhe. Spika, lipo lazima tuwajali ndugu zetu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, sitaki nipoteze muda wako sana inshaalla ninafiki hapo.

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Spika, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu makadirio , mapato na matumizi ya fedha ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2012, 2013.

Mhe. Spika, natoa pongezi za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniteua kuma mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Tatu ninakushukuru wewe mwenyewe Spika, kwa kunikaribisha katika Baraza lako hili tukufu na ninawashukuru waheshimiwa wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuniahidi kunipa mashirikiano na mimi naahidi kushirikiana ili kuleta maendeleo katika taifa letu.

Mhe. Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa hatua ambayo imechukuwa kwa ajili ya kujenga maofisi ya viongozi mbali mbali, na hasa ukizingatia katika mwaka huu wa fedha takriban Mikoa yote ya hapa Zanzibar malengo yao yote yanasema ujenzi wa ofisi za mikoa na wilaya. Kwa hiyo napenda kuishukuru serikali kwa jitihada hiyo.

Mchango wangu hasa ni kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini. Mhe. Spika, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini mpaka sasa hivi wanafanya kazi katika mazingira magumu, jambo ambalo linapunguza ufanisi wa kazi. Afisi ya Wilaya ya Mjini Mhe. Waziri wapo katika Hoteli ya Bwawani, mwanzo walikuwa wanafanyakazi katika Wizara ya Biashara ambapo jengo hilo hivi sasa linafanyiwa ukarabati. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri achukue jitihada za makusudi, ninaamini hilo jambo atakuwa analijua azungumze na Mhe. Waziri wa Biashara, ili kuona

kwamba hili jengo lilimalizika kufanyiwa ukarabati, warudishwe kwenye jengo hili waendelee na kazi zao ili kuboresha ufanisi katika kazi zao.

Jengine Mhe. Waziri napenda kuchangia kuhusu bajeti za Mikoa na Wilaya ambapo shughuli nyingi za maendeleo zinafanywa katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Na ukiangalia kuna kamati mbali mbali za mikoa na wilaya, kuna kamati za maendeleo za Wilaya, kamati za maendeleo za mikoa, RDC na DDC. Kamati hizi miongoni mwa wajumbe wa kamati hizo ni waheshimiw wabunge, waheshimiwa wa Baraza la Wawakilishi, waheshimiwa madiwani ambapo kisheria sheria za tawala za mikoa zinasema kila baada ya miezi mitatu zinakutana zinajadili mambo mbali mbali ya maendeleo ya Wilaya na Mikoa, lakini zimeshindwa kukutana kutokana na upungufu wa fedha ambazo zinatokana na kupatiwa wilaya hizo na mikoa.

Hivyo basi kuna mambo Mhe. Waziri achukuwe juhudi za makusudi angalau hizi kamati ziwe zinakutana waongezewe pesa katika OC ambazo zinakuwa ni kidogo sana ambazo zinashindwa hata kukutana katika vikao vyao mbali mbali vya kujadili maendeleo. Kwa hivyo Mhe. Waziri achukuwe juhudi za makusudi ili angalau OC ziongezwe, ili waweze kutengeneza mipango yao kwa ufanisi zaidi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza ninamshukuru Allah kwa kutupa uhai uzima na taufiki kuzungumza katika Baraza lako. Pili ninakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pia ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake marefu yaliyotolewa katika kitabu hiki.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka nianze na Idara Maalum. Mhe. Spika, Idara Maalum inachukua vikosi, mimi nilikuwa ninamuuliza tu Mhe. Waziri kwamba tuna vikosi viwili hivi kimoja kinaitwa JKU kimoja kinaitwa Valantia. Naomba katika maelezo yake aje anieleze tofauti ya malengo baina ya vikosi hivi viwili. Kwa sababu mimi katika bajeti nyingi zilizopita nilikuwa nikichangia kwamba si vibaya kuajiri ndugu zetu lakini kama malengo yao ni mamoja basi bora kuwachanga wakawa kitu kimoja kikajulikana.

Mhe. Spika, bajeti ni upangaji mzuri wa matumizi ya fedha zinazopatikana kutokana na vyanza mbali mbali. Sasa kama kuna sehemu ambayo tunaweza tukachanganya, administrative cost yaani gharama ya uendeshaji wa shughuli ile itapungua sana na fedha zile zitakwenda katika kuwahudumia wananchi. Sasa kadri tunavyokwenda hatuoni tofauti ya malengo baina ya JKU na Valantia zaidi ya jina.

Sasa mimi naomba serikali isiwe kakatavu katika maazimio yake inakuwa *very rigid*, Serikali nzuri katika utawala bora ambayo iko *flexible* ikiona hapa ni nguvu inaitwa sijui. Ikiona kweli hapa kuna njia *correct* ya kusahihisha inajifanyia masahihisho. Mimi katika bajeti ijayo tukijaaliwa nitakwenda kutafuta wataalam wanaifanyie hesabu katika administrative cost ya vikosi hivi viwili ambayo serikali ingeokoa kwa kuvichanganya pamoja. Lakini Mhe. Spika, katika utaratibu mzima wa uendeshaji wa serikali kuna mambo matatu makubwa.

Kwanza kuna sekta ya uzalishaji, hii ni tunaita *cluster* ya uzalishaji, lakini kuna claster ya huduma halafu kuna *cluster* ya ulinzi. Sasa kwa sababu Tanzania kuna jeshi la Tanzania, kuna jeshi la Polisi na kwa bahati nzuri Zanzibar kuna KMKM. Mimi nauliza hawa JKU na Valantia wana *role* gani katika *cluster* hizi ni wazalishaji, walinzi au ni watoa huduma? Kwa sababu lazima tujiambie hatuwezi kwenda kama gari la ng'ombe linakuelekezwa linakwenda, nchi lazima iwe na muelekeo. Hivyo ifike wakati lazima tujiulize je vikosi hivi vya JKU na Valantia viko katika *cluster* gani, ikiwa ni uzalishaji Mhe. Spika, hatuoni katika kitabu hiki wamezalisha kiasi gani na kuipatia manufaa nchi yetu. Ikiwa wao ni watoa huduma hatuambiwi wanatoa huduma gani, na ikiwa wao ni walinzi basi je wanalindwa mwaka mzima kulingana na mishahara yao wanaopewa. Mimi Mhe. Spika, sina ugomvi na mtu lakini tunakwenda katika ulimwengu wa kisasa ambao kila kitu kinahesabiwa.

Halafu Mhe. Spika, hoja ambayo niliijenga tokea mwaka jana na miaka mengine iliyopita bado Mhe. Waziri yuko *very rigid* hajanyumbuka kwamba bajeti ya vikosi hivi viwili kimoja kimja ukichukua JKU kimoja, ukichukua valantia kimoja inaipita kikosi cha Zimamoto bajeti yake na majukumu ya Zimamoto na Uokoaji ni kikosi ambacho kina majukumu makubwa. Sasa Mhe. Waziri anaendelea na bajeti ndogo hii kuipa Zimamoto na ndio maana mioto mingi inayotokea haizimwi kwa sababu yeye mwenyewe Mhe. Waziri ndie anayesababisha. Kwa sababu Zimamoto ina majukumu makubwa na sisi tunakaribisha vitega uchumi, tuna mahoteli, tuna viwanda tuna mahospitali yetu,

tuna majumba yetu, sasa Zimamoto unawapa 1.88 kwa mwaka jana, mwaka huu ni 3.09. Wakati JKU wapewa 7.9 milioni mwaka huu na hawa wamepewa 3.78 Valantia. Sasa huku JKU na Valantia kuna nini hata ikawa hawa Zimamoto ambao ni *very pontential* katika kazi yao ikawa hawapewi bajeti ya kutosha.

Halafu Mhe. Spika, matumizi ya serikali yanakuwa katika maeneo mawili, kuna matumizi ya kawaida na kuna matumizi ya maendeleo, lakini kwa kweli bajeti ya Mhe. Waziri inakanganya kabisa maelezo yake. Alisema kikosi kimenunua gari mbili za kisasa za kuzimia moto lakini bajeti yake haipo. Katika bajeti ya mwaka jana iliombwa bajeti ya kawaida tu hakuna bajeti ya maendeleo kwa hivyo hizi gari mbili zitanunuliwa kwa bajeti gani.

Mhe. Spika, kuhusu Chuo cha Mafunzo nilie mkazo tu kama walivyosema kama yale waliozungumza wenzangu kwamba hali bado inatakiwa iangaliwe ili tuendane na wakati, mazingira ambayo tunawenda nayo katika vyuo vya mafunzo yaweze kufanyiwa ukarabati mkubwa na kuangaliwa ili hali iweze kutengenea zaidi, wenzangu wameshaeleza zaidi sina haja ya kueleza.

Lakini mimi ninarudia ombi langu ambalo ninalitoa kila mwaka kwamba Mheshimiwa Abeid Amani Karume alipoanzisha Chuo cha Mafunzo alifanya vile kwa ajili itolewe elimu kule, wale wanaotoka waweze kupata taaluma fulani na tukumbuke kwamba wakati huo Zanzibar ilikuwa mwisho form six hakuna Chuo wala Chuo Kikuu. Lakini katika karne yetu hii tuliyonayo Mhe. Spika, Zanzibar ina Vyuo vingi, ina vyuo vikuu vitatu bado tunaendelea kupita chuo cha mafunzo na watu wake ni wanafunzi. Sasa huenda ikawa ndio wanafunzi wetu wakafeli maana yake wanaokosa ni wanafunzi na waliofungwa ni wanafunzi, Jumuiya ya Afrika Mashariki tuliyoungana ina vigezo vyake, sisi tunaelekea katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa nini tuko *rigid?* Kukibadilisha tu tukakiita vile vile magereza wakati katika sheria za kingereza kinaandikwa hivyo, tuna *confuse* wanafunzi wamefanya hivi, wanafunzi wafanye hivi.

Mhe. Spika, haifahamiki, tunajizonga ikiwa pauro liite pauro basi, kutokana na mambo tele ambayo yako ni ushahidi umefika wakati sasa magereza tuyaite vile vile magereza. Tuseme huko nje katika umoja wa Mataifa kutokana na haya mambo yaliyoingia ya haki za kibinaadam tukaomba sisi msaada wa kutengenezewa haya majela yetu. Lakini wakasema sisi tuna Chuo cha Mafunzo, wao wakasema sisi hatutoi misaada vyuo vya mafunzo tunatoa kwenye majela.

Sasa tutaupata vipi msaada huo. Hili naomba litizame tena, je hili ni jina sahihi kwa nini Hospitali ya Mazi Mmoja ilikuwa ikiitwa V.I. Lenini ikaweza kubadilishwa nayo ilikuwa ndiyo hivyo hivyo, kwa nini tusiweze kubadilisha hiki Chuo cha Mafunzo tumekita jela ili tulingane na kile kinachotokea kule.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye Idara ya Vitambulisho. Mwaka jana waliandika kuwa wana lengo la elfu kumi na kidogo na mwaka huu vile vile lengo lao ni kutayarisha vitambulisho elfu kumi na mia tatu. Sasa mimi nauliza huu ndio uwezo wao. Kila mwaka kutayarisha elfu kumi, lakini pia je, *population* yetu ina *mature* elfu kumi kila mwaka yaani kila mwaka tunaingia miaka 18 wanaingia miaka 18 ni elfu kumi, hii elfu kumi ina *formula* gani, wametumia vigezo gani vya takwimu mpaka wakapata elfu kumi. Kwa sababu kama *population* yetu inabadilika kwa elfu kumi halafu wao wakasema wanatayarisha vitambulisho elfu kumi tungejua kwamba wanakwenda sambamba na kukua kwa hii population yetu, kwamba kiila mwaka vijana elfuu kumi wanatimia miaka 18.

Mhe. Spika, sura ya tatu ya Katiba ya Zanzibar inaeleza kwa mwenye kujua na kutaka haki za watu mtu mmoja binafsi, kinga ya haki ya lazima, wajibu na uhuru wa mtu binafsi. Vifungu vingi vilivyokuwemo katika hii sura ya tatu, leo itakuwaje watu ambao wanataka kuajiriwa kinatakiwa kitambulisho, watu wanaotaka paspoti kinatakiwa kitambulisho, kuchukua fedha benki kunatakiwa kitambulisho, kurithi, kinatakiwa kitambulisho. Kwenda kuchukua leseni ya gari kinatakiwa kitambulisho cha Mzanzibari, halafu tunawanyima.

Mimi nawashauri hasa wale waliokuwa tayari kuishtaki serikali basi mimi nitachangia katika mfuko wa kuishtaki. Kwa sababu tunawatesa wale vijana ambao wengi wameshatimia umri, tungeleta sera hii ya kuwa na vitambulisho, mabenki yote yunajua kila pahala panajua kwamba hapa panavitambulisho, lakini wengi wao wananyimwa. Juzi nilisema hapa kwamba kile kisingizio kwamba watu hawendi kuchukua basi wasende kuchukua hichi kitambulisho tu vitu vyengine vyote wanavyowekewa wachukue. Hapa kuna ajenda ambayo tunaomba sana sana ifanyiwe kazi. Bila ya hivyo itakuwa tunavunjia haki vijana wetu au watu wetu waliokosa vitambulisho.

Sisi tunaushahidi kamili ndio maana tukawa wawakilishi, hatusemi tu kwa maneno. Watu wetu wengi hawana vitambulisho na ikiwa Mhe. Waziri unawataka basi mimi nitapika chai nikualike. Si kweli kwamba vijana wanapata vitambulisho juzi hapa Mhe. Spika, nilimuuliza Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Wenzetu Tume ile ya Vitambulisho vya Jamuhuri ya Muungano wameweka program ya kupitia maskuli kutayarisha vitambulisho kwa wanafunzi. Sisi tunautaratibu gani? Au utaendelezwa, utapangwa, tunakigugumizi gani. Hawa vijana wetu wanaosoma maskuli si wakaaazi hawa, basi wawekeni hewani kama si wakaazi. Maana yake hatumwamini mtu mpaka aende yule mwanafunzi tunaemsomesha.

Mhe. Spika, suala la vitambulisho lazima Mhe. Waziri aje atoe jibu lililo na muelekeo, atupe hasa tarehe kwamba sasa waliokuwa hawana vitambulisho ikifika tarehe fulani wote watapata. Halafu atakuja kusema humu humu kwamba hatukupata lakini maneno mengine yoyote hatusikii tutajua kwamba kuna ajenda inayozungumzwa iliyojificha ambayo haileti maslahi kwa Zanzibar wala Wazanzibari. Hili ni lazima tuliseme.
Huu ni mwaka wa tano au wa sita tunapiga kelele kuhusu vitambulisho ni kitu gani, kazi kuandika katika kitambu kwamba tunasifiwa na ulimwengu kwamba tunatoa vitambulisho vilivyokuwa vizuri duniani. Hawa wengine hawapati haya sifa hiyo ina maana gani. Ikiwa wengine hawapati kuna msemo unasema, usingoje kusifiwa nje sifiwa humu ndani kwanza. Lakini hatuwafahamu, mimi mwenyewe siwafahamu kwamba nyinyi mnatafuta sifa nje ndani hamna lolote, sifa hiyo itakusaidia nini. Hawa usasifiwa nje, nenda basi ukawe raia huko. Si tunasifiwa nje.

Mhe. Spika, nakuja suala la mwisho kwamba hapa tulipitisha Sheria hapa inaitwa *Public Service Act* ambayo iliundiwa Wizara nzima, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tukawakabishi kazi zote lakini inastaajabisha kuwa Mhe. Waziri kitengo hakukitoa GSO kimebakishwa kule kufanya nini. Sekta yote ya Utumishi wa Umma iliundiwa Wizara nzima. Hii GSO madhumuni yake yote yapo katika Idara ya Utumishi na Utawala Bora, ilibakishwa kule kufunya nini. Mhe. Waziri aje atujibu.

Wakati juzi alipokuwa akijibu suala la nyongeza langu mimi nilimuuliza ni changamoto gani ambazo umezipata kutokana na ziara za Mhe. Rais akasema Wizara yangu ni kubwa. Pasi ipinguze hapo ikiwa kweli Wizara ni kubwa ipunguze hapo. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili angalau na mimi nichangie mawili matatu yanayohusiana na Wizara hii muhimu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, Baraza letu sasa limo katika mageuzi, mageuzi ya kuelekea kwenye utendaji bora na utendaji unaowatumikia wananchi. Kwa sababu Baraza letu hili ndio ngome ya wananchi na ndio kimbilio la wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, Baraza letu limo katika mageuzi na nikupongeze Mhe. Spika, kwa namna unavyojitahidi kutuwezesha Waheshimiwa Wajumbe katika kupata uelewa namna ya kufanya kazi zetu kama wawakilishi wa wananchi. Katika hali hiyo basi, wataalamu ambao mara kwa mara kupitia ufadhili wa *UNDP* wamekuwa wakitufunza ni namna ya kufanya kazi vizuri ya kuisimamia serikali kwa mujibu wa Ibara ya tano ya katiba yetu.

Suala zima la kupitisha katiba mafunzo yetu yanatuelekeza kwamba kama wawakilishi wa wananchi tusikubali kwa sababu sisi ndio wenye idhini, tusikubali kuidhinisha fedha za walipa kodi ambazo hazitokuwa na tija ya moja kwa moja kwa wananchi wa Zanzibar ambao ndio walipa kodi. Lakini mafunzo yetu kadhalika yanatueleza kwamba, fedha tutakazoziidhinisha katika bajeti hii ni lazima ziangalie thamani halisi ya fedha, tuangalie *value for money*, fedha zilizokuwa hazitoangalia *value for money* mafunzo yametukataza kwamba tusiidhinishe, kwani kwa kufanya hivyo ni kuwasaliti wananchi wa Zanzibar ambao ndio wavuja jasho wa nchi hii.

Kwa utangulizi huo Mhe. Spika, naomba nianze sasa kwenye mfumo wa serikali. Serikali yetu ina mfumo kwanza wa kuwa na Serikali Kuu na baadae kuwa na Serikali za Mitaa. Wataalamu wanatwambia kwamba maendeleo ya nchi yoyote Serikali za Mitaa huwa zina umuhimu mkubwa, ili maendeleo ya wananchi yafikiwe ni lazima na ni muhimu tuwe na Serikali za Mitaa zilizokuwa ni adilifu, fumbuzi na ambazo zina watu wenye uwezo mkubwa. Niipongeze serikali kwa kuiona dhana hii na kwa kuchukua hatua ya kuanzisha mchakato huu wa mageuzi ya Serikali za Mitaa. Lengo ni kufikia katika hatua ambayo tutakuwa na Serikali za Mitaa ambazo ziko makini na zenye kuwaletea maendeleo wananchi wetu kupitia Waheshimiwa Madiwani.

Lakini katika hili Mhe. Spika, mimi binafsi napata wasiwasi mkubwa kwamba zoezi hili la mchakato wa mageuzi ya Serikali za Mitaa limekuwa sasa limechukua muda mrefu sana, tangu tuanze kusikia suala hilo katika masikio yetu

huu haupungui ni mwaka wa kumi, inasikitisha, inashangaza kuona kwamba kwa nini zoezi hili likachukua muda mrefu na baya zaidi kwa nini wawakilishi hatuelezwi namna ambayo kwa sababu, kwa kuwa zoezi hili lishachukua muda mrefu kwa vyovyote vile tulitaka sasa lifikie mwisho ili tuangalie mambo mengine, fedha hizi tunazoziidhinisha katika hili ziingie katika masuala mengine ya maendeleo ya wananchi.

Mhe. Spika, mwaka 2010/2011 bajeti yake tulitenga, Baraza hili liliidhinisha shilingi 250 milioni, mwaka jana tuliidhinisha shilingi 150 milioni na mwaka huu tumetakiwa tuidhinishe shilingi 150 milioni. Mimi nikiwa kama Mwakilishi wa wananchi siko tayari kuidhinisha fedha aina hii, hatuwezi kuidhinisha kiwango hiki cha fedha, fedha ambazo hatujui zinafanyiwa nini; lazima sasa tufike wakati tuambiwe kwamba suala hili limefikia katika hatua hii na limebakia hatua hii na tutatakiwa tufanye nini ili tukamilishe. Hatutaki tena kama wawakilishi kusikia suala la mchakato uliokuwa hauna mwisho.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, kama ikiwa ni sera naomba niseme kwamba naondosha shilingi katika kifungu hiki kwamba sitokuwa tayari kupitisha shilingi 150 milioni kwa kuziingiza kwenye mchakato wa mageuzi ya Serikali za Mitaa, mchakato ambao hatuujui mwanzo wala mwisho. Kwa hilo nakomea hapo.

Lakini vile vile Mhe. Spika, katika suala hili la mageuzi ya Serikali za Mitaa, mbali ya mchakato tunaouzungumzia lakini kwa kuwa sasa hivi mfumo unao-*exist* ni mabaraza haya tuliyonayo. Lakini katika hili Mabaraza yetu pamoja na halmashauri Mhe. Spika, yanakoseshwa mapato makubwa na Masheha.

Kamati yangu ilifanya ziara ya kutembelea Mabaraza pamoja na Halmashauri manung'uniko makubwa ni kwamba Mabaraza na Halmashauri mapato yake yameshuka kwa sababu sehemu kubwa au baadhi ya sehemu ya mapato ya vyombo hivyo yanachukuliwa na masheha, sasa ikiwa masheha wanachukua baadhi ya mapato naomba Mhe. Spika, kupitia Baraza lako niambiwe kwa sababu sisi ndio tunaoidhinisha, vyanzo vyote vya mapato tunaidhinisha sisi. Serikali itakavyokusanya na vyombo vyake vya kukusanya sisi ndio tunaoidhinisha. Kwa hivyo, naomba niambiwe kwamba ni sheria gani iliyowapa mamlaka Masheha kukusanya mapato.

Lakini vile vile katika hili naomba nielezwe Mhe. Waziri atakapokuja mapato haya ya masheha yanaingia katika kifungu gani cha hesabu za serikali. Naomba niondoke katika hilo sasa niende kwenye Wakuu wa Mikoa.

Mhe. Spika, ni shahidi kwamba mara nyingi tunapozungumzia tunazungumzia na Rais naye anazungumzia, kumekuwa na mijadala ambayo hata juzi Mwanasheria Mkuu alitutolea ufafanuzi juu ya hatma ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Sisi tunachozungumza kwamba hawa watu kwa sababu serikali ni mpya wanapaswa kwa kweli wateuliwe japo ni wale wale wathibitishwe ili waweze kutumika vyema. Sasa hivi wasiwasi nilionao kwamba kwa sababu kuna haya maneno ya hapa na pale yanayokwenda baina ya Baraza, Wananchi, Serikali, hata utendaji wao sasa hivi umeshuka. Sasa naomba tu, vyovyote ilivyo na kadiri tunavyozungumza hivyo tunataka kujua ikiwa ni suala la kwamba wanaondoka weshamaliza kipindi chao hatima ya posho zao ni zipi. Kwa sababu wote watendaji wanapoondoka pale huwa kuna kitu mkono wa kwaheri.

Niliwahi kusikia kwamba tayari watu hawa washapewa mkono wao wa kwaheri, naomba Mhe. Waziri atakapokuja anithibitishie kwamba je, Wakuu wa Mikoa na Wilaya tayari wameshapewa mkono wao wa kwaheri au bao? Na kama bado ni kwa nini. Naomba niishie hapo.

Suala jengine la mwisho katika Serikali za Mitaa naomba nizungumzie suala la Baraza la Mji la Chake Chake na katika hili sitaki kwenda mbali sana kwa sababu na huu mchakato unanizuia kuzungumza kwa umbali sana. Kwa sababu kila nikikaa naambiwa kuna mchakato nasubiri mchakato uive hauivi, lakini bado nazungumzia kwamba kuna umuhimu wa suala hili kupatiwa ufumbuzi wa haraka na katika Baraza la Mji la Chake Chake kuna tatizo wananchi wa Chake Chake na Wapemba kwa ujumla, kwa sababu Chake Chake sasa hivi ndio *centre* ya biashara ya Pemba. Kero kubwa tulionayo sasa hivi ni njia inayotoka *Barclays* mpaka Hospitali na kuingia njia ya Miembeni, haina tofauti hata kidogo na bao la soo. Limekuwa ni kero na ndio sehemu kubwa ya Baraza linapopatia mapato yake kupitia wafanyabiashara.

Kwa kuwa hapa nilimsikia Naibu Waziri akizungumza kwamba njia hizi ni mali ya Mabaraza ya Miji na Halmashauri, wao kama Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kazi yao ni barabara kuu, sasa kwa sababu hiyo ndio mamlaka yao na ingawa nawajua watanambia uwezo wao ni mdogo, lakini nataka nijue wana mpango gani Baraza la Mji angalau kututilia fusi au angalau kushirikiana na Mwakilishi na Mbunge, kushirikiana na Wizara ya

Miundombinu katika kuona kwamba zile fedha zinazokusanywa mbili mbili mule madukani na masokoni basi zinakuwa zina thamani halisi za fedha zinazotozwa kwa wananchi. Kwa suala la Serikali za Mitaa naomba niishie hapo.

Sasa nataka niingie katika suala la Ikulu. Mhe. Spika, kwa muda mrefu katika Baraza hili vile vile tumekuwa tukiidhinisha fedha nyingi sana, bahati nzuri Ofisi ya Rais Ikulu upelekwaji wake wa fedha huwa ni kwa asilimia takriban zinacheza kwenye asilimia 100, 90 haipungui hapo. Na kwa muda mrefu kumekuwa na hii miradi iliyokuwa haimaliziki, ukarabati wa majengo ya Ikulu umekuwa ndio hadithi ya kila siku katika Baraza hili.

Mwaka 2010/2011 Baraza hili liliidhinisha shilingi 1,450,000,000/- kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Ikulu. Mwaka 2011/12 tuliidhinisha shilingi 300 milioni na mara hii hadithi inakuja ile ile tuidhinishe fedha kwa ajili ya Ikulu.

Mhe. Spika, mimi nasema kwa nini fedha zote hizi tunazoziidhinisha kwa ukarabati zisitumike kwa ajili ya kujengea kasri moja kubwa. Maana yake tunamhitaji Rais wetu aishi katika kasri, heshima ya wananchi ni Rais na Rais lazima aishi pahala pazuri, lakini kutumia kiwango hiki kikubwa cha fedha kwa ajili ya kukarabati majengo mabovu mimi nadhani ni kuuwa fedha za wananchi.

Mhe. Spika, nataka niwaambie hiyo Ikulu anayokaa Rais tulikwenda katika wizara tukakubaliana na tukaagiza kabisa, kwamba jengo analokaa Rais si nyumba ya serikali, nyumba ya serikali ni nyumba ambayo ina hati, jengo la Ikulu halina hati. Kwa hivyo, tunakarabati majengo ya watu. Katika ulimwengu huu wa watu kudai mali zao kwa sababu hatuna hati kama ni jengo la Ikulu Mhe. Spika, ni aibu na hatuwezi kutumia tena fedha kwa ajili ya kukarabati, kesho na keshokutwa tukija tukisikia Rais katolewa virago vyake nje inakuwaje, ni nyumba ya watu ati. Kwa hivyo, ushauri wangu kwa nini sasa serikali isijielekeze katika kujenga nyumba ambayo itaitwa ndio *State House*, Kasri ya Wananchi wa Zanzibar.
Mhe. Spika, pamoja na hayo lakini vile vile matumizi haya tunayoidhinisha hayafuati sheria za matumizi, ni aibu kuwa ofisi kubwa kama ile kuambiwa fedha zinatumiwa hazifuati sheria za matumizi na unaposema ikiwa fedha hazifuati sheria tuliyojitungia sisi wenyewe maana yake huo ni wizi, huo ni ubadhirifu. Kwa msingi huo tunataka maelezo kwa nini Baraza hili liidhinishe fedha ambazo hazifuati utaratibu. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja aje ajenge hoja kwa nini tumpe fedha ende akazivuruge, kwa sababu pesa iliyokuwa haifuati utaratibu maana yake ni kuvuruga hiyo ndio tafsiri sahihi. Kwa hivyo, Baraza hili hatuwezi tukaidhinisha fedha ambazo huwa hazifuati utaratibu au Mhe. Waziri atapokuja aje atueleze vizuri namna ambavyo kuwa ili tuwe na imani na tumuidhinishie fedha hizi ukiachia mbali hizi za nyuma ambazo zishavurugwa.

Lakini nataka niseme hapa. Mhe. Spika, kamati yako ya *PAC* tulitaka kuyaona hayo majengo ambayo yalifanyiwa ukarabati, jawabu lake tuliambiwa maana yake mkienda kule Rais kalala mtamkera, tukawaambia jamani kamati yangu hii haihitaji kwenda vyumbani yale majengo ni ya wananchi, angalau tupite huku tu, tujiridhishe kwamba hicho kibanda tulichoambiwa kimejengwa kilijengwa kweli, tukiambiwa paa limewekwa je limewekwa kweli. Lakini nataka niseme kwamba na naomba nilalamike mbele yako kuwa hadi wakati huu kwa kweli kamati imeshindwa kwenda kuona hayo majengo ambayo tumeyaidhinishia pesa.

Kwa hivyo, ikiwa kamati imeshindwa kwa wakati huu mimi sasa hivi sishawishiki tena tutoe fedha zaidi, labda anambie tukitoka hapa saa saba twende Rais hayuko, twende hatuingii ndani sisi tutapita huku nje nje tu, hatuna haja ya kuingia ndani. Lakini lazima fedha tunazozitoa tujiridhishe na hapo Mhe. Spika, bado naendelea kusema kwamba fedha hizi hazifuati utaratibu kitu ambacho ni hatari na ni aibu kubwa sana katika mambo haya.

Lakini kwa miaka ya nyumba ambapo mara hii sikuona kuna ujenzi ule wa majengo ya Ikulu Bwefum, huku nyuma bajeti mbili tatu Bwefum, Bwefum, tulitegemea mara hii Bwefum iingizwe ili tuone kwamba majengo yale yamekamilika, kazi tulioifanya nzuri tuone kwamba imefikia pahala, hadithi hii sikuiona mara hii je, majengo yale ya kina Bwefum na kwengineko yamefikia pahala. Lakini ikiwa hayakufikia pahala maana yake ni kusema kwamba tumefanya kitu tumekiacha njiani ni kusema kuwa fedha zote tulizozitumia kwa ajili ya majengo yale ni kwamba fedha zile zimepotea, badala ya kuzichukua fedha zile tukazielekeza kwenye madawa Hospitali, vikalio katika skuli na huduma nyengine leo tunapoteza fedha namna hii. Kwa hivyo, Mhe. Spika kwa hilo naomba niishie hapo.

Mwisho naomba niingie katika Idara Maalum. Naomba niungane na wenzangu kwamba katika dunia ya sasa kunakuwa na kazi mbili kubwa kazi ya huduma na kazi ya uzalishaji. Vikosi vyetu hivi hata wale Wanajeshi wa

Jamhuri ya Muungano kama kuna kipindi tuliwahi kusikia Mzee Rashid kuna kipindi aliwaambia Wanajeshi sasa wacheze ngoma, maana yake wapo wanatumia fedha nyingi na hakuna uzalishaji wa aina yoyote sasa hivi Wanajeshi wacheze ngoma. Sasa tukafika pahala tukasema sawa, Wanajeshi waingie katika *operational function* zile ili pakitokea majanga, maana yake nini, maana yake tunataka tujue kwamba vikosi hivi vinachukua fedha nyingi sana za walipa kodi. Kwa hivyo, ama serikali sasa ifike pahala ibadilishe sera ili kila kikosi kieleweke kazi zake, hatuwezi kuwa na vitu ambavyo kazi zake hatuzielewi. Zimamoto kazi yake tunaijua ni kuzima moto na uokozi, kuna hawa KMKM kazi yake ni ulinzi na mambo ya magendo na vitu vingine, lakini hawa wengine nao Mhe. Spika, tunataka tuwaje ama ni wazalishaji ama watoaji wa huduma.

Lakini vile vile miradi ya vikosi nayo haifuati sheria, matumizi ya miradi inayoidhinishwa katika vikosi Mhe. Spika, haifuati sheria. Hata katika mafunzo yetu ya jana tuliambiwa kwamba tusiidhinishe matumizi ambayo hayafuati sheria, kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwa nini katika vikosi vyake sheria ya manunuzi haifuatwi. Unaposema sheria ya manunuzi haifuatwi maana yake huo ni ufujaji wa fedha za umma.

La mwisho naomba niseme kwamba Idara ya Vitambulisho Mhe. Spika, kwa muda mrefu tumekuwa tukizungumzia vitambulisho. Wawakilishi wako wanalia kuhusu vitambulisho, serikali inakuja na majibu tofauti kuhusiana na vitambulisho. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu hii hadithi ifike mwisho. Kwa sababu kadiri ninavyojua Mhe. Waziri atakuja hapa atatwambia hivi na hivi kitu ambacho malalamiko yataisha, mimi naomba nilitumie jukwaa hili niseme tu kwamba, kwa kadhia hii ambayo inawaathiri wananchi wetu kadhia ambayo haina majawabu kutoka serikalini wananchi wanaendelea kutesema.

Mhe. Spika, sasa hivi kitambulisho ni kila kitu katika maisha ya mwananchi, si suala la kupiga kura tu ni kila kitu kinachohusiana na maisha ya mwananchi. Kwa hivyo, kwa mamlaka ya Baraza lako Mhe. Spika, nitatoa hoja sio leo lakini nitatoa hoja kwamba Baraza lako sasa liunde kamati, kwa sababu tushazowea kila kitu sasa kiundiwe kamati, kila kitu kiundiwe kamati teule kwa nini sisi hatuwezi tukafika pahala tu serikali ikaja na majawabu tukashauriana tukafika pahala tukaondoka, huu ukaidi wa kuwa sisi tunasema hivi, wewe unasema hivi, wawakilishi wanasema hivi, waziri anasema hivi.

Sasa mimi nitatumia kanuni kuliomba Baraza hili ili tuondoshe tatizo hili linalowakumba wananchi wetu tuunde kamati ili baadae twende tukalichunguze suala hili, ukweli, mbivu na mbichi tuijue katika suala hili. Hili suala la vitambulisho na kadhia hii ya wananchi iwe ndio mwisho hatutaki kusikia tena. Kuna mambo mengi ya kufanya wawakilishi, serikali ina mambo mengi hatuna haja ya kulumbana kila siku katika suala ambalo wawakilishi limo ndani ya uwezo wetu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)* aliyenijalia kuwa na hali ya uzima na afya nikasimama mbele ya Baraza lako tukufu kujadili mambo yetu ya nchi. Pia nikupongeze na wewe uliyenipa fursa hii. Nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha. Sasa moja kwa moja niende katika mjadala.

Mhe. Spika, kwanza mimi nakwenda katika Baraza la Manispaa. Baraza la Manispaa katika miji ni kitengo ambacho kinastahili kuuweka mji safi na mambo mengineyo. Lakini nataka niseme tu, kwamba katika mji wetu wa Zanzibar sehemu ya Darajani ndio kioo cha mji wa Zanzibar, mgeni yoyote au hata wenyeji kama hawajafika Darajani bado hawajafika mjini. Mhe. Spika, ukiangalia dampo lilivyo pale Darajani sehemu ya maegesho ya magari linatia unyonge mji wetu.

Mhe. Spika, pale lilipowekwa dampo hapapendezi katika mji ni afadhali Mhe. Waziri na Baraza la Manispaa kutafuta sehemu nyengine wakaweka dampo lile. Kwa sababu ikinyesha mvua hakukaliki na ndio mji wetu nasi tumesema dhana ya utalii kwa wote na wageni wetu wanatembea sehemu zote zile. Pale pana mkahawa, *Marikiti Cafe* wageni wanafika lakini mimi mwenyewe binafsi nilifika siku moja hakuliki chakula kwa uvundo unaonuka kutokana na dampo lile pale. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunaliomba Baraza la Manispaa kufikiria upya kuweka dampo pale.

Vile vile Manispaa kuna watu wanaopanga samaki sehemu hizo za Darajani kutafuta riziki, sawa sio sehemu ya soko la kuuzia samaki, lakini wanavyowafurusha na kuwakamata wale samaki wao basi huwatoza pesa hawawapeleki kwenye vyombo vya sheria kama vile utaratibu unavyotaka wa sheria, mtu anatozwa kama shilingi 20 elfu anatia mfukoni kazi imemaliza. Ni lazima tubadilike tusifanye kazi kwa unyang'anyi kabisa, kwa nini kama ana kosa humpeleki kwenye vyombo vya sheria, lakini akifika pale anachukua pesa anatia mfukoni basi kazi imemalizika samaki wake anamrudishia au wakati mwengine asimrudishie lakini amuachie. Hili sijambo jema.

Mhe. Spika, katika Baraza hili la Manispaa nenda Soko la Malindi kaangalie uchafu uliokisiri kule, uchafu umekithirikabisa. Pale pana samaki wanauzwa kwa mnada na rejareja, walaji angalieni sana kukinyesha mvua funza linatoka kabisa na sisi tumetangaza dhana ya utalii kwa wote na hao watalii wetu wanapita kutembelea masoko kama hayo, wakiona hali kama ile tunapata sifa mbaya kwa wenzetu.

Mhe. Spika, haipendezi samaki kuwauza chini kule kuna vimelea mbali mbali vinawaharibu samaki wale lakini utakuta wanawekwa chini, mnada unafanyika chini na uchafu umekithiri. Maji ya karo yanapita sehemu hizo hizo basi jambo hili si jema kabisa samaki ni chakula na chakula ni afya. Kwa hivyo Mhe. Spika, tunaomba Mhe. Waziri na Baraza la Manispaa kuangalia vizuri.

Wenzetu wa Dar es Salaam katika Soko la Samaki lilioko Feri wametengeneza meza nzuri tu kwa kunadia samaki, baadae kuna sehemu wameweka kwenda kuwatengeneza kwa matayarisho, lakini sisi unakwenda pale Malindi labda watu kama sisi ndio tunakula samaki, lakini kama mtu mgeni akiona hali kama ile hanunui kabisa ni hali mbaya sana. Hilo moja.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika Ofisi ya Usajili na Kadi ya Utambulisho katika ukurasa wa 34(a). Mhe. Spika, mmezungumzwa humu lakini mimi napata mashaka sana kuhusu kadi hizi za utambulisho wa Uzanzibari. Ukiangalia kadi hii mbele na nyuma kitambulisho cha Mzanzibari, mbele na nyuma lakini kuna kitu Mzanzibari Mkaazi hili ndilo lililowakwaza watu wakawa hawapewi vitambulisho, huu ukaazi. Lakini ukiangalia kitambulisho chenyewe hakina maana ya kutiliwa Mzanzibari Mkaazi kimeandikwa Kitambulisho cha Mzanzibari, hapa pana kitu kimejificha tunaomba kitu hiki kifike mwisho au serikali inaogopa kitu gani hapa, mimi sioni kitu cha kuogopa. Tumeamua wenyewe kwamba kila Mzanziabari apate kitambulisho ni haki yake ya msingi, kila mtu awe na kitambulisho.

Wamesema wenzangu hapa kila unachotaka lazima uwe na kitambulisho hiki, ukienda Benki uwe na kitambulisho, ukitaka ajira uwe na kitambulisho, ukitaka kumchukulia mtu dhamana uwe na kitambulisho, kila unachokifanya ni kitambulisho hapa kwa nini Mzanzibari akose.

Jambo jengine unaambiwa mtu mwenye mamlaka ya kukihitaji kitambulisho hiki basi utoe umuoneshe na kwa jambo moja tu kujua huyu aliyekitoa kitambulisho hiki ni Mzanzibari? Kuna herufi ndogo za maandishi hizi zisomeni sana jamani kitakupeni maelezo. Anasema ukimuonesha yule mtu athibitishe kama ni Mzanzibari? Mhe. Spika, imefika wakati kwa kila mwananchi kupata kitambulisho hiki, inatia uchungu na inatufedhehesha kabisa, kwa nini niseme hivyo?

Kwa sababu ukizingatia vijijini wengi wao hawana vyeti vya kuzaliwa lakini ni Wazanzibari na wapo muda mrefu kule vijijini. Mtu tu, mwanawe anaugua mama na baba wameondoka wamekwenda kumuangalia mtoto wao aliyeko Dar es Salaam mwaka 2000 na 2005 walikuwa wanapiga kura, lakini hii 2010 hawakuwa wapiga kura ati hana cheti cha kuzaliwa mwenye umri wa miaka 50, 60 hao wapo na dagoni hawendi wapo pale pale ni wakulima. Mhe. Spika, tunawakosesha watu haki zao za msingi kwa jambo lililojificha. Sasa tuiombe serikali Mhe. Waziri akija hapa atueleze kuhusu jambo hili.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa kule kuna Masheha hawa ni marais wa ile sehemu zao husika. Hawa ndio muhimili mkubwa wa mahitaji ya sehemu za shughuli za maendeleo ya wananchi lakini wamejifanya waungu watu hawa, kila wanachosema wao ndio *ok*, mtu ata alalamike vipi mwananchi hana haki ni tatizo tunakoelekea. Nchi yetu ni tulivu, tuna serikali ya Umoja wa Kitaifa, tunafahamiana hatutaki turudishwe tulikotoka, mwananchi usimpoteze matumaini yake.

Mhe. Spika, kwa kulisema hilo basi hao masheha kama wamechoka kuteuliwa basi ni afadhali tuchague Serikali za Mitaa kama wenzetu wa Tanzania Bara wanavyofanya, au si hivyo sheha akitoka CCM naibu sheha atoke *CUF*

tupate ule uwiano mzuri wa kujenga imani. Hii itakuwa nzuri zaidi kuwajenga wananchi wetu matumaini mazuri sana, kwa kuwa ni mashirikiano tunafanya kazi kwa pamoja, lakini hii *supporter* tunayowapa hawa nao aa, imekuwa mtihani mkubwa. Mhe. Waziri namuomba alifikirie sana hilo na alifanyia kazi.

Nikija katika Vikosi Maalum vya KMKM tuwapongeze tu kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuliokoa zao la karafuu. Lakini imezungumzwa hapa katika Kikosi hiki ukurasa wa 76 kifungu (a) mpaka (h) kuna vitendea kazi vikubwa na vidogo vimenunuliwa lakini kwa masikitiko makubwa sana nasema kituo kilichopo Likoni, Kojani nacho ni Kituo cha KMKM lakini masikini ya Mungu hata *Fiber boat* hawana. Kuna bahari kubwa tu, lakini hana boti ya kuweza kupiga *patrol* hawana.

Mhe. Spika, inasikitisha zaidi anapokuja mgeni wa kitaifa boti mpaka ziletwe mjini kwa gari zikishakumsafirisha mkuu huyo halafu zinaondoka, inasikitisha na mashine walizonazo si nzuri ni mbovu kabisa za matengenezo kila wakati, wanalazimika kuazima mashine za watu hawa tena za wavuvi. Kwa hivyo, nasema na Kituo cha KMKM kiliopo Kojani kina hadhi kama vituo vingine basi wapatiwe angalau usafiri wa boti.

Mhe. Spika, kwa kujali muda wako na mchango wangu huu mfupi naomba niishie hapo waziri atakapokuja atupe maelezo kuhusiana na mambo ya vitambulisho na mengine niliyozungumza. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe tunakushukuru kwa mchango wako huo. Waheshimiwa Wajumbe tunakabiliwa na upungufu wa muda tukizingatia pia vile vile kwamba tuko nyuma ya ratiba ya kuendesha shughuli zetu. Wajumbe waliyoomba kuchangia hoja hii jumla yake ni 33, waliokwishachangia hadi sasa ni 12 bado kuna 21 hawajachangia**.** Nimejaribu kupunguza punguza muda ili tupate wajumbe wengi zaidi lakini bado haikusaidia. Kesho ambayo bado tutakuwa tuko nyuma ya ratiba yetu asubuhi tunategemea tufanye majumuisho ya hoja hii. Kwa hivyo, muda tuliobakia nao ni muda wa saa tatu kasorobo za jioni tumalize Wajumbe 21 ni vigumu na pengine haiwezekani.

Kwa hivyo, nikuombeni Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu yote ni ya kwetu kufuata taratibu za muda wa kuchangia ni muhimu, kufuata ratiba yetu tuliyojipangia ni muhimu kwa sababu hii inakwenda na bajeti ya matumizi, tukichukua muda mkubwa zaidi kuliko ule uliopangwa hatimaye tutapata tatizo kama tulivyopata katika kumaliza mwaka wa fedha uliopita, kwamba tulishindwa baadhi ya mambo kuyafanya kwa sababu tumemaliza vifungu vyote. Kwa hivyo, inabidi tuangalie pande zote ili twende kwa mujibu wa matumizi yaliyoidhinishwa na Baraza hili, sisi tuoneshe mfano tukienda zaidi ya hapo itakuwa tunakwenda kinyume na matumizi yaliyoidhinishwa na Baraza hili, kama vile tunavyoziambia wizara zitumie kwa mujibu wa idhini tuliyotoa basi na sisi tujirudie tutumie kwa mujibu wa idhini hiyo hiyo.

Sasa jioni niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tupange *points* zetu vizuri, tujaribu kupunguza muda, tujaribu kuepuka kurudia rudia ili tupate wajumbe kiasi tutakaoweza kuwapata na kama tulivyojipanga kwamba kesho Mwenyezi Mungu akipenda asubuhi tumalize hoja hii.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo basi naahirisha kikao hiki hadi saa 11 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ninakushukuru wewe na Inshaalla nitajitahidi kwenda na muda. Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake. Lakini pia nichukue nafasi hii ya kumpa pole sana swahiba wangu Dr.Mwinyihaji.

Mhe. Spika, Wizara hii ni wizara kubwa, ni wizara yenye dhamana nzito. Bahati mbaya nilisema mara moja, na leo ninarudia kwamba wizara hii ya Rais imejazwa vitu, imeingiziwa mambo yanayopoteza heshima ya wizara. Taswira ya wizara ya Mhe. Rais kwa vikombezwakombezwa vilivyoingizwa harufu ya wizara inakuwa chafu.

Mhe. Spika, kwa sababu kuna eneo ambalo kamati yetu bado tunalifanyia kazi, nataka niiache kwa kadri itakavyowezekana. Lakini Mhe. Waziri nakuomba unisikilize kwa makini sana. Nataka majibu ya maeneo haya

nitakayoyataja. Muda leo hautoshi lakini ukija na majibu maridhawa mimi tutakuwa pamoja, kwa sababu ya eneo hilo ambalo tunalolisubiri inshallah leo nitatumia muda mfupi sana.

Mhe. Spika, Baraza la Mji wa Wete, Chake-Chake na Mkoani, haya masoko yetu hebu twambie tukusikie na wananchi wa miji hii wasikie ni lini masoko haya yatajengwa. Kuna uvumi kwamba kulikuwa na mswada wa fedha, na fedha hizo zikawa zimeshafika hapa nchini. Lakini zimetelekezwa ofisini kwako. Munaulizana mukarabati au mujenge. Uvumi huo ni kweli ama usahihi wake ni upi.

Na kama ni kujenga ni kiasi gani cha fedha kimepangwa kuyajenga masoko haya ya miji mitatu hii. Lakini kwa Baraza la Mji wa Wete Mhe. Spika, sasa hivi tuna tatizo la uzoaji taka hatuna gari. Mhe. Spika, mama zetu wanazifanya kazi hizi za kusafisha mji ule katika mazingira magumu mno.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri atatwambia nini juu ya hili. Vifungu muda hautoshi lakini nilikuwa leo nikamatane na vifungu mpaka kieleweke lakini una bahati nzuri na muda, leo unakuokoa.

Mhe.Spika, Wizara hii Mhe. Rais amemteua Dk. Mwinyihaji. Nina imani anamuamini kama tunavyomuamini. Dk. Mwinyihaji, ofisi hii ndugu yangu nakuomba fanya kama vile tulivyokuwa kule tunakotoka. *Otherwise* mambo hayatokuwa mazuri. Sisi tunajua unaimudu, ninashangaa kwa nini yakupite mambo kwapani kiasi ya hiki yanavyokupita.

Mhe. Spika, baada ya masuala ya Baraza la Mji, maeneo yasiyofaa kuwa vituo vya kuegesha gari za dala dala hapa Unguja. Mhe. Waziri nakuomba sana fanya ziara ya makusudi na uzingatie hayo ninayoyasema. Kituo cha daladala kilichopo njia ya kwenda Kwarara barabara ya Fuoni pana skuli, msikiti na njia nne zimegawika, hali ni mbaya mno kiasi kwamba wanaotunza usalama wa pale, askari wetu hawa wa barabarani wanashindwa hiyo hali. Inatishia maisha ya watu. Haitokuwa vyema hata kidogo kusubiri yafike ndio uje hapa utwambie niaminini. Tunakwambia hivi sasa na sisi utuamini kwamba hali ya pale haifai, ni mbaya na haipendezi.

Lakini pengine ni Soko la Mwanakwerekwe. Pale imekuwa ni maudhi, karaha, aibu, haifai hata kidogo, soko lipo hali yake tunaifahamu lakini uegeshaji wa magari, matoriri, baiskeli na mikokoteni, ni hapo hapo kiasi kwamba hata ukipita kwa ile vespa mgonjwa, mzazi inakuwa taabu. Juzi mzazi kazalia pale pale hapana pa kupita na gari.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ninakuomba tafuta iwezekanavyo, si kuongeza viburuji tu kule nyuma, wale wenye mikokoteni gari ikishusha mzigo imemaliza kazi iondoke. Kuna watumiaji wa barabara ile wanaolipia kodi. Leo gari zile nyengine ni maduka. Duka linaendeshwa ndani ya gari.

Mhe. Waziri ninajua hayo huyajui lakini mimi ninakwambia. Tunayashuhudia na mimi ninafahamu ni mwana kamati, nafanya kazi si kwa ule muda tu lakini pia katika shughuli maalum ninakwenda kuyatizama haya mambo ni kero. Kamati ikipangwa kwenda pale basi mpaka wale wauzaji wa nje wanaondoshwa. Inakuwaje hivi sasa ile hali namna ile. Mhe. Spika, Mhe. Waziri haya mengine tunayoyasema hayataki gharama.

Jengine Mhe. Spika, ni upande wa Tawala za Mikoa. Serikali za Mitaa duniani kote zinaleta ufanisi mkubwa wa maendeleo ya nchi husika. Mhe. Spika, wizara hii suala la Serikali za Mitaa linakuwa na kigugumizi kikubwa. Ninashukuru hii kauli iliyotoka hivi sasa. Lakini Mhe.Waziri tunakuomba Mwenyezi Mungu akifikisha katika bajeti inayokuja hatutaki tena hii kauli ijirudie.

Sioni sababu ya kigugumizi ya Tawala za Mikoa. Serikali za Mitaa ikapewa nafasi yake ya kufanya kazi. Kwa nini Serikali kuu ipo tu na Serikali za Mitaa zinafanya shughuli zake.

Mhe. Spika, Mikoani na Wilayani ofisi zetu zina matatizo makubwa. Mhe. Spika, Ofisi ya Wilaya ya Wete ukija ukileta ugeni ni mtihani pale, vyoo vyetu havifanyi kazi, maji hatuna, tunaombewa na ile hoteli iliopo jirani yetu.

Kwa hivyo kwenye kitabu hiki haya siyaoni, lakini Mhe. Spika, ninakuomba sana kwamba afahamu Mhe. Waziri zile ofisi zinafikiwa na ugeni mkubwa lakini licha ya ugeni, hata wanaofanya kazi katika ofisi zile wanahitaji huduma ile ni ya lazima. Si vyema hata kidogo unafikwa na shida ya kujisaidia wafukuzia kwa majirani.

Jengine Mhe. Spika, wenzangu waliliona, kitabu kimejaa lugha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya mwaka uliopita na ujenzi, ukarabati, majengo ya Ikulu, majengo ya serikali. Ikulu ni ngapi hazitajwi, majengo ya serikali ni mangapi hayatajwi. Takwimu ipi ya gharama haitajwi Mhe. Spika, utaratibu huu hatuutaki. Hatutaki lugha za kufunga funga, hapa tunapitisha fedha za watu na sisi ndio tuliopewa dhima. Usipotuwekea wazi tukikwambia tunazuia hapa, tunamega shilingi mia mia mpaka utuweke sawa haya.

Tunataka lile bango kitita na hapa utuwekee kwenye masuala ya sarufu. Hizi fedha za watu, mwaka jana hukutwambia zile ulizokamilisha Ikulu gani na umetumia gharama zipi, lakini na mara hii zimebaki shilingi ngapi au bado. Humu munatwambia tu majengo munataka kuyauza ya serikali, huku munataka kuyakarabati, tufahamu nini. Ndipo niliposema hiki ni kizungumkuti na lugha hii si sahihi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wewe ni Dr. unaongoza ofisi hii. Umeaminiwa na sisi tunakuamini. Usitufikishe mahali ofisi hii ikaanza mtitiko.

Mhe. Spika: Una dakika 5.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, dakika nne zinatosha kumshukuru.

Mhe. Spika, fungu 08 Baraza la Mapinduzi item 0501 gharama za mafuta na vilainisho zimezidi nusu ya mwaka jana. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja twambie kuna nini.

Lakini Baraza la Mji wa Wete Mhe. Spika, mshahara umekwenda zaidi ya nusu ya watumishi waliopo hivi sasa. Mhe. Waziri uliomaliza mwezi wa Juni mwaka huu, Julai hii ni mara mbili. Waniambie kumeongezwa watumishi pale. Lakini kwenye uendeshaji umeiondoa fedha ile kumbe umezidisha kwenye mishahara, huku uendeshaji umefuta karibu nusu tena nyengine. Jee kuna nini.

Mhe. Spika, la mwisho nataka majibu hayo. La mwisho ni Vikosi vya SMZ. Kelele kwamba tunaajiri wengi, hawana vitu vya ufafanuzi wa shughuli zao, kumbe kuna siri. Kuna siri moja pengine zipo nyingi.

Mhe. Spika, kwenye vikosi hawajui mishahara mipya, vikosi hawapewi *pay slip*s zao, hawana chakula, hawapati posho ya likizo, hawana posho ya uhamisho, hawajui posho ya usafiri, hayo mazingira magumu hawaulizwi. Sasa katika yote haya na ile namba kubwa ya ajira huu ndio msitu au chaka Mhe. Spika.

Hapa mkaguzi na mdhibiti ripoti yake magugu mengi ya matumizi machafu yapo humu. Hapa pana jambo Mhe. Waziri tunakuomba uje utupe uzuri kwenye maelezo, na kasma hizi za vitabu ninafikiri huko ndio tutakuwa na maelezo sahihi. Ninatajataja Mhe. Spika, kutokana na muda wako kusudi nije nipate ile fursa ya vifungu. Ninakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninachukua nafasi hii kukushukuru na nikumbushe tu bajeti yoyote inatakiwa ianze kwa wananchi huko chini. Bahati mbaya sana bajeti zetu haziwafikii walengwa, na huyu Mwakilishi badala ya kupewa dakika 20 anapewa dakika 15, kwa hivyo kwa kweli Wazanzibari hatuwafanyii haki.Lakini najua siwezi kukulaumu kwa sababu ya muda lakini kuna haja ya kuzingatia.

Mhe. Spika, mimi kwanza naomba niseme kwa upeo wangu siwezi kuunga mkono hoja hii hadi pale Mhe. Waziri atakaponiridhisha.

Mhe. Spika, bajeti hii ametuomba tumpatie shilingi bilioni hamsini ikiwa bilioni arobaini na sita nukta sita ni kazi za kawaida, na bilioni moja nukta tisa kazi za maendeleo. Kwa ujumla bajeti hii kila shilingi mia Mhe. Spika, Wazanzibari wametengewa shilingi nne ndio za maendeleo, shilingi tisini na sita ni kwa ajili ya kazi za kawaida; mishahara na maposho. Kwa hivyo Mhe. Spika, hii bajeti ya Mhe. Waziri kila shilingi mia ya bajeti yake amejikaza sana kwenda shilingi nne kwa maendeleo ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, kuna sehemu moja nilitembelea na nikapewa hadithi moja. Kuna mtu alikuwa amezoea sana kuwadanganya watu, aliwadanganya watu kwa muda wa miaka 50. Siku moja akasahau akasema ukweli ndio siku hiyo hiyo aliyokufa. Kwa hivyo ninawasihi Wazanzibari wenzangu kwamba tusijaribu kudanganya, kwa sababu ukizoea sana, kuna siku moja utakufa kwa kusema ukweli.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwenye hotuba hii kwenye ukurasa wa 56 ametwambia kwamba Baraza la Manispaa limekamilisha michoro kwa ajili ya kujenga ofisi ya mapato. Mimi nina-*challenge* ama ametutania ama sentesi yake haikuwa sahihi.

Mimi nimebahatika kupata barua mbili Mhe. Spika. Barua ya kwanza ni Wazanzibari wazalendo waliomba eneo la makontena kupewa kwa ajili ya kuendeleza *shopping mall.* Barua hizo Mhe. Spika, zipo na hao wote wazalendo wamekataliwa. Lakini nimebahatika kupata barua ya Kampuni ya Mtaliana, aliyeomba kujenga *shopping mall*, yeye amekubaliwa.

Mhe. Spika, naomba niisome. Anasema kwamba *"the various departments of Zanzibar government including Second President's Office have gone through your development proposal and they come to the conclusion that there is no problem with the concept design as long as structure assembly"*, kwamba ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imeona *concept* ya *project* yake na haina tatizo.

Na wanasema kwamba waombaji wote waliomba kampuni hii ndio *the best one*, kwa hivyo wamekubali kuwapa. Lakini Mhe. Spika, nimetishika sana pale barua hii ambayo imeandikwa na Ndugu Rashid A. Juma – Director, alisema kwamba, *"there are several government procedures and requirements have we need to consider for the sitting with your selves to negotiation and drop up the agreement our shares and participation in the proposal development.*

Mkurugenzi anamwambia kampuni kwamba kabla hatujakaa tunaomba tujue hii nini *share* yetu kama tatizo serikali. Hii ni rushwa. Ndio Mhe. Waziri anatwambia kwamba kumbe mchoro huu umo kwa ajili ya ofisi za Manispaa. Kwa barua hii kuna mtu tayari wameamua kumpa kwa ajili ya *shopping mall*.

Mhe. Spika, anawadanganya nani. Mhe. Spika, hii ni hatari. Kumbe Wawakilishi wanatumiwa kupitisha bajeti kwa ajili ya kupewa Mtaliana, Wawakilishi hawatumiwi kupitisha bajeti kwa ajili ya Mzanzibari mzalendo ni hatari kubwa. Na kwa kweli mimi kama nimechaguliwa na watu wa Jimbo la Kiwani sitofanya kosa hili. Mwenyezi Mungu aninusuru kupitisha bajeti kwa ajili ya ujanja.

Leo Mhe. Spika, Mhe. Waziri tangu niingie humu ndani ya Baraza la Wawakilishi huu ni mwaka wa saba sijawahi kumsikia akiniambia neno zuri ambalo ni la ukweli, hadaa, mtego na hila.

Leo Wawakilishi wanaambiwa wapitishe bajeti hii, kumbe kuna barua tayari Mtaliana anapadowea ajenge *shopping mall.* Mhe. Spika, hii ni hatari na kwa kweli wawakilishi tuwe makini sana kuwakingia kifua kwa ajili ya hadaa. Hilo moja Mhe. Spika.

Mhe. Spika, la pili mara kadhaa tumekuwa tukiambiwa Waziri wa Vikosi na Waziri wa Sheria kwamba Mzanzibari yeyote ambaye anayekwenda Mahakamani akila kiapo anapata cheti cha kuzaliwa na kadi ya Mzanzibari. Mimi nimebahatika kupata orodha ya Wazanzibari ambao wameenda Mahakamani, Mahakama imesema hawa watu tunawatambua na hawakupata haki zao.

Mhe. Spika, ni kusema kwamba hata Mahakama haiheshimiwi. Mahakama kumbe ndogo kuliko Waziri, Mahakama kumbe ni ndogo kuliko mkono wa mtu. Ikiwa Mahakama imesema kwamba huyu mtu ana sifa ya kupewa hiki kitambulisho, leo hapewi aje atwambie hapa utawala bora, maana utawala wa hadaa. Ikiwa Mahakama ndio chombo cha kutoa haki na imesema huyu ana sifa ya kupewa kitambulisho cha Mzanzibari, ushahidi Mhe. Spika, ni huu hapa. Na kama watu wataitwa leo basi wanaweza kufika watu elfu thalathini haki yao hawaipati. Leo tunaambiwa nchi hii kuna utawala bora hakuna matatizo, ni maneno ni sawa sawa na hadithi.

Mhe. Spika, hii ni *point* ya pili kwamba sina sababu ya kuunga mkono hotuba hii. Miaka mitatu Mhe. Spika, baadhi ya watu walilalamika hapa kwamba hakuna haja ya kuajiri vijana wengi katika vikosi. Lakini serikali ikajenga hoja kwamba hawa ni wenzetu, maana yake tunataka jeshi tukakubali. Wakachukuliwa vijana zaidi ya 200 wakapewa kozi, hatimaye walirudi wakaomba ajira.

Wametumikia kulinda ofisi na nyumba zetu zaidi ya miaka mitatu, leo wanaambiwa vijana wale hawana sifa, wanafanya kazi ile kwa makosa, maana yake mtu anapewa bunduki wakalinda leo wanaambiwa wamefanya kwa makosa. Mhe. Spika, haya si maneno yangu ni maneno ya vijana kwa barua, na ni majibu kwa serikali kwa vijana.

Mhe. Spika, vijana 200 ambao tumewatuma wamelinda nyumba, ofisi na mali zetu, leo wanaomba kazi wanaambiwa hawana sifa. Lakini wamechukuliwa watu ambao hawajapitia jeshi wameajiriwa katika jeshi na orodha ipo.

Sasa unafikiria nini ikiwa mtu unampa mafunzo ya kupiga bunduki hana sifa, unamchukua mtu ambaye hajapitia jeshi unampa kazi ya jeshi, tutarajie nini. Kwa kweli Mhe. Dr. Mwinyihaji, kaka yangu na Waziri wangu ana kila sifa ya kuambiwa kuwa ajiuzulu, ana kila sifa kwa hiyari yake kujiuzulu.

Kwa sababu Mhe. Spika, mimi ningetegemea vijana ambao tumewafunza kwa kuwapa silaha wakalinda, wakapewa kipaumbele wakaajiriwa. Leo unapowaambia kama hawana sifa, maana yake kamati za ulinzi za Mikoa zimefanya makosa. Si kweli. Kamati ya Ulinzi ya Mkoa mpaka inaamua huyu aende jeshi maana yake huyo mtu amekubalika. Lakini Mhe. Waziri kwa kweli ni mtihani.

Mhe. Spika: Una dakika 5.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, dakika 5 bado lakini ninakubali hivyo hivyo kwa sababu ya Spika.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba ametoa mafunzo kwa Halmashauri katika Unguja na Pemba. Mkoani, Wete na Pemba kwa jumla hajatoa mafunzo hata siku moja. Madiwani wenyewe wanasema kuwa hawajamuona kutoa mafunzo hata siku moja. Sasa atwambie ni mafunzo yepi. Maana Pemba kutoka Micheweni mpaka Wete hakuna mafunzo. Kwa hivyo kama fedha hizi zimetumika katika mafunzo ni mafunzo yepi. Ni Halmashauri zipi za Pemba ambazo ametoa mafunzo haya.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda niseme tu mimi kwamba nimemzoea sana na ninamjua sana Mhe. Waziri wangu, na kila Mhe. Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi anamjua sana. Kwa hivyo hatuna haja ya kumpa bajeti hii kwa sababu ataendelea kutufanyia masikhara.

Na ninaomba sana mimi aniambie, nini madhumuni ya sentensi hii kwamba kuna mchoro umekamilika kwa kujenga ofisi ya mapato ya Baraza la Manispaa, huku akitoa barua kwa Mtaliana ajenge *shopping mall*, kakusudia nini.

Mhe. Spika, ninashukuru sana. Siungi hoja mpaka nipate ufafanuzi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya dakika 15 kama ulivyosema ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwanza nimpongeze kwa usomaji na umahiri wake wa kusoma *speech*. Juzi tulishuhudia akisoma hii *speech* kama charahani, hatukutegemea kama ataimaliza lakini tunashukuru ameimaliza.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu katika Ofisi ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, mimi niwapongeze watu hawa wa Vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi. Pamoja na matatizo na malalamiko mengi ambayo yanatolewa na Waheshimiwa wenzangu lakini kwanza lazima tuwapongeze. Kwa sababu wanafanyakazi kwa bidii na uzuri sana

Mhe. Spika, vitambulisho hivi vya Mzanzibari Mkaazi ni vya aina yake, na wenzetu hawa wameshatunukiwa shahada mbali mbali juu ya vitambulisho vyenyewe. Pamoja na shahada wanazopewa Mhe. Spika, bado wanahitaji kuwezeshwa zaidi ili wapate vifaa vya kisasa zaidi, kwa sababu hivi vifaa walivyokuwa navyo inaonekana vina mapungufu, kuna baadhi ya *contact* ambazo mwananchi angetakiwa ziwe zinaonesha moja kwa moja, lakini humu kidogo zimekosekana.

Kwa hivyo, niiombe serikali ifanye-*follow up* juu ya vitambulisho hivi, na ifanye uwezekano wa kuwawezesha wenzetu hawa wa vitambulisho, ili wawe na mitambo ya kisasa zaidi kuliko hii waliyokuwanayo sasa hivi.

Mhe. Spika, vitambulisho hivi vimewekwa kwa mujibu wa sheria ya nchi, na vina taratibu zake za kisheria. Mimi naamini kama sheria zitafuatwa, basi malalamiko haya yatapungua. Kila mtu ana haki ya kuwa na kitambulisho. Sheria inasema kwamba mtu aliyetimia umri wa miaka 18, basi anayo haki ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari na kwa sababu vitambulisho hivi ndivyo vinavyomuwezesha kila mtu aweze kupata baadhi ya haki zake. Ukitaka passport ni lazima uwe na kitambulisho, ilimradi kila jambo linahitaji kitambulisho. Kwa hivyo, haki ya kupata kitambulisho hiki ni muhimu na ni ya msingi, lakini ni lazima taratibu zifuatwe.

Mimi ninavyofahamu Mhe. Spika, ukitaka kuwa na kitambulisho cha Mzazibari Mkaazi, ni lazima uwe na barua ya sheha, ambayo itakuwezesha kufika katika ofisi inayohusika kwa ajili ya kupata kitambulisho. Sasa mimi sioni tatizo liko wapi na mimi naamini ofisi ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, kama utafuata taratibu basi kitambulisho chako utakipata, wala hakuna tatizo.

Mhe. Spika, mimi muda wote huu niliokuwepo sijapata malalamiko kutoka katika jimbo langu, kwamba mwananchi amekwenda kutafuta kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi akakikosa. Sasa nakua mzito sana wa kuamini juu ya watu wanaolalamika kuhusu suala hili.

Juzi Mhe. Spika, nilikwenda katika Ofisi ya Vitambulisho vya Mzanzibari Wilaya ya Mjini kwa shughuli zangu binafsi, kwa bahati nilioneshwa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi vilivyopo pale ambavyo wananchi hawajaenda kuvichukua, ni vingi mno. Lakini sasa huku ukipata malalamiko kwamba watu hawana vitambulisho, lakini unapoingia kwenye ofisi ile basi utakuta idadi ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ni vingi, ambavyo watu wameshapigwa picha, vimeshachapishwa lakini wananchi hawaendi kuvichukua. Sasa utajiuliza kulikoni, kwamba mtu amekwenda amepiga picha kitambulisho chake kipo, lakini hajaenda kukichukua. Kwa hivyo, nahisi hapa pana matatizo kati ya wananchi wenyewe na ofisi zenyewe na utaratibu wenyewe.

Kwa hivyo, mimi binafsi Mhe. Spika, niwapongeze sana wenzetu hawa wanafanya kazi vizuri sana, wanajitahidi na kwa kweli mtu anapofanya kazi nzuri ni wajibu wetu tuseme kwamba huyu anafanya kazi vizuri. Anapofanya kazi vibaya basi ni wajibu wetu tuseme kwamba huyu anafanya kazi vibaya.

Mhe. Spika, nije sasa kwenye Idara maalum ya vikosi. Wenzetu hawa wa vikosi vya SMZ wana majukumu yao mbali mbali, wengine uzalishaji, ulinzi, wengine wanalinda baharini na mambo mengine, wanajitahidi kutulinda, wanajitahidi kufanya kazi zao na wao ni lazima tuseme kwamba wanafanya kazi vizuri.

Lakini Mhe. Spika, kidogo kuna manung'uniko ya hawa askari wao, hawa wamekuwa na manung'uniko mengi sana, hawa wapiganaji wa vikosi vyetu, mbali ya maofisa, hawa askari wa chini ambao ndio *frontlines*. Hawa wamekuwa na malalamiko ya kila siku, wana malalamiko juu ya *style* zao, wana malalamiko juu ya taratibu wanavyo shughulikiwa na wana malalamiko mengi Mhe. Spika. Nimuombe Mhe. Waziri kwa makusudi basi akutane nao hawa wapiganaji, ili kuwasikiliza matatizo yao. Wengine hawajui mishahara yao inakwenda vipi. Leo anapewa shilingi mia, kesho anapewa shilingi hamsini na keshokutwa anapewa shilingi mia na hamsini, yaani imekuwa hakuna utaratibu maalum juu ya mishahara yao. Hii ni hatari, hawa ni vijana ambao tunawategemea katika masuala mbali mbali ya kitaifa. Sasa kama mtu hafahamu hasa maslahi yake, hili ni jambo la hatari.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwa kweli unahitaji ukae na hawa wapiganaji ili uwasikilize matatizo yao. Sisi wanatujia kama Wawakilishi wao, kuna matatizo sana. Maslahi yao yanahitaji kulindwa, mikato inakuwa ni mingi isiyokuwa na utaratibu, wamekuwa wakikatwa fedha zao ovyo na wanaposema wanatishiwa kufukuzwa kazi. Kwa hivyo, hii ni hatari sana Mhe. Spika.

Jengine Mhe. Spika, nakumbuka hapa Mhe. Waziri tulikubaliana hapa kwamba askari hawa ambao huwa wanapewa fedha za chakula, sijui wenyewe mnaziitaje. Lakini fedha hizi wakati wanapokwenda *detach*, kama askari amepangwa *detach* kutoka hapa kwenda mpaka mahala fulani, basi fedha zile ambazo wanapewa kila mwezi zinakatwa na tulikubaliana kwamba fedha hizi zisikatwe. Hata kama askari anakwenda *detach* mahala fulani, basi fedha zake anazolipwa azipate kamili vile vile, hata kama huko anakokwenda anakula, kwa sababu na huku anakoondoka nako kunaliwa vile vile. Ana mke na watoto. Kwa hivyo, unapomchukua na kumpeleka *detach* maana yake zile pesa za *ration* zinakatwa. Sasa huku anakotoka afanye nini.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nasema wakati utakapokuja kufanya majumuisho juu ya suala hili, basi utupe uwazi juu ya askari wetu hawa. Haiwezekani kwamba askari anakwenda *detach*, halafu mshahara wake unakatwa, eti kwa sababu

kule anakula. Hivi hatuna *advantage* yoyote kwa mtu jamani, kila kitu tunakuwa tuko *strict,* hatuna kitu ambacho kitamwezesha angalau askari akapenda kwenda *detach*.

Mhe. Spika, nakumbuka hili tuliwahi kukubaliana na Mhe. Waziri na mwenyewe akasema kwamba hili ni tatizo. Lakini inaonekana bado linaendelea na wapiganaji wanakatwa fedha zao wanapokwenda *detach*.

Jengine Mhe. Spika, wapiganaji hawa hawa wanakatwa fedha za michezo bila ya ridhaa yao, wakati ukiangalia kwenye hii bajeti kuna mafungu ya fedha za michezo. Mhe. Spika, nadhani hili tusiwalazimishe wapiganaji wetu, tusiweke kwamba ni kitu cha lazima, michezo sio kitu cha lazima ni kitu cha hiyari. Kwa hivyo, anayetaka kuchangia atachangia na asiyetaka kuchangia basi.

Mhe. Spika, la mwisho. Mhe. Spika, naona unaniangalia sana, nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuifungua ile njia ya Mji Mkongwe. Taarifa nilizokuwanazo ni kwamba Mhe. Waziri jana usiku njia ile ilifunguliwa. Nadhani kuna mtu amemnong'oneza Mhe. Waziri kwamba atufungulie ile njia, na kwa sababu mimi nilileta karatasi yangu ya kuchangia, kwa sababu ya njia ile tu. Kwa hivyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuchukua hatua ya kuifungua ile njia, ili wananchi wakaweza kuitumia.

Kwa kweli Mhe. Spika, kulikuwa kuna malalamiko mengi na manung'uniko mengi juu ya njia ile na Mhe. Waziri mwenyewe alituahidi kwamba ataifungua, lakini ndio kwanza jana usiku ameifungua. Kwa hivyo, nampongeza kwa usikivu wake, namuomba aendelee kwa kila jambo ambalo anaambiwa kuwa hili baya, basi aone kwamba hili ni baya.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako, naunga mkono hoja na nakutakia kila la kheri, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwanza nataka nianzie katika ukurasa huu wa 33 ambao unazungumzia hivi vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, bado nasema hivi vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi vina matatizo kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kama mimi Mheshimiwa nikienda katika ofisi ya vitambulisho, basi itakuwa haitimizi hata dakika tano nitachukua kitambulisho niondoke. Lakini sasa tuwaulize hawa wananchi wa chini, pamoja na kwamba mheshimiwa kasema kwamba kuna vitambulisho vingi, walivyokuwa wenyewe hawajavichukua, ni kweli kabisa. Lakini tatizo lake ni nini. Tatizo lake ni kwamba mtu anakwenda siku tatu au nne anataka kitambulisho na kipo, basi anaambiwa wewe jina lako haliko. Kwa sababu mimi nilikuwa na watu katika jimbo langu zaidi ya watu 60 waliokwenda na wana vibali vyao vya kuchukulia vitambulisho, walipiga picha kwa ajili ya kupata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, lakini kitambulisho hakionekani, sasa mtu anakata tamaa, kwa sababu anakwenda zaidi ya siku tatu, nne au wiki mbili anakwenda na kutaabika tu, halafu wanakata tamaa.

Mhe. Spika, bado nasema Wazanzibari kama ni haki yao kupata hivi vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, basi wapewe. Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita mimi nilizozana sana na Mhe. Waziri, na nilizozana naye kwa sababu ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kwa wazee. Kwa sababu Mhe. Spika, mzee wa miaka 60 au 70, na nilieleza kama huko nyuma wazee wetu walikuwa hawana umuhimu wa kupata vyeti vya kuzaliwa. Sasa mzee anakuja kama mama Mhe. Asha au zaidi ya Mhe. mama Asha, unakuja kumwambia alete cheti cha kuzaliwa leo, atakitolea wapi hicho cheti cha kuzaliwa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tulisema hapa na mimi nilizozana naye sana hapa, na akaniahidi kwamba suala hili litamalizika. Lakini tatizo lake ni kwamba sisi tunakuja humu tukizungumza tunapewa ahadi nzuri, lakini utekelezaji wake unakuwa haupo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri nilizozana naye sana hapa na nikatoa mifano, kama jamani hii sheria kama ina matatizo tuiwekeni sawa, lakini haiwezekani mzee wa miaka 70 au 80 umwambie akalete cheti cha kuzaliwa, atakitolea wapi, na nilitoa mifano kwamba kama kwetu Micheweni na zaidi ya Micheweni, walikuwa wazee zamani hawana umuhimu wa kupata cheti cha kuzaliwa. Sasa unapomnyima haki mzee yule na mtoto wake ni Mzanzibari lakini baba ni mgeni, maana tutizame matatizo yaliopo. Mwana ni Mzanzibari Mkaazi, lakini babangwa ni mgeni wa kupigwa mikwaju.

Sasa hivi Mhe. Spika, huwezi ukenda hata Mahakamani ikiwa una mtoto wako kashtakiwa unakwenda kumchukulia dhamana, huwezi kupewa dhamana kama huna kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, sasa hivi huwezi kufanya kitu chochote kama huna kitambulisho. Kwa hivyo, kuwanyima wenzetu tunawapeleka wapi na nchi yao ni hii, wao tunawafanya wageni kwa nini. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwa hili anieleze vizuri sana mpaka nione kama nitaweza kukubali suala hili, si hivyo mimi nitakuwa mkaidi kweli kweli mara hii, tena aandae majibu mazuri ya kuja kunijibu, kwa sababu katika kipindi kilichopita aliniahidi, lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Hilo moja.

Suala la pili Mhe. Spika, jambo ambalo nitakuwa mkaidi na Mhe. Waziri ni suala la Ikulu ya Micheweni. Waheshimiwa Wajumbe nyote ni mashahidi humu, mpaka Mhe. Abubakar aliingilia kwenye suala hili. Kwa hivyo, Mhe. Waziri aliniahidi akasema kuwa nakuahidi kama Mwenyezi Mungu akipenda suala hili litamalizika. Leo imeshamalizika tena miaka miwili, hakuna suala lolote linalofanywa, ni gofu tu lile la Micheweni. Mhe. Spika, tunapoanza kujenga magofu tu kisha tukayaacha. Kubeba mzigo kuwa unaupeleka kisha ukautua njiani, ni sawa sawa na kuwa hujaufanya kitu chochote. Kwa hivyo, na hili nalo Mhe. Waziri aandae hoja nzuri ya kuja kunijibu Mwenyezi Mungu akipenda. Kesho ajitayarishe aje anijibu vizuri mpaka ikiwa nitaridhika basi nitakubali, si hivyo basi mimi naona kama nitazuia shilingi. Mhe. Spika, hilo ni jengine.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze, nataka niwapongeze sana kwa dhati kabisa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Micheweni, naipongeza kwa nini Halmashauri ya Micheweni. Kwa sababu walijipangia malengo ya kukusanya milioni 30 katika kipindi kilichopita, lakini hadi kufikia mwezi wa Machi wameshakusanya milioni 60. Kwa maana hiyo nawapongeza sana na ninawaomba wawe na moyo zaidi na waendelee kukusanya. Lakini wakishakusanya basi zitumike fedha kwa ilivyo, kwa sababu ni fedha za wavuja jasho, hii kodi imekusanywa kutokana na wavuja jasho.

Mhe. Spika, suala jengine kutokana na hilo hilo, niilaumu serikali kuu kama serikali kuu inawanyima haki Halmashauri zetu za Mawilaya, kwa sababu gani. Kuna kampuni ambazo zinakuja zikitengeneza barabara, kampuni hizi zinakuwa zinachimba vifusi kwa ajili ya kutengenezea barabara, lakini serikali imewasamehe kodi kutokana na vifusi kusafirishwa kutoka eneo hili kwenda eneo jengine. Lakini sisi kama Halmashauri ya Wilaya tuseme pale kwetu Micheweni ukichukua jiwe, kokoto, mchanga hata ukichukua miti, unachopita nacho chochote unalipia Halmashauri ya Wilaya. Sasa hivi baada ya kuzisamehe ushuru kampuni, basi wanawanyima na hawa Halmashauri za Wilaya. Kwa hivyo, serikali ingewalipa Halmashauri za Wilaya ushuru wao, si hivyo kampuni zinapokuja na kutiliana nao saini basi ushuru wa Halmashauri za Wilaya waachiwe wenyewe wakusanye fedha zao, kwa sababu yale ni mapato yao wenyewe Halmashauri za Wilaya. Kwa sababu wanapochukua kifusi kusafirisha nje asilipe, basi anawanyima hawa mapato yao, kwa hivyo serikali izuie mapato yake ya kodi kuu za serikali. Lakini mapato ya Halmashauri za Wilaya waachiwe wakusanye mapato yao. Hilo ni jengine.

Suala jengine Mhe. Spika, ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu manispaa. Mhe. Spika, manispaa ndio yenye jukumu la usafi pamoja na wananchi, lakini manispaa ndio wenye jukumu la usafi katika mji wetu wa Zanzibar. Sasa Mhe. Spika, hii mitaro inayojengwa, serikali inagharamika kwa kujenga mitaro na fedha nyingi za serikali zinapotea. Lakini manispaa haiishughulikii hii mitaro baada ya kwishakujengwa inakuwa basi, wanaachiwa watu wanatupa taka ovyo, inaachwa mitaro inajifukia na halafu tunakuja kupata kazi nyengine ya kuja kufukua mitaro kwa gharama nyengine. Sasa kwa nini fedha za wavuja jasho hazionewi imani, kwa sababu kuifukia mitaro ile ikabidi tuje tuifukuwe tena kwa mara nyengine, tunaifukua tena kwa gharama nyengine mpya.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni suala hili la Halmashauri. Wananchi wa Micheweni walijenga soko wakajenga na ghala. Kwa bahati nzuri lile ghala walilojenga halitumiki tena kwa sababu serikali haiagizi tena vyakula. Lakini sasa hivi lile ghala linatumika kama chombo cha kuhifadhia masanduku ya uchaguzi, tuseme lile linatumika kwa ajili ya serikali, lakini sasa hili soko wananchi wao wenyewe hawakulitumia, halafu kuna watu wamezifanya kama ni ofisi zao na wakati huku wananchi wenyewe wanapiga kelele kila leo. Kwa hivyo, tunataka tujue kwamba hawa wanaokodishwa, wamekodishwa na nani lile soko na ilikuwaje mpaka wananchi wenyewe wasishirikishwe na wakati wamejenga wenyewe kwa nguvu zao. Kwa hivyo, na hili naomba Mhe. Waziri aje anipe ufafanuzi kuhusu soko lile la Micheweni ambalo wananchi wenyewe walijitolea, sasa soko limechukuliwa na limefanywa maofisi na upande mwengine limekodishwa. Kwa hivyo, na hili wenyewe wananchi wanataka wajue je, ilikuwaje mpaka soko lile wapewe watu wengine kuliko wao wenyewe.

Suala jengine Mhe. Spika, ambalo nataka nilizungumze ni suala la Chuo cha Mafunzo, lakini kwa kifupi ni Magereza. Mhe. Spika, kwa kusema kweli mule katika magereza kuna mambo mengi, lakini cha ajabu ukifika mule wale wanafunzi wa magereza, jamani wale ni wafungwa, wanavuta bangi, wanavuta sigara na wanavuta na vitu vyengine. Hetu tujiulize hizi bangi wanazozivuta kule ndani wanazipatia wapi. Hizi bangi wanazozivuta wanazipata kutoka kwa walinzi wetu, askari wetu ndio wanaowapa bangi na wanawapa kwa sababu gani, kwa sababu fedha tunazowapa haziwatoshi, mishahara tunayowapa ni midogo. Kwa hivyo, inakuwa wale walinzi wetu wanafanya biashara ya kujitafutia maisha, kutokana na mishahara tunayowapa wasivute bangi wafanye nini.

Mhe. Spika, kuna posho ambalo tunawapa hawa askari wetu, tunaliita posho la hali ngumu. Leo askari unakwenda kumpa posho eti ni la hali ngumu unampa shilingi 1,500/- ndio fedha hizo zimsaidie nini, asiuze bangi auze nini. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hawa askari wetu awaangalie kwa jicho la huruma, hawapati posho za likizo, hawalipwi mishahara na maposho yao yamelimbikizana. Mhe. Waziri walipe hawa watu pesa zao. kwa sababu wakilalamika wao wanailalamikia serikali, serikali musiitie aibu, hii serikali yetu musiitie aibu walipeni watu pesa zao, mnafanya fokochofokocho. Mhe. Spika, huu ni wakati wa ukweli na uwazi, mambo ya fokochofokocho yamekwisha yamepitwa na wakati

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, una dakika tatu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakuheshimu sana na naheshimu sana kiti chako. Naomba nimalizie hapo. Siungi mkono mpaka nitakapopata majibu mazuri sana kutokana na hoja zangu nilizozisema. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo na mimi nikatoa maoni yangu juu ya hotuba hii inayoendelea. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake bora.

Vile vile nawapongeza watendaji wake wakuu, na wote waliomsaidia kutayarisha hotuba hii. Mhe. Spika, sina budi vile vile nimpongeze Waziri kwa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio inayoongoza.

Mhe. Spika, mimi niende katika ukurasa wa 9 kwenye vipaumbele ambavyo Mhe. Waziri ametuainishia. Vipaumbele hivi naviona ni vingi sana, vile vya mwanzo ni sawa sawa na vya leo, maana yake nikizungumza vya mwanzo ni vya mwaka jana, yaani ni sawa sawa na vya mwaka huu. Vile vya mwanzo hakuweza kufikia hata nusu yake, lakini vya leo vimekuja vile vile.

Mhe. Spika, nimekuwa na wasi wasi hapa, kuwa tunatoa vipaumbele vingi katika serikali yetu, lakini kuvitekeleza hatuwezi. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri utakapokuja utuambie ni vipaumbele gani ambavyo utavichukua, tutaweza kuvitekeleza na mwakani tuvichukue vyengine, tusichukue vipaumbele vingi, sasa hivi tuchukue vipaumbele kidogo kidogo ambavyo tutaweza kuvitekeleza.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 39 kuhusu Afrika ya Mashariki. Katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki kuna muundo wa taasisi za Kiswahili pale, lakini Zanzibar kwa sababu haiwezi kusimama wenyewe, haina miguu ya kusimama katika Afrika ya Mashariki, basi taasisi ile imechukuliwa na Tanzania, lakini Tanzania ikaileta Zanzibar. Tayari mahojiano yale yamepita, sasa tunataka Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze, taasisi hii ya Kiswahili ni lini itakuja hapa Zanzibar Afrika ya Mashariki na itafanya kazi wapi na ofisi zake ziko wapi.
Mhe. Spika, nije tena katika ukurasa wa 50 katika Mkoa wa Kusini Unguja. Nataka kuishauri kamati ya ulinzi na usalama ya Mkoa wa Kusini. Kamati ya ulinzi ya Mkoa wa Kusini, sasa hivi sehemu ya Dunga eneo la Mesi ya Jeshi, pale siku za Jumamosi na Jumapili pamekuwa na hatari sana za kuhatarisha nchi hii. Nimekuwa natoa indhari kwa muda mwingi sana, kwenye mambo kama haya yakitokea. Nilitoa indhari juu ya ndugu zetu wa Uamsho ambao walitaka kutugonga na gari, lakini matokeo yake yakaachiwa mpaka sasa wamekuwa na nguvu kubwa. Sasa nawaambia na kamati ya ulinzi na usalama ya kusini nyoka anakuja kwao.

Lakini katika ukurasa wa 58 Mhe. Spika, nije kwenye Baraza la Manispaa. Mhe. Spika, nalipongeza sana kwa usafi mkubwa walioufanya. Lakini bado Mhe. Spika, lina mapungufu mengi sana Baraza la Manispaa. Nimesema limefanya matengenezo katika mitaro midogo midogo ya Mpendae, mimi sitaki kusema watu wazima waongo. Lakini nataka kusema wanalidanganya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, mitaro tumeisafisha wenyewe na tumetengeneza madaraja wenyewe. Kubwa zaidi katika kitabu cha mwaka jana, kwenye ukurasa huu wa 45, Mhe. Waziri ametuambia kwamba atatengeneza mitaro mikubwa kutoka Magomeni kupitia Kwabintihamrani, Jang'ombe hadi Kilimani kwa kupitia baharini. Mradi huu utachukua zaidi ya dola milioni 38. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nikwambie kwamba mradi huu ni ndoto, bado hatujauona watu wazima tunaanza kuota mchana. Wananchi wangu wa Jimbo la Mpendae bado wana kilio kikubwa sana, hivi sasa tayari kumekuja mambo mengine, kuna msingi mdogo unaotoka Mwanakwerekwe Jimbo la Magomeni kupitia Kwamchina mwanzo na kuingizwa Jimbo la Mpendae sehemu ya Kwabitihamrani.

Sasa hapa balaa linatukuta hili, hatujaletewa maji kutoka kwengine watu pale wanazama, leo tunaletewa mtaro ule na uingie pale, mimi na wananchi wangu hatutakubali kuletewa maji yale au Mhe. Waziri atuambie ni kitu gani kinachofanyika pale na vipi watafanya. *(Makofi)*

Vile vile tunataka *time frame*, kwamba hili la mwaka jana bado halijatekelezeka na leo unatuletea maji Kwabitihamrani. Kwa hivyo, mimi pamoja na wananchi, na mimi nitakuwa mbele kwa ajili ya kulisimamia hili suala na wala hatutalikubali. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu Soko la Mwanakwerekwe. Mhe. Spika, pale pahala ni pabaya sana kama tunavyopajua, tuangalie usafi wa pale ni mgumu sana na wala hauridhishi, na kamati yangu ilitembelea pale na iliona mambo mengi. *(Makofi)*

Lakini isitoshe kuna wafanyabiashara ambao tayari wanapanga bidhaa zao barabarani Mhe. Spika Mwenyezi Mungu atuepushie mbali, siku moja gari ikifeli *break* na kukatika *tire road* patakuwa na hasara kubwa itakayotokea. Kwa hivyo, tuangalie wapi tutawapeleka wale wafanyabiashara wa jioni wanaokaa pale chini, na wao tuwaelimishe jinsi gani barabara inavyotumiwa, pamoja na athari zake zinazoweza kutokea.

Mhe. Spika, wafanyabiashara wa pale wanalalamika sana kwamba wauziwa vibaraza kwa shilingi 400,000/= na wao wenyewe wanalipa shilingi 1,000/= kila siku, lakini hawapewi hata risiti na hilo ni tatizo Mhe. Spika. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba alishughulikie suala hilo. *(Makofi)*

Vile vile kuna *Diplomatic Shop (Supermarket)*, Mhe. Spika mimi ninayo mikataba mitatu, barua hizi tatu zinapingana kila moja. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika wakati atakapokuja anieleze ni nani mdhibiti au mwenye haki zaidi Manispaa au yeye? ama mtu mwengine kwenye barua hizi. Kwa kweli lile ni tatizo Mhe. Spika na litazaa tatizo.

Kwa maana hiyo, atueleze kwamba Manispaa ndio wanaodhibiti au serikali kupitia Waziri ndiye anayedhibiti, ama huyu mtu mwengine ndiye mwenye udhibiti pamoja na mamlaka ya kuweza kudhibiti au kumiliki hii *Diplomatic Supermarket*, ni aibu sana Mhe. Spika. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atakapokuja atuambie ni nani hasa mmiliki wa pale.

Sasa niende kwenye ukurasa wa 59 kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi. Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi imefanya kitu kikubwa sana na sina budi kuwapongeza na wanafanyakazi kubwa, na Katibu wa Halmashauri ile ni mtu ambaye ni makini sana tena ni mahiri. *(Makofi)*

Vile vile panapo pazuri hapakosi kasoro. Kwanza kwenye Nyumba za Mchina zilizopo kwenye Soko la Mboga Mboga, pale kuna jaa kubwa na halafu usiku au jioni taka zinachomwa nyuma na kusababisha *air pollution* kubwa na kuleta matatizo makubwa, jioni ukiangalia pale ni hatari tupu.

Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri atuambie jaa lile litaondoshwa lini na moshi ule utakuwa haupo pale, kwa sababu wataalamu wa afya wanasema "*prevention is better than cure*", si hasha watu wa pale wakaanza kuumwa na Kifua Kikuu Mhe. Spika na moshi ni mwingi sana. Kwa hiyo, tunakuomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja atuambie lini atakuja kuliondoa jaa lile au Halmashauri wataliondoa lini.

Katika sehemu za Mwanakwerekwe kuna ucheleweshaji mkubwa sana wa kuzoa taka. Kwa mfano, wanaweza kukaa mwezi mmoja hawajapita na mwisho wa mwezi ukifika wanakuja kudai fedha, na kama hujatoa wanakuletea polisi,

sasa balaa lililotokea pale kama nyumba ile hakuna mtu mzima basi hata mtoto anaweza kuchukuliwa na kupelekwa polisi, na hii ni hasara kubwa Mhe. Spika. *(Makofi)*

Vile vile kwenye ukurasa wa 74 Idara ya Uratibu wa Kazi Maalum. Mhe. Spika, niwapongeze sana watu wa Vikosi vya SMZ, ni hatua kubwa wanachukua tena najua kazi kubwa ambayo wanayoifanya Vikosi vya SMZ. Kwa kweli kama tutathamini sana kazi za Vikosi hivi na kuwatilia bajeti yao vizuri, basi wataweza kudumisha uchumi wetu na kukaa sawa kabisa. *(Makofi)*

Lakini tatizo kubwa ambalo tunalo ni kwamba hatutekelezi kama dhana halisi ya JKU, kwa maana tukisema Jeshi la Kujenga Uchumi, basi lile ni jeshi la kujenga uchumi la kweli. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi mwenyewe nilishawahi kuwa jeshi katika jeshi lile kwa mujibu wa sheria mwaka 1989, na nililima mtama mwingi kule Bambi. Kwa hivyo, najua kama wataingiziwa vizuri bajeti yao na kupewa fedha, basi wataweza kuendeleza hasa na JKU itakuwa ni kweli. *(Makofi)*

Hata hivyo, hivi sasa tunalalamika tu kwamba wizi maidarani heshima haifanyiki, wafanyakazi wote hawafanyi wajibu wao. Mhe. Spika, tuwapeleke kule JKU, basi watafanyakazi vizuri, watapata nidhamu nzuri ya kuweza kufanya kazi. Kwa hivyo, ni vyema tuirudishe sheria na iwe kwa mujibu wa sheria, akimaliza mtu skuli aende kule na kupata kidogo changamoto. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie kuhusu Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Mhe. Spika, tuwapongeze sana kwa kazi kubwa wanazozifanya moto na tunajali sana kazi zao. Lakini Kikosi cha Zimamoto kinakosa vitendea kazi. *(Makofi)*

Kwa mfano, hivi karibuni katika Jimbo langu la Mpendae kwenye Skuli ya *Glorious*, kuna mtu alikuwa akisafisha kisima ni kutumbukia mule na kufariki, lakini ilichukuwa masaa mengi na kikosi kile hakikuweza kufanya kazi mpaka wakaitwa wazamiaji wenyewe wakaja kufunga, na maiti ile ikatoka nje. *(Makofi)*

Sasa ni aibu kwa Kikosi chetu kama hiki kuwa hakina vitendea kazi, na visima vyenyewe tunavyochimba tunataka serikali iwashauri wananchi, aina gani ya visima vichimbwe na tatizo visima vyembamba, mtu anakwenda chini na gesi dakika mbili anarudi mbio juu siwezi, sasa hicho kikao au itakuwa. Kwa hivyo, nasikitika sana Mhe. Spika kuwa Kikosi hiki cha Zimamoto hakina vifaa vya kutosha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimalize kwa sababu najali muda wako na hitimisho langu ni kuhusu Madiwani. Mhe. Spika, Tanzania Bara Madiwani wanalipwa kiasi cha shilingi 160,000/= na safari hii watalipwa shilingi 200,000/=, lakini Waheshimiwa Madiwani wetu wa hapa hawalipwi hata senti 5. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nataka kumwambia Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kama ameshindwa kuwalipa Waheshimiwa Madiwani, basi tuje pamoja kwako lile posho langu la kila siku na kila kikao nitalitoa, ili walipwe Waheshimiwa Madiwani. Kwa kweli Waheshimiwa Madiwani wanafanyakazi kubwa sawa na sisi, serikali imepoteza muda pamoja na fedha nyingi kwa ajili ya kufanya uchaguzi wa Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Sasa namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aje aniambie ni sera gani amefanya au kama hana fedha basi tuje kwako aandike posho langu, na niko tayari kutia saini na wakapewe Madiwani na wagawane kile kidogo watakachokipata. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru sana lakini siungi mkono hotuba hii mpaka nitakapojua hatima ya Jimbo langu la Mpendae na misingi ile niliyopelekewa. Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunakushukuru na sasa nimkaribishe Mhe. Mbarouk Wadi Mussa na baadae Mhe. Bikame Yussuf Hamad.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia fursa hii. Nianze mchango wangu kwenye kitabu hiki ukurasa wa 89, na wala usishituke Mhe. Spika naanzia mbali na baadae nitakuja huko kwenye hitimisho la Mhe. Waziri, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kitabu cha Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ukurasa wa 89 kwenye kifungu 165 kinaeleza hivi:-

> "…Natoa wito kwa wananchi kuendelea kuheshimu sheria za nchi tulizoziweka wenyewe kwa lengo la kujenga mustakbali mwema wa maendeleo ya nchi yetu".

Mhe. Spika, nimeanza huko kwa makusudi, Mhe. Waziri yeye anawataka wananchi waheshimu sheria, sawa kabisa. Lakini na mimi nimtake Mhe. Waziri pia aheshimu sheria, kwa sababu tukiangalia hiki kitabu chake cha mwaka jana na mwaka huu. Kwa kweli mwaka jana kuna mambo mengi alizungumza kwamba atayatekeleza, lakini ukiangalia ule utekelezaji ulivyokwenda na nitatoa mfano mmoja tu ambao wenzangu wengi wameuzungumza hapa. *(Makofi)*

Katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ule mradi wa ujenzi wa *State Lodges* zile, ambapo pale kwa kweli Mhe. Spika matumizi ya fedha ambayo yalifanyika pale hayakuwa yamefuata utaratibu. Mhe. Spika, ndipo pale niliposema kwamba Mhe. Waziri yeye anawahimiza wananchi kufuata sheria, basi na yeye ni vyema kumuhimiza kwa sababu na yeye anasimamia watendaji pale katika wizara yake, kwamba wanakiuka taratibu za matumizi ya fedha. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri na yeye awe katika hilo, na aje atupe kidogo ufafanuzi mzuri juu ya usimamizi wake katika matumizi ya fedha za serikali.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele katika mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Mradi wa Shamba la Mboga Mboga Bambi. Mradi huu Mhe. Spika umeshakuwepo kwa muda mrefu sana nafikiri hivi sasa utakuwa ni mwaka wa tatu kwenye kitabu hiki unaendelea. *(Makofi*

Kwa kweli mradi huu umeshatumia fedha nyingi sana za walipa kodi, lakini tija au faida ya mradi huu mimi bado sijaiona. Kwa mfano, tulikwenda na kamati kule na tukatembelea kwenye mradi huu na tulikuwa na maswali mengi ambayo yalikosa majibu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, atupe kwa kina hasa mradi huu faida gani ambayo sisi au SMZ imepata kwenye mradi huu. Mhe. Spika, jambo la kushangaza ni kwamba hata ile fedha yenyewe inayopatikana na kuuza hicho kidogo kinachouzwa basi inakaa kwenye Ubalozi wa Misri au wale wataalamu wa Misri, na sisi huku tumekuwa kama wasindikizaji tu. Sasa utaona kuna mchango au fedha za walipa kodi zinachukuliwa na kuingizwa pale kwa ajili ya mradi ule, na wala hakuna faida inayopatikana.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho hapa aje atueleze kwa kina hasa juu ya mradi huu, faida ambayo SMZ inapata kwenye mradi huu au ndio tunakwenda kwenye hasara tu kama mambo mengine.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, nisogee mbele kidogo kwenye ukurasa wa 36 kuhusu Jumuia ya Afrika ya Mashariki, na alizungumzia sana Mhe. Mjumbe aliyepita na wala sitaki nilizungumze sana. Mhe. Spika, katika Jumuia kuhusu suala la uanzishwaji wa Taasisi ya Kiswahili katika Afrika ya Mashariki, na Mhe. Mjumbe mwenzangu alilizungumza hilo. Kwa hivyo, atakapokuja Mhe. Waziri atusaidie tu maelezo yake.

Vile vile kwenye ukurasa wa 40 kuhusu Jumuia ya Ukanda wa Bahari ya Hindi. Mhe. Spika, kuna taarifa kwamba Jumuia hii huwa inatoa fedha kwa ajili ya nchi ambazo ziko kwenye ule ukanda.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja atueleze Zanzibar tumefaidika vipi na jumuia hizi juu ya zile fedha zinazotolewa, pamoja na mambo mengine ambayo yanapatikana kwa hizi nchi ambazo ni wanachama wa hii jumuia. *(Makofi)*

Katika hizi Jumuia ya Wazanzibari wanaoishi nje, Jumuia ya Maendeleo ya Kusini mwa Bara la Afrika *SADC*, Zanzibar ilikuwa na nyumba pale *South Africa*. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze nyumba ile sijui ipo na bado inamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi, na kama ipo inafanya kazi gani au ina shughuli gani? *(Makofi)*

Kwa kweli nakwenda haraka ili muda niuwahi vizuri, kwa sababu leo Mhe. Spika umeweka bango la kweli kwenye muda. Mamlaka za Serikali za Mikoa ukurasa wa 45, nianze na Mkoa wa Mjini Magharibi kwenye kitabu chake Mhe. Waziri anatueleza kwamba Mkoa wa Mjini mambo ambayo imekusudia kuyafanya yamo mengi sana, lakini ni kuanza matayarisho ya ujenzi wa jengo jipya la Ofisi za Mkoa liliopo Amani, na kufanya matengenezo ya jengo la Ofisi Mkoa Vuga.

Mhe. Spika, mimi napata shaka kidogo maana ninapopafahamu kama ndipo mkoa inapotaka kujenga lile jengo lao la zamani pale, nadhani kama pale pameshakodishwa tena kuna *Show rooms* za Magari na sijui atajengea wapi Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupe maelezo kwamba zile *Show rooms* za Mkoa wa Mjini au mmekodisha ama ile sehemu imeuzwa, kwa sababu isijekuwa anatupa maneno kwenye vitabu na utekelezaji ndio yale aliyoyasema Mhe. Mohammed Said Mohammed haupo. Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri akaja kutusaidia maelezo kuhusu zile *Show rooms* ambapo yeye Mhe. Waziri anatumbia kwamba anataka kwenda kujenga pale. *(Makofi)*

Nikiendelea sasa niende kwenye Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao ni Mkoa wangu. Mhe. Waziri kwenye kitabu chake ukurasa wa 48 ameeleza kwamba mambo ambayo yanaendelea pamoja na kazi za maendeleo ambazo zitaendelea kufanywa; ni kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Kwa kweli mimi napata shaka kidogo hapa, maana ujenzi huu imekuwa kila siku unaendelea.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze hapa kwamba ujenzi huu utakamilika lini, kwa sababu kila kitabu kinachokuja hapa ujenzi huu umo, sasa ni vyema Mhe. Waziri atuambie ni lini ujenzi huu anategemea ataukamilisha, kwani umekuwa ni mradi endelevu wa ujenzi ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Kutokana na hali hiyo, sijui anataka kutujengea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au kutujengea kasri, kwa sababu haimalizi. *(Makofi)*

Vile vile katika mambo ambayo umeyafanya ni kwamba Mkoa umeshajihisha viongozi na wananchi kujenga jumla ya madarasa 39, na kutoa elimu kwa wazazi jinsi ya kuondoa tatizo la kupasi kwa wanafunzi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze wapi alipokaa na kutoa elimu hiyo kwa wazazi, kama alifanya semina au alikaa kwenye madarasa, naomba aje atueleze vizuri katika hili na mimi ni mzazi lakini naona hujaniita na wala sina taarifa hizo, inawezekana umewaita wenzangu na mimi niko kwenye vikao, lakini ningepata taarifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tukiendelea unasema Mkoa ulisimamia matayarisho ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A Unguja kwa kununua kiwanja na kukisafisha. Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kiwanja cha Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wamekinunua, hivyo nataka kujua wamenunua wapi na kwa nini, kwa sababu kule ardhi ya serikali ipo kubwa sana na wala hatujaitumia kabisa, sasa leo iweje anakanunue kiwanja ama kwa mtu au vipi. Kwa hivyo, nataka ufafanuzi juu ya suala hili. *(Makofi)*

Sambamba na hilo nataka kujua ajira zilizofanyika katika mkoa ule. Kwa mfano, kumefanyika ajira katika kipindi cha miaka kama miwili huko nyuma, na kumekuwa na utata tena kelele kweli, upendeleo, na ajira zote amechukua mtu mmoja. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atuambie wamefanya ajira ngapi pale pamoja na hao walioajiriwa.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele nije kwenye suala la kuendeleza juhudi za kupunguza migogoro ya ardhi kwa kushirikiana na wizara husika, pamoja na wadau wengine zikiwemo Halmashauri za Wilaya na jamii yenyewe. *(Makofi)*

Kwa kweli hapa kuna shughuli Mhe. Waziri kwenye migogoro ya ardhi, na tulizunugmza hapa katika michango yetu wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Lakini hapa anasema kwamba amewakabidhi tena Wakuu wa Mikoa. Mhe. Spika, nataka niseme kwamba baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni tatizo katika hili, mnapowapa mgogoro ukatatuliwe na mwenye mgogoro inakuwa shughuli na wala hautatuliki, hivyo hili litaendelea kuwa tatizo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze vizuri, kwamba ni migogoro mingapi ambayo tayari wameshaitatua ya ardhi na ipo mingapi ambayo bado hamjaitatua na kwa nini? *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika 4.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakubali na ninakwenda haraka kwenye Idara Maalum kwenye ukurasa wa 75 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM). Mhe. Spika, kikosi chetu hiki kwanza nianze kwa kukipongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya, na hata mara hii imeonekana na watu wote ni shahidi kwamba KMKM imefanya kazi nzuri sana ya kuzuia magendo, karafuu kama zilivyovunwa ndivyo zilivyouzwa na kama uchache palipenya kidogo na hilo jambo ambalo litakuwa ni gumu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna tatizo hapa la malimbikizo ya aina mbili katika kikosi hiki, kuna ya wastaafu wa KMKM bado wanadai na wanahangaishwa kila siku hawajapata malipo yao. Vile vile kuna baadhi ya askari wetu wa kikosi hichi wanadai maposho yao bado hawajalipwa. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupe ufafanuzi juu ya masuala haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimalizie kwenye Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ukurasa wa 83. Kwa kweli Kikosi hiki kinafanya kazi kubwa sana, kazi ya kuokoa maisha ya watu na mali zao, kinajitahidi sana. Lakini Mhe. Spika, nikubalinae na Mhe. Mjumbe aliyepita kwamba kikosi hiki kina tatizo kubwa la zana, hakina zana.

Kwa mfano, tuliwahi kuona tatizo moja Mpendae la kuingia mtu kisimani, Mhe. Spika tukio lile lilichukua karibu masaa saba kumtoa ndani ya kisima mpaka kufika juu, tangu alipozama mule mchana ametolewa karibu saa mbili ya usiku na Waheshimiwa Wajumbe kama 5 au 6 tulikwenda pale, kuona wenyewe namna vijana au askari ama makamanda wetu hawa walivyohangaika kutaka kumtoa, lakini wanashindwa kwa sababu hawana zana za kumtolea, wanakwenda mpaka wanamgusa lakini hawezi kuja juu naye, basi ilikuwa shughuli kubwa kweli mpaka tuliwaonea huruma.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwenye bajeti yake hii sikuona ununuzi wa zana kikamilifu sijauona, umo kidogo lakini hajatuchanganulia ni zana gani atakazonunua.

Vile vile suala jengine Mhe. Spika, Zanzibar ni kisiwa kwa hivyo usafiri wetu mwingi tunatumia bahari sisi. Kwa hivyo, sijaona Mhe. Waziri katika bajeti yake namna gani kutakuwa na uokozi wa baharini unapotokea. *(Makofi)*

Kwa kweli tumeshaona mifano hapa Mhe. Spika, lakini leo Kikosi hiki sijaona angalau maombi ya fedha kwamba wanataka kununua boti ndogo tu ya uokozi wa baharini au uzimaji moto wa baharini. Kwa mfano, leo hii na Mwenyezi Mungu aepushie mbali Mhe. Spika kikitoka nje kidogo tu ya kisiwa ukitokezea moto ndani ya chombo kile basi ni hatari, hapa sijaona kabisa katika hili. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja anieleze kwa kina kwa nini hajaweka fungu la ununuzi wa vyombo vya uokozi wa baharini, vyenginevyo bajeti hii Mhe. Spika kuna fungu nataka niliondoshe na baadae tukanunue hicho chombo.

Baada ya kusema hayo, bado sijaunga mkono hoja hii mpaka nipate ufafanuzi wa mambo haya. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa naomba nimkaribishe Mhe. Bikame Yussuf Hamad na baadae Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, ahsante kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu pia kumtakia rehma Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*) kwa kutuwezesha kukutana hapa jioni hii tukiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Spika, nikianza na hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, nianze katika maelezo yake kwenye ukurasa wa 9 kifungu cha 10 Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

“Matayarisho ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, yamezingatia mipango ya kisekta iliyowekwa katika Dira ya 2020 (*Vision* 2020), malengo ya Maendeleo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA II) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi …”

Mhe. Spika, haya ni maneno yaliomo ndani ya kitabu hiki. Lakini mimi nilipoyaona malengo haya ya bajeti hii nilidhani kwamba italenga na kuzingatia kila upande wa maendeleo haya yaliyotajwa humu.

Sasa wakati nilipokisoma hiki kitabu nimeona miradi mingi iliomo ndani ya kitabu hiki ni ya kiserikali tu na wala hakuna miradi inayokwenda kwa wananchi moja kwa moja, kwa ajili ya kuweza kujitafutia riziki kwenye maisha yao. Kwa kweli haya ndio malengo ya vitabu vingi vya Wizara kutuelezea kwamba watazingatia maendeleo ya MKUZA pamoja na mambo mengine.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja aniambie ni eneo gani ambalo kuwa linazungumziwa kwenye kitabu hiki, kama vile kupunguza umasikini au maendeleo ya miradi ya Milenia. Lakini ninachokiona humu ni ujenzi wa sehemu tofauti, ukarabati wa nyumba mbali mbali za Ikulu, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya ndio yaliomo humu mengi, na kwa upande wa miradi ya wananchi sijaiona. Kwa hivyo, pengine ni kutokana na kutokujua tu kusoma pengine hiki kitabu nikakifafanua vizuri.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri aje anieleze MKUZA humu unazungumzia pahali gani au MKUZA ni kujenga hizi Ikulu na haya majumba ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya naona mimi si mwanzo mwaka huu, hii ni Serikali ya awamu ya saba lakini bado leo tunaanza serikali hii ya awamu ya saba tunaambiwa ndio kwanza kunajengwa sasa hivi nyumba za Wakuu wa Mikoa. Sasa mimi nataka niulize niambiwe, hizi nyumba wakishajengewa Wakuu wa Mikoa wakishamaliza ule muda wao zile nyumba huwa ni zao au huwa ni mali ya Serikali. Kwa hivyo hapo Mhe. Spika ninamuomba Mhe. Waziri aje anieleze na mimi nifahamu.

Halafu na mimi niingie katika hii ofisi ya usajili wa kadi za vitambulisho. Mheshimiwa hapa Serikali katika ameandika hapa katika kifungu cha siku imeandaa rasimu ya marekebisho ya sheria ya usajili ya namba hiyo aliyoitaja hapo na inahusu utoaji wa vitambulisho vya wageni wanaoishi nchini. Si vibaya Mheshimiwa kama pana wageni wanaishi katika Zanzibar na wao wakafanyiwa mpango kupatiwa vitambulisho hakuna ubaya wa hilo. Lakini sasa na sisi kuna mambo tuzingatie kuwa bado kuna watoto wetu hawajapata vitambulisho hivi na hawajapata vitambulisho hivi kwa sababu wengine hawana vyeti vya kuzaliwa hilo ni tatizo moja liliopo, hasa vijijini kwetu huko tunakotoka. Wengine hawana uzoefu wa kuwa keshazaa ende akatafute cheti cha kuzaliwa hawana, sasa lakini ni watoto wetu ni Wazanzibari, kwa hivyo tutafute namna ya kuwasaidia.

Kwa sababu kwa mpango uliopo wa kumwambia mtu ende akatafute ushahidi wa mahakamani halafu pale hapewi bure, pale pana karibuni shilingi thalathini na tano elfu hata akikipata kile cheti cha kuzaliwa. Sasa kwa namna hii Mhe. Waziri ungeandaa mpango basi ukawasaidia waliokuwa hawana vyeti vya kuzaliwa, ni sisi kwa sisi hakuna mgeni kwa nini basi hakuna utaratibu wa kuwa angalau hana cheti cha kuzaliwa ende na mama yake akale kiapo ili apewe haki yake ile ya uzanzibari ni haki yake na yeye kwani linashindikana nini Mhe. Waziri tunakuomba hili uliangalie. Tatizo moja ni kuwa watu hawana vyeti vya kuzaliwa na wanaona usumbufu wa kwenda kuwatia vyeti vya kuzaliwa, kwa sababu mwishowe hatima yake atatakiwa pesa hana. Kwa hivyo tunakuomba Mhe. Waziri hilo ulione uwafanyie maarifa watoto wetu ni watoto wetu wenyewe hao.

Jengine niende huu Mkoa wa Kaskazini, Pemba. Mkoa wa Kaskazini Pemba mambo aliyoyafanya kipindi cha bajeti 2012 yameorodheshwa hapa, lakini 2012 hiyo hiyo na hii bajeti ya 2013 yote ni mambo mamoja hakuna geni, ni usimamizi wa amani na mshikamano, wameratibu kusimamia mambo mengine. Lakini 2013 ni hayo hayo kusimamia uratibu na kufanyaje. Sasa Mhe. Spika, badala ya fedha kuidhinishwa Barazani matumizi yake hayapatikani kwa ukamilifu tukaelezwa 2012 kunafanywa hili kwa hali gani sehemu gani. Na 2013 kinaombwa hiki kitafanywa kipi na kipi hiyo hatuoni, bado kuna yale yale yanayofanywa mwaka jana na mwaka huu yafanywe yale yale. Sasa mambo haya mpaka lini siri hizi mpaka lini hebu Mhe. Spika, watueleze mawaziri. Kinachoombewa pesa mwaka jana bajeti ya mara hii ikija tuambiwe kimetumika vipi. Sasa mtu atasema usimamizi tu wa amani, usimamizi wa amani unataka mapesa? Sasa Mhe. Spika, serikali yetu kwa kweli wanatuchanganya wakati mwingine hizi bajeti zao wakiziandika hazina mazingatio maalum.

Mhe. Spika, niende katika mamlaka ya Serikali za mitaa hapa kazungumzia na kawapongeza, kipaumbele katika kukusanya mapato kutoka vyanzo vyao mbali mbali na makadirio ya kukusanya mapato katika Serikali za mitaa kwa kuvuka lengo. Ni kweli Mhe. Spika, lakini hapa nataka nizungumzie kuhusu madiwani. Mhe. Spika, madiwani na wao ni wachaguliwa na Serikali inagharimika kwa kusimamia uchaguzi wa Madiwani. Sasa kwa nini mpaka leo hii Madiwani hawa wameshindwa Serikali kuwafikiria na wao angalau kuwapa chochote. Kwa hivyo tunamuomba Mhe. Waziri na hili alione ili hawa madiwani na wao waweze kufikiriwa japo kwa sababuni.

Mhe. Spika, jengine katika Baraza la Manispaa kifungu (e) limekamilisha kazi za ujenzi wa msingi wenye urefu wa mita mia moja na sitini pamoja na uwekaji wa taa katika eneo la kituo cha biashara Saateni. Mhe. Spika, hawa ni wafanyabiashara wadogo wadogo walioko Saateni na waliondolewa Darajani kwa mikataba maalum pamoja na serikali. Sasa wafanyakazi hawa wana mambo mengi ambayo walikubaliana na Serikali, lakini mpaka leo hii Serikali kupitia waziri bado kashindwa kuwashughulikia wafanya biashara hawa na imeshafika pahali na wao kusema kama hawakutekelezewa yale basi na wao watapata siku warudi Darajani. Na wameondolewa Darajani kwa makubaliano ya kwenda pale watahudumiwa, watajengewa uzio pale Saateni lakini mpaka leo hii Mhe. Waziri kasahau kabisa kuwa na wao ni watu wamekwenda pale kwa mikataba.

Pia kuwawekea pale kituo cha daladala angalau na wao wapate biashara pale, kwa sababu hapana biashara, ukenda wananguka huku na kule. Lakini ukija Darajani watu ni wengi na kuna wafanyabiashara wengine pale pia wametoka kule wamekwenda pale lakini serikali haiwaulizi. Sasa anangojewa yule mnyonge ende pale yeye ende akatimuliwe. Kwa hivyo Mhe. Spika, hawa watu wa Saateni na makubaliano yenu mliokubaliana nakuomba Mheshimiwa uwasikilize.

Mwisho Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri aniambie kuna miradi gani ya maendeleo iliyomalizika na iliyokuwa haijamalizika kwa Wilaya ya Micheweni kwa sababu humu sijaiona, anieleze ni miradi gani ambayo imekamilika na ambayo haijakamilika kwa Wilaya ya Micheweni. Kwa sababu kipindi kilichopita cha bajeti kuna fungu nililiuliza lakini akanambia Mheshimiwa kuna miradi tele ambayo itakwenda katika Wilaya ya Micheweni. Sasa naomba humu mimi ninaitafuta sijaiona lakini aje aniambie Mhe. Waziri ni mradi gani unaopelekwa kule kwa Wilaya ile ya Micheweni hasa ukizingatia na hali za Wilaya ile ilivyo.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, ninasubiri Mhe. Waziri aje anieleze na mimi yangu nije nimuunge mkono hoja yake. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nichukuwe nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaaliwa hapa kukutana jioni ya leo. Lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Afisi Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Awali ya yote nichukuwe nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa kitabu hiki ambacho kama kitatekelezwa kama kilivyoandikwa basi ninaamini kwamba nchi yetu itapiga hatua.
Baada ya pongezi hizo Mhe. Spika, niingie katika ukurasa wa 20 wa kitabu hiki. Mhe. Waziri ametwambia kwamba katika mradi wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ikulu na nyumba za Serikali, Mhe. Spika, lakini katika kitabu hiki sijaona ukarabati wa Ikulu ndogo ya Fumba, ninaamini kwamba Mhe. Waziri na sote tunafahamu kwamba lengo la kuwepo Ikulu hizi ndogo ili kumpa nafasi Mhe. Rais na kwa kutambua kwamba Mhe. Rais ana kazi nyingi na majukumu mengi basi zimejengwa Ikulu hizi ndogo ili aweze kupumzika. Lakini kwa masikitiko makubwa sijaona ukarabati wa Ikulu hii ya Fumba.

Mhe. Spika, sote tunafahamu kwamba Ikulu ya Fumba imeshaanza ukuta wake kuliwa na bahari na siku za nyuma tuliona kwamba Serikali ilianza kufanya ukarabati lakini kwa bahati mbaya naona ukarabati ule umesita. Sasa ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie labda sababu gani ambazo zimepelekea Ikulu ya Fumba kusitishwa kufanyiwa ukarabati.

Baada ya hayo Mhe. Spika, niendelee katika ukurasa wa 44 wa kitabu hiki na Mhe. Waziri alitwambia hapa kwamba anategemea kufanya ubunifu wa *structural design* na tathmini ya gharama za ujenzi wa utanuzi wa ukuta wa pwani ya Forodhani wenye urefu wa mita 340 kwa ajili ya matayarisho ya vitabu vya zabuni ya kumtafuta mkandarasi. Sasa Mhe. Spika, ninavyofahamu mimi au ninavyokumbuka mimi kwamba mradi huu ulikuwa unakwenda sambamba na mradi wa ujenzi wa bustani ya Forodhani, nichukue nafasi hii kwanza wenzetu wa *Agakhan*

Foundation niwape pongezi kwa kututengenezea bustani hii ya Forodhani na imetuwezesha wananchi wetu kwenda kupumzika.

Sasa nilichokusudia kusema kwamba mkataba uliokuwa wa ujenzi wa bustani ya Forodhani ulienda sambamba na ujenzi wa ukuta huu wa pwani ya Forodhani. Lakini leo katika kitabu hiki anatwambia kwamba anafanya tathmini ya gharama ya ujenzi wa utanuzi wa ukuta wa pwani ya Forodhani. Sasa mimi nilikuwa naomba aje kutueleza Mhe. Waziri kwamba je mkataba ule ambao walitiliana mkataba Serikali na *Agakhan Foundation* je umekatishwa? Na kama umekatishwa sababu gani ambazo zimepelekea mkataba ule kukatishwa na kama mkataba ule umekatishwa utaratibu gani wa ukatishaji wa mkataba unakuwa unafanyika.

Lakini jengine ninavyokumbuka pia kwamba mkataba ule ulikuwa tayari umeonesha kwamba *structure* wale wenzetu wa Agakhan walikuwa wameshatayarisha. Sasa inaonekana hapa itakuwa kuna marejeo kwamba wenzetu wa agakhan foundation tayari walikuwa wameshatayarisha makisio haya, lakini na serikali nayo ina mpango wa kutayarisha gharama hizi. Pia wametueleza kwamba Mhe. Waziri kwamba utatafuta mkandarasi wa ujenzi. Sasa sijui *which is which* kwa hivyo naomba Mhe. Waziri uje kunieleza vizuri nifahamu.

Lakini nikiendelea nina mchango wangu nije katika Mabaraza haya yetu ya mji. Mimi niungane na Mhe. Subeit kuipongeza halmashauri yetu hii ya Micheweni kwa ukusanyaji mkubwa wa mapato. Mhe. Spika, sisi tunafahamu kwamba Wilaya ya Micheweni ni Wilaya ya mwisho, lakini ni Wilaya ambayo imejitahidi kukusanya mapato na tunaamini kwamba ina vyanzo vichache vya ukusanyaji wa mapato lakini pamoja na hayo basi imejitahidi kukusanya mapato ukilinganisha na mabaraza mengine ya mji.

Kwa mfano Baraza la Mji la Wete, imeonesha kwenye kitabu hiki kwamba imekusanya milioni arubaini na nane, lakini ukiangalia uhalisia kwamba Baraza la Mji la Wete ni Baraza mama na ni Baraza ambalo watu wapo active kwa biashara. Lakini ukitizama kwa undani zaidi unakuta limepitwa na halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Sasa Mhe. Waziri naomba basi utapokuja kufanya majumuisho utueleze sababu gani zilizopelekea kuwa mabaraza haya mengine yamekusanya pesa kidogo ukilinganisha na halmashauri hii ya Wilaya ya Micheweni. Lakini pia mimi nina wasiwasi kwamba aidha kwenye ukusanyaji kwenye maeneo haya hayakusanywi ipasavyo, baadhi ya maeneo yanaachiwa. Lakini pia inawezekana kuna matatizo ya udhibiti wa mapato kwamba mapato hayafiki pale yanapostahiki. Sasa ninamuomba Mhe. Waziri basi ajitahidi kutayarisha mpango madhubuti kuhakikisha kwamba mapato haya hayapenyi lakini pia yanadhibitiwa ipasavyo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 59, halmashauri ya Wilaya ya Magharibi. Mimi nichukue nafasi hii kupongeza wananchi wa Wilaya ya Magharibi kwa kuitikia wito wa kuchangia ukusanyaji wa taka hasa katika maeneo ambayo yamepimwa. Wananchi kwa kweli wameitikia wito na ninaamini kwamba inaingiza mapato katika serikali yetu mapato mengi. Lakini cha kusikitisha inaonekana kwamba halmashauri yetu ya Wilaya ya Magharibi bado haijapanga mipango yao ya kukusanya taka.

Na hii inaonesha kwamba labda nitoe mfano katika eneo la Mwanakwerekwe sasa hivi utakuta kama utakwenda pale utakuta taka zote zinazokusanywa katika majumba basi zinafanywa dampo ambayo dampo yenyewe inaekwa kati kati ya njia katika ofisi za Muslim Agency. Lakini jengine la kusikitisha zaidi taka zile zinapozidi wenzetu hawa halmashauri wanazichoma moto sasa hii ni mbaya zaidi kwa sababu inapelekea *pollution*, lakini pia inahatarisha afya za wananchi ambao wanakaa katika maeneo yale ya Mwanakwerekwe.

Sasa mimi ninamuomba Mhe. Waziri akishirikiana na taasisi yake, kwanza damp ile pale iondoshwe haistahili kuwepo katika eneo lile kwa sababu inapelekea usumbufu ya watu ambao wanapita kwa miguu, lakini jengine inapelekea usumbufu kwa watu wenye vyombo. Sasa hivi hata kama magari yakipita basi inaponyesha mvua taka zile zinakuwa uchafu, tope na gari kukwama. Kwa hivyo ninamumba Mhe. Waziri aliangalie hilo na ninaamini kwamba kwa kuwa Waziri wetu huyu ni msikivu wiki hii hii anaweza akafanya maarifa damp ile ikaondoshwa.

Lakini jengine Mhe. Spika, na Mhe. Waziri huu utaratibu wa kuweka madamp katika miji mimi nadhani si utaratibu mzuri. Taka tunapozikusanya basi tuzipeleke nje ya miji ili kuweka usalama wa wananchi wetu.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu mimi nivipongeze vikosi vyetu hivi vya Zimamoto, wenzangu wengi wamepongeza kwa kweli vikosi hivi vinafanya kazi vizuri lakini nirejee kusema kama walivyosema wenzangu kwamba vikosi hivi vya Zimamoto kwa kweli havina vyombo vya kisasa na tunaona

kwamba hata ilipotokea ajali ile ya MV Spice, wenzetu wa zimamoto walienda lakini walishindwa kutambua wapi imezama mpaka ikapelekea wenzetu wa Tanzania Bara wakaja na helkopta ndipo walipotambua meli wapi imezama na maiti ziko wapi. Kwa hivyo Mhe. Waziri ninakuomba hawa wenzetu wa vikosi vya Zimamoto kwa kweli wapo tayari kuwatumikia wananchi lakini utayari ule hauwezi ukapatikana lengo kama hawana vyombo vya kisasa.

Nikiendelea na mchango wangu nije katika hili soko la Mwanakwerekwe. Mhe. Waziri ametwambia hapa katika kitabu chake cha bajeti, amefanya ukarabati wa masoko haya, mimi nimpongeze na ninamuomba aendelee kufanya ukarabati katika masoko yetu haya. Lakini Mhe. Spika, la kusikitisha kwamba soko letu hili la Mwanakwerekwe sasa hivi linaonekana kwamba limeshazidiwa na wafanyabiashara. Na hii inapelekea wafanyabiashara kuuza bidhaa zao mpaka barabarani na inapelekea usumbufu kwa madereva. Lakini si hilo pia usumbufu mkubwa inapelekea wale ambao wanaenda kununua biashara zile ndani, kwa sababu hata zile njia ambazo wateja wanapita kwenda kujitafutia bidhaa wamekuwa hawana nafasi ya kupita kutokana na kuzidiwa na wafanya biashara hao.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri kama kutakuwa na uwezekano basi wale wafanyabiashara wahamishiwe katika soko la mboga mboga, kwa sababu soko la mboga mboga limejengwa kwa gharama kubwa na wenzetu hawa wa China wametumia fedha nyingi, lakini hatimae unakuta lile soko la mbogamboga liko tupu. Lakini wafanyabiashara utakuta wamejikusanya katika soko hili la Mwanakwerekwe. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri aliangalie hili lakini pia kwa usalama wafanya biashara wetu, kama linatokea janga pale kwa kweli itakuwa hatari kubwa.

Baada ya hayo Mhe. Spika, na kwa kuthamini muda wako niseme kwamba naunga mkono hoja hii ya Waziri asilimia 99. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima jioni hii tukiendelea kujadili bajeti hii ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Lakini pia nikushukuru na wewe kwa kuniona na kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu.

Mhe. Spika, nikiingia katika bajeti hii kwanza nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Rais wetu Dr. Ali Mohammed Shein. Mhe. Spika, kama kuna kipindi kinahitaji Rais wa aina ya Dr. Shein basi ni kipindi hiki. Ni Rais muungwana, ni Rais msikivu lakini pia ni mtu msafi. Lakini kubwa kuliko lote amebeba ile roho ya maridhiano ambayo ilikuwa ndio msingi wa serikali ya umoja wa kitaifa iliyoundwa baada ya uchaguzi.

Mhe. Spika, kuingia katika mfumo huu mpya ilikuwa ni majaribu makubwa yalikuwa yanahitaji nahodha mzuri anayeweza kuyakabili barabara maji kama ya Zanzibar ambayo yamejaa misuko suko ya kisiasa katika historia yake. Lakini leo nathubutu kusema Dr. Shein kwa kiasi kikubwa ametudhihirishia kwamba anao uwezo huo na karibuni kabisa alidhihirisha hili katika matokeo yaliyotokezea na akaweza kutumia uungwana na ustahmilivu wa hali ya juu Zanzibar ikavuka tena mtihani ule tukiwa katika hali ya amani na utulivu ninampongeza na ninamshukuru sana.

Lakini Mhe. Spika, sitoacha siku zote waswahili wanasema ulianza ufizi ndio yakaja meno, sitoacha kumpongeza na kumshukuru Rais mstaafu Rais Aman Abeid Karume. Ni yeye akishirikiana na Katibu Mkuu wa CUF ndio waliojenga msingi wa maridhiano hayo. Lakini mimi ninaamini hata kama Maalim Seif angetaka ingekuwa yule mwenye dhamana ya uongozi wa nchi hakutoa ushirikiano basi yasinge kuwa haya. Kwa hivyo bado pongezi kubwa ninampa Rais mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo na shukurani niseme pamoja na kumsifu Dr. Shein mimi ninasikitika sana na Waziri wetu Dr. Mwinyihaji Makame na timu yake kwamba wanamuangusha Rais. Yeye ni mtu safi lakini ofisi yake inayobeba majukumu makubwa sana watendaji wamekuwa hamsaidii Mhe. Spika.

Mhe. Spika, wajumbe wengi wamechangia hapa wamesema ukiangalia mambo ambayo yamo katika hotuba hii Mhe. Spika, mengi yanajirejea yale yale ya mwaka jana. Ukitizama miradi iliyopangwa na shughuli zilizopangwa kufanyika, kwa mfano ukiangalia ukurasa wa 9 wa kitabu hiki halafu ukalinganisha na mambo ambayo yanayokusudiwa kufanywa mwaka huu katika ukurasa wa kumi na yakajirejea katika ukurasa wa 22 na 23 ni hayo kwa hayo maji ya futi na nyayo Mhe. Spika. Ningewambia wajumbe hata wangeangalia hotuba ya mwaka jana hakuna tofauti. Sasa haya Mhe. Spika, yanasikitisha sana kusema kweli tunamuangusha Rais.

Lakini vile vile Mhe. Spika, katika kitabu hiki tumeambiwa kwamba Rais amekuwa akifanya ziara katika maeneo mbali mbali kufuatilia utendaji tunampongeza. Lakini imesikitisha katika ziara anazozifanya tumegundua kuna baadhi ya watendaji na viongozi wakubwa kabisa wa Wizara wengine na Ofisi za Mikoa wamekuwa wakimdanganya Rais. Alipokuwa Mkoa wa Kusini Unguja ilikuwa ni kashfa Mhe. Spika, alipokataa na akasema hadharani baadhi ya taarifa alizopewa kwa sababu zilikuwa hazielezi ukweli wa mambo. Kwa hivyo nasema tabia hiyo watendaji wetu wanapaswa waiache kabisa.

Mhe. Spika, nisije nikasahasu kabla kuingia undani wa baadhi ya mambo ninayotaka kuyazungumza naomba vile vile Waziri akija mimi kwanza anisaidie katika baadhi ya mafungu ambayo yamo katika sehemu mbali mbali. Nikitaja moja moja nitachukua muda mrefu, lakini sehemu mbali mbali ya Wizara wenyewe na ofisi nyengine zinazosimamia kuna mafungu ambayo yanatutia mashaka makubwa na hili naomba pia Waziri wa Nchi anayeshughulikia fedha akumbuke maneno yangu niliyoyazungumza wakati ninachangia bajeti kubwa kwamba kuna maeneo ambayo bado yakitizamwa vyanzo vingi vya mapato Mhe. Spika, vinachezewa.

Bajeti za umeme, bajeti za ada ya ushauri, bajeti ya ununuzi wa televisheni katika kila ofisi unakuta televisheni imenunuliwa kwa shilingi milioni arubaini ninajiuliza televisheni gani inayonunuliwa kwa shilingi milioni arubaini Mhe. Spika. Na huwezi ukanambia kama kwa kutumia Wizara nzima kwa sababu kila section kuna manunuzi ya televisheni milioni arubaini, milioni ishirini na tano. Ninajiuliza kuna nini hapo Mhe. Spika, mbali za viburudishaji zimepanda katika kila sehemu. Safari za ndani na nje huduma za mitandao Mhe. Spika, hatutambui kama zimepanda na sote tunatumia mitandao lakini utakuta bajeti imepanda kiasi kikubwa sana ukilinganisha mwaka jana na mwaka huu.

Lakini kali ya mwaka Mhe. Spika, kuna bajeti katika Afisi ya Baraza la Mapinduzi sekreteriet kwenye vifaa vidogo vidogo unakuta pametengwa shilingi ishirini na tatu milioni, unajiuliza kunanuliwa vifaa gani vidogo vidogo kuwa sekreteriet ya Baraza la Mapinduzi ambayo ipo pale kasri ya wananchi People Palace kwamba inahitajika milioni ishirini na tatu. Matengenezo ya majengo Mhe. Spika, na maeneo mengine kuna eneo kwa mfano katika Mkoa wa Kusini Pemba ununuzi wa kanda umeandikwa shilingi milioni saba nukta nane. Ninajiuliza kanda gani na CD gani zinazotaka kutumiwa kwa mwaka mzima zikagharimu shilingi milioni saba nukta nane. Haya ni maeneo Mhe. Spika, naomba akija Waziri anisaidie maelezo.

Lakini vile vile Mhe. Spika, eneo jengine ambalo limenishtua na ninamuomba Waziri akija anipe maelezo ni eneo linalohusu vikosi katika bajeti ya chakula. Katika hotuba yake Mhe. Waziri alitwambia kwamba kwenye vyuo vya mafunzo kuna wafungwa sisi tunawaita wanafunzi, tumeambiwa kwamba kuna ongeza milo kwa hivyo kukiongezeka chakula ninaelewa. Lakini ninapolinganisha bajeti ya mafunzo imepanda chini ya mara mbili lakini bajeti ya vikosi vyengine vimepanda kwa kiasi kikubwa sana naomba nitoe mifano haraka haraka ili nirudi katika maelezo yangu.

Ninaomba Mhe. Spika, Waziri aangalie katika kikosi cha JKU ukurasa wa 191 wa hili buku kubwa. Mhe. Spika, bajeti ya chakula kwa mwaka jana ilikuwa milioni thalathini na nane kwa mwaka huu ni milioni mia tatu na thamanini elfu asilimia elfu moja imepanda. Najiuliza pana nini hapa, Mhe. Spika, kwenye Mafunzo kama nilivyosema ukiangalia ukurasa 195 imepanda kutoka milioni mia nne laki nne tisiini elfu hadi mia saba na hamsini milioni. Hapa naweza kuelewa kwa sababu tumeambiwa kunataka kuongezwa milo mitatu kwa wafungwa na askari wanaowahudumia. Lakini ukiangalia KMKM kwenye ukurasa wa 483 Mhe. Spika, unakuta bajeti ya chakula imepanda kutoka shilingi 15 milioni mwaka jana hadi shilingi 365 milioni mwaka huu.

Mhe. Spika, kwenye Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ukurasa wa 500 wa buku hili kubwa la gharama bajeti yake imepanda kutoka shilingi 4,100,000/- hadi 90 milioni mwaka huu wa fedha.

Na mwisho KVZ Mhe. Spika, katika ukurasa wa 518 bajeti ya chakula imepanda kutoka shilingi 20 milioni hadi 192 milioni. Naomba hayo Mhe. Waziri akija anisaidie maelezo ya kina kabisa kwamba kwa nini vikosi vyengine bajeti ya chakula ipande kwa kiasi kikubwa kama hiki. Kwa sababu katika bajeti yake hakutwambia, hakuna maelezo ya kwamba kwa nini bajeti ya chakula ipande kiasi kikubwa kama hiki, tunataka tuelezwe kuna nini hapa.

Vile vile katika mafungu Mhe. Spika, la mwisho nimalizie ni katika Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Mhe. Spika, katika buku hili kubwa kwanza kuna ada ya mikataba shilingi milioni mia tatu thalathini na saba elfu na laki

tano. Nimeangalia katika hotuba ya bajeti kama kuna maelezo yoyote ada hii ya mikataba ni ya nini hakuna maelezo katika sehemu ya Idara ya Vitambulisho na Kadi za Mzanzibari.

Lakini vile vile katika maelezo ya Waziri ya hotuba yake hakukuwa na maelezo yoyote katika ofisi hii kuhusiana na ujenzi mkubwa, lakini bado katika bajeti ya matengenezo ya ofisi kuna shilingi 80 milioni zimetengwa kwa ajili ya matengenezo makubwa ya majengo. Najiuliza jengo hilo lililokaa pale fedha hizi zinakwenda wapi. Hayo Mhe. Spika, naomba akija Mhe. Waziri atupe maelezo ya kina kabisa ikiwa kweli anataka bajeti hii tumpitishie hapa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba pia nitoe *concern* moja ya jumla kwenye vikosi, kwamba tumezowea katika bajeti zote kunakuwa na bajeti ya Utawala Unguja na Utawala Pemba, lakini bajeti za vikosi hazioneshi hivyo. Sasa mara nyingi ukienda Pemba ukikutana nao wanalalamika kwamba wao wanasahauliwa, wameachwa mkiani mpaka kinachobakia ndio wasogezewe wao, huduma ziko mbaya sana. Sasa kwa nini kama utaratibu wa serikali kwa kila wizara na idara yake kuna matumizi Unguja na Pemba kwa nini kwenye vikosi fungu lote linabakia Unguja halafu inaachwa juu ya rehema ya wakubwa wao kuwaamulia kifungu gani kiende kule. Hili pia naomba akija tupate maelezo.

Mhe. Spika, muda uliotupangia leo ni mchache inabidi twende haraka haraka. Naomba niende katika Idara hii ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Rashid Seif asubuhi alizungumza hapa, kwamba ukitizama hotuba inasema mwaka jana wameandikishwa watu 10,578, mwaka huu wa fedha wanakadiriwa kuandikishwa watu 10,500 na mimi naomba akija anisaidie maelezo kwamba hivi wastani huu unatokana na kigezo gani, ndio ukuaji wa watu waliofikia umri wa miaka 18 kila mwaka. Katika hili Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tuwe makini sana, inawezekana wewe katika eneo lako ukasema hujapata malalamiko kwa sababu huko pengine watu wote wamepewa na wakiwa wamepewa Mhe. Spika hatolalamika atayelalamika ni yule ambaye hapewi. Wanasema Waswahili "Kitanda usichokilalia hukijui kunguni wake". Sasa Mhe. Spika, wanaolalamika hivi ni watu ambao wanakoseshwa haki zao na wakikoseshwa wanakosa haki nyingi kama ilivyosemwa kuwa si habari ya uchaguzi tu, lakini kila jambo katika nchi yetu ni lazima upate kitambulisho cha Mzanzibari.

Mhe. Spika, lakini la kusikitisha zaidi ni kwamba wakati Wazanzibari hatuwapi wasiokuwa wazanzibari wanapewa, Mhe. Makame Mshimba kikao kilichopita alikuja hapa akaleta ushahidi wa Wakenya ambao wamepewa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Leo Mhe. Spika, mimi nimemletea Mhe. Waziri *sample* mbili tu hapa za watu wawili, bahati nzuri hawa ni raia wa Msumbiji na bahati nzuri Mhe. Spika, nimepata bahati ya kupata vitambulisho vyao vya Mzanzibari na Kitambulisho chao cha Msumbiji hiki hapa. Mmoja anaitwa Semi Pajume Matete na picha yake ipo halafu huyu huyu kapewa kitambulisho cha Uraia wa Msumbiji na mpaka *Passport No*. ya Msumbiji ndani yake imeandikwa, tutasemaje hakuna matatizo katika suala hili Mhe. Spika.

Mwengine anaitwa Pius Edward Pius na yeye vile vile Mhe. Spika, nitakuwa na wewe uzione baadae umpe Mhe. Waziri, kapewa cha Mzanziabari na chake cha Msumbiji hiki hapa kapewa kuna nambari yake ya *passport* ya Msumbiji. Sasa kuna Wakenya, Wamsumbiji, lakini Wazanzibari hawapewi.

Mhe. Spika, ushahidi mwengine ni huu hapa, leo Sheha wa Nungwi anamuandikia mhusika na baadae inapelekwa Polisi anatoa ushahidi kupeleka barua ya tarehe 10/12/2011 inakwenda kwa Mkuu wa Vitambulisho, Uraia na Ukaazi wa Mzanzibari Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, inaambiwa mhusika kupotelewa na kitambulisho cha Uraia na Ukaazi wa Mzanzibari Samiti Mirakwa Mesaleo, 23 Mmasai wa Nungwi, anathibitishiwa kwamba kapotelewa na kitambulisho chake apewe kitambulisho chengine cha Mzanzibari. Sasa tukisema haya tunasema kwa ushahidi, wasiokuwa Wazanzibari wanapewa na Wazanzibari wananyimwa haki zao katika nchi yao, iko siku Mhe. Spika, tutakuja kutaka kufanya maamuzi muhimu kuhusu nchi yetu hapa tutakuja kulia kilio cha mbwa mdomo juu kwa sababu itakuwa tumewapa haki waliokuwa sio.

Mhe. Spika, hii hapa mifano tele ya watu ambao wamefika mpaka Mahakamani wamepewa mpaka hati za viapo lakini wanahangaishwa kupewa vitambulisho vya Mzanzibari, wametimiza masharti yote, sio walionyimwa vyeti vya kuzaliwa wala sio waliokosa hati za viapo Mahakamani, wanapata vyote lakini bado wakifika kwa masheha wanapata usumbufu katika kupata vitambulisho. Waliokuwa wanavipata washukuru Mungu kwamba wao ni daraja 'A' katika nchi hii, lakini wako daraja 'B' Mheshimiwa bado wanasumbuliwa wakati wao ni raia wa nchi hii kama walivyokuwa watu wengine. Mhe. Spika, naomba hili akija waziri anipe maelezo ya kutosha la si hivyo nitaizuia bajeti ya Ofisi ya Vitambulisho vya Mzanzibari kwa sababu haiwatendei haki Wazanzibari inawabagua na katiba yetu imekataza ubaguzi.

Mhe. Spika, naomba vile vile haraka haraka niende katika vikosi. Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kuvipongeza sana Vikosi vya SMZ kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mhe. Spika, kwa Mzanzibari mzalendo kama mimi Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndio fahari ya Uzanzibari wangu. Hivi ni vyetu na Mzee Abeid Amani Karume alitwambia, 'Tukuza kilicho chako mpaka usahau cha mwenzako'. Kwa hivyo, mimi najinasibu navyo hivi ni vikosi vya Wazanzibari kama kuna matatizo ya kiutekelezaji ni kawaida tutarekebisha. Lakini katika hayo nilikuwa naomba Wakuu wa Vikosi vyangu hivi na wapo juu pale tunasema haya kwa nia njema kwamba yarekebishwe na ndio maana ya chombo hiki cha wananchi Mhe. Spika. Askari wao wanapenda kuwaita wapiganaji wanasikitika sana Mhe. Spika, kwamba kuna taratibu nyingi zinakiukwa kwa sababu tu ya kutumia ile nidhamu ya kijeshi wanashindwa kuyasema wao. Sasa naomba Mhe. Waziri atusaidie.

Kuna wafanyakazi Mhe. Spika, wanasema mpaka sasa hivi wengi hawajasajiliwa katika *ZSSF*, kwa hivyo watapostaafu hawa hawajui vipi watapata haki zao, lakini hakuna mfuko mbadala kwa ajili ya vikosi. Huko nyuma pengine kwa sababu ya siasa chafu ilikuwa kuna hofu kwamba akienda kule zitatoka siri za kujulikana askari wako wangapi, lakini sasa katika hali mpya ya siasa hii Mhe. Spika, hakuna sababu kwa nini askari hawa wasiwekewe fungu lao ili watapostaafu na wao wakajijua wanastaafu vipi.

Vile vile Mhe. Spika, kuna mikato mingi imetajwa hapa sina haja ya kurejea, lakini utastaajabu Mhe. Spika, unamkata askari kwa mfano sehemu ya pato lake kwa michezo lakini katika bajeti unakuta kuna fungu limetengwa kwa ajili ya kuhudumia timu za michezo za vikosi. Sasa kwa nini wakatwe maaskari hawa.

Lakini vile vile Mhe. Spika, wanaambiwa hawa linapotakiwa kujengwa jengo lolote la vikosi vyao wachangie, huku tukija katika bajeti kunatengwa bajeti ya kujenga majengo hayo. Kwa nini wanakatwa askari hawa. Mhe. Spika, kunapojengwa majengo kumekuwa na utaratibu hakutangazwi *tender* katika vikosi vya SMZ badala yake wanatumika kujenga na wengine tumepiga kelele mara nyingi wasajiliwe basi ziwe ni kampuni za ujenzi ili zipate kufanya taratibu za ukandarasi halifanywi hilo Mhe. Spika, tunapewa ahadi kila siku lakini halitekelezwi.

Mhe. Spika, wanapopewa uhamisho hakuna posho la uhamisho ambalo wanapewa. Tuliwahi kutembelea Pemba kule hali wanayoishi ni ngumu sana askari, hasa tulichowahi kutembelea ni Kikosi cha Mafunzo. Kwa hivyo, nilikuwa naomba haya yatizamwe sana.

Jengine la mwisho katika suala la vikosi Mhe. Spika, ni suala zima wanapopewa mishahara yao, unaambiwa kwa mfano katika Kikosi cha Mafunzo wanakatwa shilingi elfu elfu wanaambiwa hii ni *bank charges*. Sasa *bank charges* kwa nini akatwe askari ambaye anapokea mshahara wake, haya ni mambo ambayo yanahitaji majibu kama nilivyosema tunawapenda wakuu wa vikosi vyetu tunaamini wanafanya kazi kubwa ya kutulinda tunapokuwa tumelala, lakini hiyo Mhe. Spika, isiwe sababu ya kutokuwajibika katika maeneo mengine ya uwazi.

Mhe. Spika, maelezo mengine kwa haraka wamezunguzma wenzangu hapa kwamba kuna maeneo ambayo yanatia mashaka. Mhe. Omar Ali Shehe amezungumza asubuhi na mimi naomba nimuunge mkono, kwamba kuna hii sera ya Serikali za Mitaa mageuzi yake, kila mwaka ikija inaambiwa fedha inapitishiwa lakini haimaliziki na mimi nasema kama sijapata maelezo fungu hili la shilingi 150 milioni kwa kuendeleza sera za serikali za mitaa nitalikataa sitolipitisha mpaka nipate maelezo ya kina.

Lakini vile vile wawakilishi wengi hapa wamehoji uhalali wa kuendelea na *GSO*. Mimi Mhe. Spika, nasema *GSO* iendelee, tatizo letu ni kwamba kazi walizokuwa wakizifanya huko nyuma zilikuwa zinaingiza mambo ya kisiasa, lakini bado inafanya kazi, hapa hata nje tukiingia wanaofanya kazi ile ni *GSO*. Lakini pia nataka niwatetee Mhe. Spika, unawakuta wanafanya kazi katika hali ngumu hata usafiri hawana, wakija hapa watu kama wale usalama wa taifa ni watu wenye hadhi yao wanaomba *lift* kwa Waheshimiwa Wawakilishi haipendezi, sijui hata kama posho zao wanapewa, tunajua ni watumishi wa Serikali ya Muungano lakini wanapokuwa hapa pia wanatutumikia kama Wazanzibari tutizame njia ya kuwatunza.

Mhe. Spika, niende katika suala la *ZUSP*. Mradi huu wa *ZUSP* Mhe. Spika, mwaka jana tulitajiwa ukawa na malengo makubwa makubwa, mwaka huu hauna maelezo kwa sababu hakuna kilichofanyika Mhe. Spika. Mwaka mzima uliopita tunachotizama katika magazeti ni matangazo ya *tender* yasiyomalizika ya kutafuta huduma lakini hakuna hata kimoja kilichofanyika. Na niliipeleleza Bajeti Kuu ya Serikali iliposomwa mara hii haikugusa *ZUSP*

tofauti na Bajeti Kuu ya mwaka jana kwa sababu hakuna kilichofanyika. Kwa hivyo, ndio pale niliposema Mhe. Waziri na watendaji wake wanamuangusha Mhe. Rais.

Mhe. Spika, mambo ya uchafu, ya wanyama kuendelea kuzagaa mitaani yameshazungumzwa yote sina haja ya kurejea tutakuja kubana tupate maelezo katika kupitishwa vifungu, lakini nimalizie la mwisho kabisa Mhe. Spika, moja.

Mhe. Spika, nimeanza kwa kumpongeza Mhe. Rais naendelea kumpongeza lakini niseme Wazanzibari tumefika pahala na nalisema hili katika ofisi hii kwa sababu hii ndio ofisi ya Kiongozi wetu wa juu na Rais wa nchi Mhe. Spika, ndiye *symbol* ya nchi, ndio alama ya utambulisho wa nchi, tumefika pahala haturidhiki Rais wetu kuwa hatambuliwi kwa heshima yake kama Rais kimataifa. Kwa hivyo, nataka kuwaomba Wazanzibari sana katika marekebisho yanayokuja walitizame hili, tuliposema mambo ya nje yaondolewe katika mambo ya Muungano tunataka Rais wetu wa Zanzibar anapotoka nje mpaka Tanzania atambuliwe Rais wa dola huru ile mipaka yake yenye heshima yake kitaifa na kimataifa ili Zanzibar kweli itambuliwe na kusimamia hadhi yake.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nitaiunga mkono bajeti lakini baada ya kupata maelezo ya kina juu ya hoja hizi, na mimi naamini waziri akitaka anaweza. Jana alipojuwa kuna bajeti yake leo kaweza kuondosha maguzo pale Forodhani. Kwa hivyo, kumbe akitaka akiamua anaweza na haya atoe maelezo tuone utendaji unabadilika ili tupitishe bajeti yake la si hivyo Mhe. Spika, patakuwa na mbinde hapa. Ahsante sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, kwa kuanza mimi nitaanza ukurasa wa 81 ambao unazungumzia Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusu nyumba za kulala askari, nasema hivi na sijui kwa sababu ile hoja aliyoisema Mhe. Ismail Jussa kuwa utawala Unguja inawasahau sana wenzao kule Pemba. Sisi kama kamati tuliwahi kupitia katika nyumba hizo za maaskari Pemba, lakini kwa kweli hali tuliyoikuta kule sio nzuri nyumba moja inakaa familia tatu na wenyewe pia wana watoto wanne mpaka watano lakini chumba ni kimoja tu wanachotumia. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba hili alitizame kwa sababu hii sio haki, muwaboreshee maisha ili na wao wawatizame vizuri wale wanafunzi wao.

Mhe. Spika, nikiendelea nije hapo hapo Chuo cha Mafunzo lakini katika ujenzi wa majengo ya Chuo kipya cha Mafunzo Hanyegwamchana. Mhe. Spika, tunasikia kwamba lile eneo ambalo linataka kujengwa hiki chuo kumetokea mgogoro kuna wananchi wametokea wanasema kuna baadhi ya maeneo ni ya kwao. Mhe. Waziri namuomba akija atufafanulie kwamba hili tatizo limefikia wapi, kumekuwa na muwafaka isije ikawa kimeshajengwa chuo kuna wananchi wanataka kulipwa pesa zao kwa kuondolewa katika eneo.

Lakini la pili Mhe. Spika, katika hili kuna tetesi sijui kama ni kweli au vipi, lakini Mhe. Waziri nimuombe akija atutolee ufafanuzi. Tunasikia kwamba kuna wajanja wameanza kuzila hizi pesa za ujenzi wa chuo. Kwa hivyo, mimi naomba kutoa indhari kwamba kama hili lipo basi Mhe. Waziri alisimamie kuona kwamba hizi pesa zilizotolewa zinafanyiwa kazi iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka niingie kidogo kwenye Baraza la Manispaa ukurasa wa 57. Mhe. Spika, naomba niunge mkono hoja walizotoa Waheshimiwa waliopita kwamba Baraza kwa kweli limeshindwa kufanya usafi wa mji na naomba nithibitishe hilo kwa kuwa na wao wenyewe wanajua kwamba wameshindwa wamesema limekusanya na kuzoa taka wastani wa 25,920 sawa asilimia 45, hawazoi hata nusu ya taka ambazo mji unatoa. Lakini niwashukuru Baraza hili kwa kulijua hilo na wakaamua kuja na mikakati mipya kuwa katika malengo yao waliyojipangia mwaka huu wana mkakati wa kutekeleza mpya katika uzoaji wa taka. Mhe. Spika, nilikuwa naomba Baraza la Manispaa wabadilishe kila mikakati itayowezekana ilimradi mji uwe msafi.

Nikitoka hapo naomba niwashauri Baraza la Manispaa kwamba katika huo mkakati mpya wa uzoaji taka wangeanzisha *system* ya kuzoa taka usiku sio asubuhi watu wanakwenda makazini wao ndio wanainamisha migongo barabarani wanafagia.

Lakini pia katika huo huo mkakati wangeweka *dustbin* ndogo ndogo kwenye miji ili zile taka ndogo ndogo za mikononi watu wawe wanatupa kwenye zile *dustbin* ambazo watakuwa wanaweka.

Mhe. Spika, nikiendelea hapo hapo Baraza la Manispaa nilikuwa nataka kuzungumzia ajira za hawa watu wanaofagia miji yetu. Mhe. Spika, Baraza la Manispaa lina tabia ya kukusanya watu wakawajengesha taifa kwa kuwazolesha taka miezi miwili mitatu, lakini ajira zinapokuja wanachukua watu wengine wanawaweka katika zile ajira. Mhe. Spika hii sio haki tunaomba Baraza la Manispaa wanaowajengesha taifa ajira zikitoka muwapatie ajira zao.

Mhe. Spika, sasa niingie katika taa za barabarani. Mhe. Spika, tunapofuana macho kwa kuendesha *full light*, tatizo taa za barabarani haziwaki. Ki ukweli nawaomba Baraza la Manispaa nimeona wamekuja na mkakati wa kuimarisha taa za barabarani naomba kama wana mkakati huo basi wauzingatie ili bajeti inayokuja angalau watuelezee wamefikia wapi katika mkakati huu na tuone miji yetu inang'ara kwa taa za barabarani.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, katika buku kubwa la makadirio hili linaloonesha vifungu fungu la Manispaa halimo, sijui sikuperuzi vizuri au vipi, lakini naomba Mhe. Waziri akija atupe maelezo kwa nini fungu la Manispaa katika buku kubwa halimo.
Mhe. Spika, kwa kumalizia Waswahili wanasema 'Mcheza kwao hutunzwa'. Naomba niingie katika Halmashauri ya Kusini na Halmashauri ya Wilaya ya Kati. Nianze na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini ukurasa wa 64. Naipongeza Halmashauri hii kwa kuvuka lengo lao la kukusanya mapato na kufikia asilimia 116 natoa indhari kwamba wajitahidi makusanyo hayo yawafikie walengwa ambao ni wananchi kwa kuwasogezea huduma muhimu za jamii.

Mhe. Spika, nikimalizia hapo sasa niingie Halmashauri ya Kati kwa kuipongeza pia kwa kutoa huduma kwa jamii lakini niwashauri kwamba wawe wanajipangia malengo ambayo wataweza kutimiza. Bajeti ya mwaka jana walijiwekea lengo la kukusanya mapato kiasi fulani lakini hawakufikia lengo lile na bajeti ya mwaka huu hivyo hivyo wamejiwekea lengo lile lakini hawakufikia. Kwa hivyo, nilikuwa nawashauri kwamba watafune watachokiweza kukitafuna wasi-*bite what they can not chew*.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, nilikuwa naomba tu katika huu utaratibu wa ukusanyaji wa mapato angalau wangekuwa wanatuelezea hivyo vianzio vya mapato ambavyo wanakusanya, isijekuwa kwamba Wawakilishi tunapitisha bajeti hapa kwamba wanakwenda kukusanya kiasi fulani kumbe wakifika huko wanawanyonga wananchi. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kufika katika hali ya uzima na salama, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii.

Mimi Mhe. Spika, nitagusia gusia tu kwa sababu mengi yameshazungumzwa. Lakini nimepata mambo kumi ya msingi yanayopaswa kuyazingatia, sitoyasoma yote nitasoma nambari mbili, tuweke maslahi ya taifa mbele kuliko maslahi yetu binafsi. Nakifunga hiki cha mambo kumi, hayo nitakuja kuyaelezea kila wizara itakapofika, lakini sasa hivi naelezea hii.

Mhe. Spika, kwanza niunge mkono mambo yote ambayo wameyazungumza wenzangu, lakini na mimi nataka niseme kwamba, kisiwa cha Pemba Mhe. Spika, kuna baadhi ya mambo hawatendewi haki na nayasema haya si kwa sababu ya ubaguzi nayasema haya kwa ushahidi. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri tena sana jirani yangu, ndugu yangu, mwenzangu, kwamba anapofanya suala la mgao wa aina yoyote basi Kisiwa cha Pemba akikumbuke kwa sababu na kile nacho ni kisiwa ambacho kinazalisha pesa nyingi sana kuletwa Zanzibar. Nitakuja kwenye Mabaraza yetu ya Miji.

Mabaraza yetu ya Miji yote ya Pemba hayatendewi haki, moja tulipandishiwa mshahara hapa lakini kuna *area* zao watu wa Unguja wamelipwa Wapemba wahajalipwa, aje anieleze Mhe. Waziri si hivyo na mimi nitakuwa mgumu kwa bajeti hii. Lakini pia magari hapa Unguja yapo ya kusombasomba taka kule Pemba gari lipo moja kule Wete litakaa litasomba taka siku moja wiki mbili limelala, aje anieleze ni sababu zipi ambazo baadhi ya mambo hayatendeki kule Pemba.

Mhe. Spika, nirudi kwenye mambo ya vikosi vyetu na mimi nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kuwapongeza vikosi vyetu vya SMZ. Vikosi vyetu vya SMZ Mhe. Spika, vinafanya kazi kubwa sana, kazi zozote ambazo ukielekeza

kwenye vikosi lakini ndio watu wa mwisho wanaoonekana hawana mana, wameeleza wenzangu na mimi nashajidia, tuwape haki zao kama ni vikosi vya SMZ. Kwa sababu askari ana mantiki yake.

Pemba amezungumza Mhe. Wanu Hafidh nyumba wanazolala vikosi vyetu kwa kweli ni uchafu. Hilo moja, lakini la pili jengine ni kwamba wanapotoa uhamisho kupeleka watu Pemba hawawapi pesa zao za uhamisho kwa nini tunauliza na nyumba kule hakuna na siku zote bwana askari hakai uraiani, askari anatengewa sehemu yake maalum hawezi kuwekwa uraiani. Sasa naiomba serikali kwa nguvu zake zote tuangalie vikosi vyetu vya SMZ tulivyonavyo tuhakikishe kila pahala tunawajengea nyumba zao za kukaa.

Nije katika suala la Manispaa nakwenda kidogo kidogo. Mimi nasema Manispaa shaghala baghala, mchafukoge, nathubutu kusema hivyo. Mimi nashangaa Mkurugenzi, Mstahiki Meya, Waziri mwenyewe, wanasafiri saa ishirini na nne hivyo kweli hawaangalii wenzetu wanafanya mipango gani ya kuweka mji wao safi. Wanakwenda wakikisoma nini kule, tunashindwa sisi Saateni ukienda hujulikani chochote uchafu watu hawakujipanga kukaa, ukija Mwanakwerekwe ndio huko. Sasa hivi hata gari kuingia kule ndani hazipati kuingia na watu wote mwenye maembe matano basi anaweka pale analipishwa. Namuomba Mhe. Rais tena namuomba kwa hekima na taadhima nakuomba Mhe. Rais ufanye ziara ya ghafla usitoe taarifa ukatembelee masoko yetu utizame uchafu uliopo.

Soko la mbogamboga, lile soko limejengwa kwa ajili yetu Wazanzibari na zamani ilikuwa pale mchele, maharage, yafikie kule, leo soko lile ukienda Mhe. Spika, utalionea huruma nguvu za wenzetu ambao wanatusaidia lakini hatuzithamini.

Mhe. Spika, nije katika *plan* ya mji nakuja hapa hapa Manispaa. Hivyo kweli huu mji wetu hauna *plan* Mhe. Spika? Mimi nauliza hauna *plan*? Kama hauna plani kwa nini hatufuati plani ya mji na hiki ndio kioo cha Zanzibar, mji wa Zanziar kioo chake ni mjini, leo ukienda hilo soko la Darajani pale hapasemeki lakini Mwenyezi Mungu anatulinda na mengi kwa sababu katupa uzima wa aina yake katika viwiliwili vyetu, tunapokula vitu hivi hatudhuriki Mhe. Spika. Namuomba Mhe. Waziri akae na wizara husika kuhusu *plan* ya mji pamoja na Manispaa. Sasa hivi watu wanajijengea tu ovyo.

Mhe. Spika, tuseme pale Skuli ya Darajani wamesema wenzangu unafika wakati kwa sababu hatukuwapangia *plan* na tulidanganya tukasema tutawapangia pahala pazuri tuwapeleke, matokeo yake Mhe. Spika, ukienda katika soko la Saateni pale kwa kweli utaona hata sijui ufanye nini. Namuomba sana Mhe. Waziri, tunamwita *doctor* kwa ajili ya uwezo wake. Asituvunje moyo. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, na mimi niseme kwamba mpaka nitakapopata maelezo mazuri ndio nitaiunga mkono hoja hii kwa yale ambayo nimeyachangia.

La mwisho Mhe. Spika, ninataka Mhe. Waziri aje aniambie Ikulu ya Wete ipo mikononi mwa nani. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ninaelewa ipo kwa nani. Hapa nitakamata kidogo kwa sababu tatizo letu tulilonalo tumerithi majengo mengi sana lakini *maintenance* hatuyafanyii. Ile Ikulu ya Wete ni historia Mhe. Spika.

Baada ya kusema hayo na mimi siungi mkono hoja mpaka nije nipate maelezo ya kina katika wizara hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kunipatia nafasi hii.
Kwanza ninataka nivipongeze vikosi vyetu. Mhe. Jussa kasema anaona fahari. Nimefurahi sana. Vikosi vyetu KMKM, Valantia, JKU, Chuo cha Mafunzo na askari wa *fire*, wote hawa wana kazi moja kuhakikisha wanalinda amani na utulivu ndani ya nchi hii.

Sasa Dr. Mwinyihaji kaongeza katika bajeti yake chakula kimepanda. Mimi ninasema kama kimepungua njoo kwangu nitaongeza, wapewe chakula washibe wawe na nguvu kuilinda nchi yetu. Hawa ndio tunaowategemea, sisi hatuna jeshi lakini Baraza lako Tukufu sura ya “Idara ya Maalum”.

Kutakuwa na Idara Maalum katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo kazi zake na shughuli zake zitakuwa kama zinavyoidhinishwa na sheria zinazohusika. Sheria tunazozitunga hapa. Lakini sasa vikosi hivi sasa kifungu 123(1) “Rais atakuwa Kamanda Mkuu wa Idara Maalum na atakuwa na uwezo wa kufanya chochote kile anachohisi kwa maslahi ya taifa”. Kamanda Mkuu maana yake nini Mhe. Spika. Maana yake ni *commander in chief*.

Juzi Misri kwa miaka 88 *Muslim Brotherhood* nafasi hawajapewa. Juzi wamepewa Rais lakini *commander in chief* wameambiwa hapana, hawajapewa. Kwa sababu *commander in chief* ndio taasisi tunayoikamata nchini kwetu Dr. Ali Mohamed Shein.

Sasa Dr. Shein Mhe. Spika, ameapa. Anasema Dr. Shein, nimeapa kulinda amani. Dr. Shein muungwana, mtekelezaji. Na tazama uungwana wake. Anasemaje? Anasema wakati nikiingia madarakani nimekabidhiwa nchi ikiwa na amani. Kwa hivyo sioni sababu ya hivi sasa kuogopa ama kuchelewa kulinda nchi kwa sababu ya maslahi ya Wazanzibari. Anakubali kama alipoingia madarakani tulimkabidhi amani. Baraza hili hili ndio tuliofanya Katiba hii.

Sasa Mhe. Spika, tumuachie Dr. Shein na Baraza la Mawaziri, Makamu wa Kwanza na wa Pili wa Rais wafanye kazi. Mwaka jana nilisema hii bajeti si yao wao hawa, kuanzia bajeti ya keshokutwa tuwaachie wafanye kazi wajenge nchi. Tuwatizame sasa.

Kwa sababu wao ni *front bench*, sisi ni *backbencher*. Lakini Mhe. Rais kasema hivi, "Migogoro ya ardhi ipo mikononi mwa viongozi". Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amesema mali ya ardhi imekuwa ni chanzo cha utata kuibuka kwa migogoro katika jamii ambapo mara nyingi Masheha na viongozi wa serikali za mitaa kuhusishwa moja kwa moja kuwa vinara wa migogoro hiyo.

Dr. Shein muacheni, Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Masheha, rafiki zangu msaidieni. Dr. Shein vitu viwili kakabidhiwa. Kakabidhiwa amani na Wakuu wa Mikoa na Wilaya hajawagusa, hajawafinya, kuweni waungwana, mlipeni wema, wengine wanaumwa kwa wasi wasi lakini aah! kawaachia. Hebu fanyeni utaratibu tunakuombeni na sisi viongozi wa Baraza hili kama tumo katika mambo haya ya ardhi basi tuache Mhe. Spika.

Leo sio siku ya ardhi lakini siku ya ardhi tutoe historia ya ardhi. Tumuachie Dr. Shein na Baraza lake la Mawaziri na sisi Wawakilishi tufanye kazi. Wakuu wa Mikoa na Wilaya mulichopata mushapata hebu acheni. Ninakuombeni kwa dhati kabisa ndani ya moyo wangu, wacheni hii serikali ifanye kazi.

Mhe. Spika, amani imetafutwa kwa taabu sana. Zanzibar haijawa na utulivu wa kisiasa, tangu mwaka 1957 mpaka 2010 Zanzibar haina amani, utulivu wa kisiasa, tumepigana Juni, tumeuwana tarehe 27 sijui Januari, hatuzikani. Tumefanya juhudi chini ya uongozi wako Mhe. Spika. Ukaunda kamati ya Baraza la Wawakilishi, busara zako na hekma zako ndio leo watu wakapata raha.

Dr. Shein kasema anaambiwa anaogopa, watu wamesema. Alifahamisha kuwa amani ya Zanzibari ni muhimu na atahakikisha anaeleza hilo bila ya kuogopa kutokana na kula kiapo cha Urais, hivyo wajibu wake ni kusimamia ili wananchi wawe katika utulivu. Amani ya Zanzibari bado ipo katika mabega yangu. Mimi ndiye Rais wa Zanzibar niliyeapa kulinda nchi na nitahakikisha amani ya Zanzibar inabakia kama ilivyo na ninasikia kuna maneno mengi yanasemwa eti nchi imenishinda, naogopa. Simuogopi mtu yeyote zaidi ya Mwenyezi Mungu, nitawalinda wanyonge wote wa Zanzibar.

Sasa ninataka kwa ruhusa yako Mhe. Spika, niwaulize Wajumbe wako. Tutamsaidia Dr. Shein katika hili, tutamlinda kwenye uwoga. Sisi kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi tunamuhakikishia ukamwambie kuwa Baraza la Wawakilishi tupo nyuma yake asiogope. Kwa sababu Baraza hili ni ngome ya wananchi. Ninasema tena nenda ukamwambie Baraza la Wawakilishi lipo nyuma yake, watu wanasikia kwa sababu Baraza hili ni ngome. Sasa tumuachie na timu yake ifanye kazi na sisi sasa tutizame nchi inavyokwenda.

Mhe. Spika, leo sina mengi ya kusema lakini niliona nitoe hii habari ambayo ni muhimu. Lakini ninataka kusema lugha, ndugu zangu Wawakilishi *backbenchers*, mimi sio mkubwa wao lakini ni mzee wao. Lugha zetu watu wanatusikiliza. Baraza la Wawakilishi halitungi sheria za kutukandamiza na hata Tume ya Nyalali imetaka sheria 40 zifutwe za kukandamiza Zanzibar haimo. Kwa hivyo tuzungumze lugha ya kiistaarabu lakini tusiseme kuwa sheria za kukandamiza. Zanzibar hakuna sheria za ukandamizi.

Sheria za Zanzibar zote alizozitunga ni Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ndiye AG wa mwanzo huyo na nyengine. Kwa hivyo tujitahidi na lugha. Vile vile tuheshimiane, tusiitane majina ya mabaya, wezi, mafisadi, hakuna hapa. Sisi sote ni wamoja tunakosoana, tunaambizana lakini sote lengo letu ni moja kuijenga Zanzibar yetu.

Zanzibar ni nchi, Zanzibar dola. Ndio maana nikasema vikosi hivi ndivyo vikosi tunavyovitegemea kulinda. Kwa hivyo tuwaunge mkono, tuwasaidie sana na sisi tuwe nao pamoja.

Mhe. Spika, leo nimeona niseme hayo machache. Nilitaka niwahakikishie Waheshimiwa Mawaziri sisi na wao ni wamoja na ninawapongeza kwa kazi wanayoifanya waendelee, wakikwama sisi tupo.

Kwa hayo Mhe. Spika, ninamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wa Zanzibar Dr. Shein maisha marefu, afya njema na oktoba 2012 tumkabidhi bendera ya Makamu Mwenyekiti wa CCM na aongoze nchi. Kwa hayo machache ahsante sana.
Mhe. Spika, nimesahau ninaunga mkono hoja kwa sababu jimbo langu ni Ikulu, ingekuwa balaa sana. Ninaunga mkono Ali Mzee Ali na jimbo langu la Ikulu pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi Baraza ninampongeza kwa bango kitita aendelee nalo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ninashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mimi moja kwa moja nianze tu na amani. Mhe. Spika, nchi yetu ni nchi ya amani na wajibu ni kulinda amani. Amani haiwezi kupatikana mpaka haki iwe inatendeka.

Mhe. Spika, kwanza ninashukuru kwa wenzangu waliochangia kuona kuwa kumbe katika majimbo ya wenzetu wale watu wanaostahiki kupiga kura wanapatiwa haki yao mia juu ya mia.

Wamezungumza hapa lakini Mhe. Spika, mimi ninasikitika sana kuna baadhi ya majimbo na moja ikiwa ni jimbo langu, kuna watu wameshatimia umri wa miaka 18 na hawa ni lazima wapatiwe haki yao ya kupiga kura wakati wa sifa zote zinazostahiki. Wanapokwenda kwa Sheha ili kupatiwa kitambulisho cha Mzanzibari, Sheha anasema kuwa fomu zimemalizika, wakati fomu zenyewe ni kutolewa kopi tu na shughuli ikaendelea kama kawaida.

Sasa ikiwa kuna sehemu kuna watu wote wanapewa na wengine hawapewi Mhe. Spika, hili ni tatizo, tena ni tatizo kubwa sana. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Spika, kwanza kwenye vitambulisho hivi na umhimu wake tunavijua tuone kuwa wananchi wamefanyiwa haki. Kwa sababu hizi kauli ni mbili. Kuna wengine wanasema wote wanapata, kuna wengine wanasema kuna wengine hawapati. Mimi ninafikiri ipo haja ya kuundwa kwa makusudi kufuatilia suala hili kule ambapo matatizo haya tunaendelea nayo.

Jengine Mhe. Spika, nizungumze kuhusu soko la Mwanakwerekwe. Hili soko ninashukuru limejengwa kwa makusudi ya kutoa huduma lakini sasa limeshazidiwa na huduma. Watu wote hata wanaotoka huku mjini huwa wanakimbilia kwenye soko lile. Matokeo yake asubuhi watu hujazana, gari, vespa na vyombo vyote vyengine havina pa kupita. Msongo ni mkubwa sana na watu wanaoongezeka wanakwenda kule kwa mahitaji.

Mimi ninamuomba Mhe. Waziri aniambie atafanya nini kuona kuwa ametafuta mahala pa kuongeza soko ili huduma iwe inafanyika ipasavyo. Hilo ni la pili.

Jengine kwa sababu ya wakati Mhe. Spika, tumeona Manispaa moja kati ya kazi zake ni kuweka usafi. Lakini kwenye kitabu wamesema kuwa wamefanikiwa kukusanya asilimia 45 tu ya takataka. Takataka ni uchafu, hizi asilimia zilizobakia 55 ziko katika kukusanywa na chombo gani na hakuna, kwa nini wakashindwa kufanya kazi yao ipasavyo.

La mwisho Mhe. Spika, kwa sababu wakati hakuna ni kuwa Baraza la Mji Wete limetoa mipango mizuri itakayofanya katika kipindi hiki cha fedha cha mwaka 2012/13. Ningeliomba basi kwa makadirio ya hayo shilingi milioni hamsini ambazo wamejipangia kukusanya, pia kile kipande kidogo kutoka kwenye barabara ya Afisi ya Mkoa mpaka Mafunzo na chini kidogo kule pwani kitengenezwe ili watu waweze kukitumia ipasavyo.

La mwisho kabisa kwenye ukurasa huu kuna makusanyo ya makadirio ya mwaka uliopita na mwaka ujao ambapo kuna Halmashauri nyengine zimekusanya zaidi ya asilimia iliyokusudiwa lakini nyengine hazikufika kabisa. Nikitaka kujua kwa nini hizi nyengine hazikufika.

Mhe. Spika, ninashukuru.

Mhe. Spika: Mhe. Salim ninakushukuru sana na ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote tumemudu kuwasikiliza Waheshimiwa 25, wamebakia Wajumbe kama 10.

Tutaangalia hali itakavyokuwa kesho asubuhi baada ya kipindi cha maswali na kutakuwa na Kauli ya Serikali kutoka Wizara ya Afya. Lakini ninakusudia nije kumuomba Mhe. Waziri kiasi saa tano aje afanye majumuisho, nikiamini shughuli ya maswali na Kauli ile ya Serikali kutoka Wizara ya Afya itakuwa tumemaliza.

Kama muda utakuwepo kuna baadhi ya Mawaziri wameomba na ninategemea na wao wasaidie kwa upande wa serikali akiwemo Mhe. Haroun Ali Suleiman na baadhi ya wengine wawili watatu.

Kwa hivyo nikuombeni Waheshimiwa Wajumbe msingi michango ni mingi, siwezi kusema kwamba inatosha au laa, lakini ni mingi karibu maeneo mengi tumepita. Marejeorejeo ni dalili ya kuonesha kwamba michango ni mingi ya kutosha. Sasa kama kesho hatujapata muda wa kuita angalau wajumbe wawili watatu, nichukue nafasi hii kuwaomba mapema na niwaombe basi turidhike na ile michango tumeipokea. Lakini kimsingi shughuli hii ili twende na ratiba yetu Mwenyezi Mungu tumalize kesho kipindi cha asubuhi.

Basi Waheshimwa Wajumbe nikushukuruni kwa mashirikiano makubwa ya kuendesha shughuli zetu, na sasa basi niakhirishe kikao hiki hadi kesho saa tatu za asubuhi.

(Saa 1.45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 03/07/2012 saa 3.00 asubuhi)